UCHANGANUZI WA USIMULIZI KAMA MTINDO KATIKA NYIMBO ZA BAHATI BUKUKU

A CRITICAL ANALYSIS OF NARRATION AS A STYLISTIC DEVICE IN BAHATI BUKUKU'S SONGS

NA

ASIGE NELSON ABOGE

TASNIFU HII IMEWASILISHWA KATIKA IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA ZA KIAFRIKA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI YA CHUO KIKUU CHA KENYATTA

MACHI, 2021.

UNGAMO

TASNIFU HII NI KAZI YANGU MWENYEWE NA HAIJATOLEWA KWA MAHITAJI YA SHAHADA KATIKA CHUO KINGINE.

Sahihi……. **Tarehe……**

ASIGE NELSON ABOGE

C50/NKU/CE/26003/2014

TASNIFU HII IMEWASILISHWA KWA IDHINI YETU KAMA WASIMAMIZI WALIOTEULIWA NA CHUO CHUO KIKUU CHA KENYATTA.

Sahihi…….. **Tarehe……**

Dr. PAMELA M. NGUGI

Sahihi……. **Tarehe……**

PROF. PETER GITHINJI

TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa babangu mzazi Isaac Kavai Asige. Maombi, heri njema na ushauri ulionipa ulinipa ari ya kukamilisha kazi hii. Mungu akubariki na kukupa maisha marefu ili unufaikie matunda ya kazi hii.

SHUKRANI

Shukrani zisizopimika zimwendee Mwenyezi Mungu kwa mengi aliyonipa ikiwemo uhai, afya njema, baraka zake, neema pamoja na uwezo wa kukamilisha kazi yangu. Atukuzwe milele.

Napenda vilevile kuwashukuru wasimamizi wangu, Prof. Githinji Peter na Dkt. Ngugi Pamela kwa kila hatua ya kazi hii. Msaada ambao nilipokea kutoka kwenu ikiwemo fikra, maarifa, mapendekezo na mwongozo ulinisaidia katika kuafikia malengo yangu. Vilevile, masahihisho kutoka kwenu yalikuwa na msingi mwema na msaada mkubwa katika kazi hii na maisha yangu kwa ujumla. Shukrani za dhati kwa uvumilivu wenu na Mola azidi kupanua mipaka yenu.

Shukrani za dhati waaidha ziwaendee wahadhiri wote katika idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika. Niliweza kupata maarifa na ujuzi mwingi kutoka kwao. Shukrani vilevile ziwaendee wahadhiri walionifunza katika Bewa la Nakuru wakiwemo Prof. Onyango Ogolla, Prof. Githinji Peter pamoja na Dkt. Mayaka kwa msaada wao. Nilipokea uzoefu wa matarajio ya kozi kutoka kwao. Mungu awabariki sana.

Wanafunzi wenzangu tuliokuwa pamoja katika Bewa la Nakuru pia wanastahili shukrani nyingi. Tulisaidiana kama ndugu na kuhimizana katika kila hatua ya elimu yetu. Msaada wote niliopata kutoka kwao, kimaarifa na pia kifedha, ulinijenga kielimu. Siwatum Zipporah, Mwangi Peter, Mose Ann, Gilbert Ng'etich pamoja na Maritim Joel, ahsanteni sana kwa kunifaa kwa hali na mali. Mungu awabariki. Rafiki yangu wa dhati, Julia Ogali, ninakupa shukrani sizizopimika. Umekuwa wa msaada kwangu sana katika upigaji taipu na urudufishaji wa kazi yangu. Mwenyezi Mungu azidi kukupa moyo uo huo wa msaada kwa wengine. Ninakupenda dadangu.

Ninatoa shukrani zisizopimika kwa wazazi wangu wapendwa, Bwana Isaac Kavai Asige na Bi Anna Jerono Kavai kwa kunitia ari ya kuendeleza masomo yangu zaidi ya shahada ya Digrii. Maombi, subira na uvumilivu wenu haupimiki. Ninawapenda sana. Asanteni sana.

Ninawashukuru ndugu zangu wapendwa David Asiji, Caroline Javaya, Elvis Chogo pamoja na Dominic Changilwa kwa kunipa moyo na kwa heri njema iliyonifikisha nilikofika masomoni. Zaidi, namshukuru dadangu mpendwa Caroline Javaya kwa kunifaa kwa hali, mali na makao bila kusahau msukumo wako wa kila mara wa kutaka kuniona nimefanikiwa. Ninakupenda sana.

Mke wangu na rafiki wa dhati, Loraine Nasimiyu Aboge, isingekuwa mawaidha yako, kunihimiza kila mara na kunifufua moyo katika hali mbaya, huenda nisingekamilisha utafiti huu. Wewe ndiye wangu Lazizi. Ninakupenda sana.

Kwa wanangu wapendwa, Chelsea Ndori Aboge na Damian-Lucas Kavai Aboge, yote ninayoyafanya ni ili niweze kuwa mzazi bora kwenu. Asanteni sana kwa kunipa ari ya kujiendeleza, ata iwapo hamfahamu yanayoendelea kwa udogo wenu wa sasa. Ninawapenda sana.

IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza vipengele vya usimulizi katika nyimbo teule za Bahati Bukuku. Nyimbo aghalabu huwa na mbinu za kimtindo ambazo huwasilisha jinsi maudhui yalivyojitokeza katika nyimbo hizo. Uhakiki huu ulijikita katika vipengele vitatu; mitindo ya simulizi kwa kuzingatia ploti na wakati, suala la maudhui pamoja na uchanganuzi wa sauti ya usimuliaji na mahusiano ya wakati wa usimulizi. Maswali ya utafiti yalikuwa; ni kwa njia gani mbinu ya masimulizi katika uimbaji imejitokeza katika nyimbo za Bahati Bukuku kuzingatia ploti na wakati? Je, mbinu ya usimulizi imesaidia vipi katika kutambua maudhui katika nyimbo za Bahati Bukuku? Je, vipengele vya sauti ya usimuliaji na mahusiano ya wakati wa usimulizi imedhihirika vipi katika nyimbo teule za Bahati Bukuku? Utafiti huu una malengo matatu ambayo ni; kueleza jinsi usimulizi katika nyimbo imejitokeza kwa kuzingatia vipengele vya ploti na wakati, kudhihirisha usimulizi kama njia ya kuwasilisha maudhui na pia kufafanua jinsi vipengele vya sauti ya usimuliaji na mahusiano ya wakati wa usimulizi vimejitokeza katika nyimbo teule za Bahati Bukuku. Nadharia iliyotumika ni ya Naratolojia inayojumuisha usimulizi katika tanzu za fasihi. Nadharia hii hujumuisha usimulizi katika tanzu kama vile nyimbo, mashairi, maghani na kadhalika. Suala kuu katika nadharia hii ni simulizi na usimulizi na pia uhakiki wa ploti kama kipengele muhimu cha usimulizi. Uteuzi wa sampuli kimaksudi ulitumiwa katika ukusanyaji wa data pale ambapo uteuzi wa nyimbo zilizotumiwa katika utafiti ulitokana na kanda za video tepetevu za nyimbo za injili za Bahati Bukuku. Data yenyewe ilinakiliwa kwa kurejelea malengo ya utafiti na msingi wa nadharia husika. Utafiti wa maktabani ulitumika katika kukusanya data kupitia usomaji wa vitabu, majarida, makamusi, tasnifu za awali pamoja na makala ya mtandaoni yaliyosaidia katika kuafikia malengo ya utafiti huu. Hii ni baada ya kununua albamu zinazosheheni nyimbo za Bahati Bukuku, pamoja na kutoa nyimbo zingine mtandaoni, kuzisikiliza na kuzihakiki kulingana na malengo ya utafiti. Utafiti huu utawafaa watafiti wa baadaye katika kazi zao za kuhakiki mada zinazohusiana na utafiti huu. Vilevile utafiti huu utachangia katika kuonyesha jinsi mbinu ya kimtindo ya usimulizi inavyoweza kufanikisha uwasilishaji wa maudhui kwa wasikilizaji wa nyimbo hizi kwa kuzingatia nyimbo zilizoimbwa kwa kutumia mtindo huu. Hali hii itafanikishwa kupitia hadithi ambazo zimeweza kujitokeza katika nyimbo za Bahati Bukuku ambazo zimeweza kuwasilishwa kwa kaida za utambaji wa hadithi. Utafiti huu pia utawafaa watafiti wa baadaye ambao tahakiki zao zitaandikwa kwa kutumia nadharia ya naratolojia.

ABSTRACT

This study sought to discuss the narrative aspects in Bahati Bukuku's songs, a gospel singer based in Tanzania. Songs always have stylistic devices that portray how themes of the songs are communicated. The study focused on three main aspects; narrative themes, narrative style and narrative time. The research questions were; in what way is narration portrayed as a stylistic device in Bahati Bukuku's songs based on plot and narrative time? In what way does this stylistic device assist to discover the themes communicated in Bahati Bukuku's songs? How do the narratives in Bahati Bukuku's songs illustrate narrative levels and voices? The research was guided by these objectives; to explain how the style of narration in a song is illustrated in Bahati Bukuku's songs based on plot and narrative time, to discover the contribution of this stylistic device in discussing the themes in the selected songs and to explain the aspect of narrative levels and voices in Bahati Bukuku's songs. The study was mainly guided by the theory of Narratology which generalizes narration in all aspects of literature including songs, poems and stories among others. The theory also evaluates the plot as an important aspect of narration. Purposive sampling technique was used to collect data where the sampling of the songs that were used in the research were retrieved from a wide variety albums released by Bahati Bukuku. Library research was useful in achieving the objectives of this research through reading of books, journals, dictionaries, completed thesis and other online resources. This was after purchasing Bahati Bukuku's music albums, and also downloading her most recent tracks, listening and evaluating them according to the objectives of the research. This research will be useful to future researchers in the line of this study. In addition, this research establishes how the style of narration in a song can go a long way in helping listeners and researchers understand the themes communicated by Bukuku in her songs. This will succeed through the narratives that have been enjoined in Bahati Bukuku's songs that have been presented by considering aspects of narration. This research will also be useful to future researchers whose analysis will adopt the theory of Narratology.

UFAFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU

Naratolojia: Nadharia ya uchanganuzi wa muundo wa simulizi au hadithi.

Usimulizi: Uelezaji wa matukio katika hadithi.

Ploti: Mfululizo wa matukio yanayojenga hadithi na namna matukio hayo yanavyosababishana.

Umara: Idadi ya mara tukio limeweza kutokea katika hadithi au matini.

Usimulizi mosi: Hali ya tukio kutukia mara moja na kusimuliwa mara moja.

Usimulizi rudufu: Hali ya tukio kutukia mara moja ila linasimuliwa zaidi ya mara moja.

Usimulizi banifu: Hali ya tukio linalotukia mara kadhaa kusimuliwa mara moja.

Muda: Ni uhusiano wa kiwakati katika hadithi.

Muhtasari: Hali ambapo kasi ya usimulizi huharakishwa.

Udondoshi: Hali ya kasi ya masimulizi kuwa juu sana na maelezo fulani kuachwa katika matini fulani.

Onyesho: Njia ambayo huleta uigizaji katika matini ya usimulizi.

Mtuo: Hali ya msimulizi kuingiza maelezo ya pembeni katika hadithi yake. Maelezo haya huenda yana uhusiano au hayana uhusiano na hadithi.

Mpangilio: Uhusiano baina ya mfuatano wa matukio katika hadithi.

Analepsia: Mbinu ambapo masimulizi ya matukio yaliyotukia nyuma yanasimuliwa kabla ya yale yaliyotangulia kutendeka.

Prolepsia: Mbinu ya usimulizi ambapo msimulizi husimulia matukio yatakayotukia baadaye lakini anayasimulia wakati huo.

Maudhui: Ujumbe wa jumla unaojitokeza katika kazi ya fasihi.

Hadithi: Habari ya mambo yaliyotulia.

Wakati- hadithi: Muda unaotumika katika hadithi kuanzia mwanzo hadi mwisho.

Wakati- matini: Wakati unaochukua matini kusomwa.

Usimulizi kabla: Kipengele kinachoeleza usimulizi wa matukio kabla ya kutukia kwake.

Usimulizi sawia: Usimulizi ambao matukio yake yanasimuliwa jinsi yanapotendeka.

Usimulizi baadaye: Usimuliaji wa matukio baada ya kutukia kwake.

Usimulizi zongomezi: Hali ambapo muda wa usimulizi na muda wa utendaji huchangamana.

YALIYOMO **UKURASA**

UNGAMO……ii
TABARUKU…… iii
SHUKRANI……..iv
IKISIRI……v
ABSTRACT.....vi
UFAFANUZI WA ISTILAHI……vii
YALIYOMO……...viii
SURA YA KWANZA…….. 1
UTANGULIZI……..1
1.0 Usuli wa mada……..1
1.1 Wasifu wa Bahati Bukuku……... 3
1.2 Suala la utafiti…….. 5
1.3 Maswali ya utafiti…… 5
1.4 Malengo ya utafiti……6
1.5 Sababu za kuchagua mada ya utafiti……6
1.6 Upeo na mipaka ya utafiti……8
1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada……...8
1.7.1 Yaliyoandikwa kuhusu nyimbo…… 8
1.7.2 Yaliyoandikwa kuhusu usimulizi……..11
1.8 Msingi wa nadharia……..14
1.9 Mbinu za utafiti……19
1.9.1 Sampuli……20
1.9.2 Ukusanyaji wa data…….. 20
1.9.3 Uchanganuzi wa data……21
1.9.4 Uwasilishaji wa matokeo……..21
SURA YA PILI…… 22
USIMULIZI KATIKA NYIMBO ZA BAHATI BUKUKU…… 22
2.0 Utangulizi…….22
2.1 Dhana ya usimulizi…….. 22
2.2 Ploti…… 23
2.2.1 Utangulizi maalum……24
2.2.2 Tamati maalum……. 28
2.2.3 Nafasi ya mhusika mkuu katika usimulizi …… 30
2.2.4 Kilele cha usimulizi…….. 35
2.3 Kipengele cha wakati……...39
2.3.1 Kipengele cha umara…….40
2.3.1.1 Usimulizi mosi……...40
2.3.1.2 Usimulizi rudufu…… 42
2.3.1.3 Usimulizi banifu…….43

2.3.2 Kipengele cha muda……..44
2.3.2.1 Kigezo cha muhtasari……44
2.3.2.2 Kigezo cha udondoshi……46
2.3.2.2.1 Udondoshaji bayana……46
2.3.2.2.2 Udondoshaji usio wazi……47
2.3.2.2.3 Udondoshaji batini……..48
2.3.2.2.4 Udondoshaji dhahiri……49
2.3.2.3 Kipengele cha onyesho…….. 49
2.3.2.4 Mtuo……...51
2.3.3 Mpangilio……..52
2.3.3.1 Analepsia……53
2.3.3.1.1 Analepsia ya nje……..53
2.3.3.1.2 Analepsia ya ndani……..54
2.3.3.1.3 Analepsia mseto……..55
2.3.3.1.4 Analepsia wasifu……55
2.3.3.1.5 Analepsia tawasifu……..56
2.3.3.2 Prolepsia……57
2.3.3.2.1 Prolepsia ya ndani……...57
2.3.3.2.2 Prolepsia ya nje……...57
2.3.3.2.3 Prolepsia mseto……... 58
2.3.3.2.4 Prolepsia tawasifu……... 59
2.3.3.2.5 Prolepsia wasifu……..59
2.4 Hitimisho…… 60
SURA YA TATU…… 61
MAUDHUI KATIKA NYIMBO TEULE ZA BAHATI BUKUKU…….. 61
3.0 Utangulizi……61
3.1 Maudhui na uwasilishaji wake katika nyimbo za Bahati Bukuku…….. 61
3.2 Aina za maudhui katika nyimbo teule za Bahati Bukuku……63
3.2.1 Imani ya dini…… 63
3.2.2 Unafiki…….. 69
3.2.2.1 Unafiki wa mumewe msimulizi……69
3.2.2.2 Unafiki wa kimada wa mumewe msimulizi……...70
3.2.2.3 Unafiki wa ndugu na jamaa……... 71
3.2.2.4 Unafiki wa mawifi wa msimulizi……...72
3.2.3 Msamaha……...74
3.2.4 Nafasi ya marafiki katika maisha ya mja……..76
3.2.5 Ushirikina……..79
3.2.6 Anasa……81
3.2.7 Nafasi ya mwanamke katika jamii……83
3.3 Hitimisho…… 84

SURA YA NNE…… 86
SAUTI YA USIMULIAJI NA MAHUSIANO YA WAKATI WA USIMULIZI KATIKA NYIMBO TEULE ZA BAHATI BUKUKU…… 86
4.0 Utangulizi…….86
4.1 Sauti ya usimuliaji……86
4.1.1 Usimulizi wa nafsi ya kwanza…….. 87
4.1.2 Usimulizi wa nafsi ya pili……91
4.1.3 Usimulizi wa nafsi ya tatu…….95
4.2 Mahusiano ya wakati wa usimuliaji…….99
4.2.1 Usimulizi baadaye……100
4.2.2 Usimulizi kabla……102
4.2.3 Usimulizi sawia……104
4.2.4 Usimulizi zongomezi…… 106
4.3 Hitimisho……. 107
SURA YA TANO……. 109
MUHTASARI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO……...109

5.0 Utangulizi……109
5.1 Muhtasari wa utafiti……109
5.2 Matokeo ya utafiti……112
5.3 Mchango wa utafiti…….. 116
5.4 Changamoto zilizokabili utafiti……116
5.5 Mapendekezo ya utafiti……117
5.6 Hitimisho……. 118
MAREJELEO…….. 119

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.0 Usuli wa mada

Utafiti huu ulihusu usimulizi katika nyimbo. Kieti (1990) anafafanua kuwa usimulizi ni hali ya kutoa ama kutamba hadithi hasa kutokana na mtazamo wa msimuliaji. Mbinu hii hutumia hadithi ikidhamiria kuboresha uelewaji wa maudhui anayotaka kuwasilisha msanii. Usimulizi ni njia ya mawasiliano kati ya mwandishi, msomaji, msimulizi na msimuliwa. Matukio katika usimulizi yanaweza kuwa ya kweli kama yalivyotukia au ya kubuni. Matukio katika usimulizi huwa yamefuatana na yanayohusiana.

Utafiti huu ulifanywa ili kubainisha jinsi vipengele muhimu vya usimulizi vimejitokeza katika nyimbo lengwa. Vipengele hivi ambavyo vimefanikisha utafiti huu ni kama: ploti, wakati, maudhui, sauti ya usimuliaji na wakati wa usimulizi. Usimulizi ni njia ya mawasiliano kati ya msimulizi na msimuliwa. Simulizi nayo ni maelezo kuhusu matukio ya kihalisia au ya kubuni ambayo msimulizi huchukua kuwa ya kusisimua na tena yenye kuwa na umuhimu kwa hadhira kwa sababu ya dhima zake mbalimbali. Masimulizi huundwa kwa njia ya kusimulia matukio yenye uhusiano wa moja kwa moja na unaoonyesha mfuatano fulani wa matukio uliosukwa ili kuafikia malengo ya mtunzi.

Kwa mujibu wa Gikandi (1987), usimulizi ndiyo nguzo kuu katika fasihi ya Kiafrika. Maoni mengine yanatolewa na Toolan (1988) kwamba chochote binadamu afanyacho katika maisha yake kinahusiana na usimulizi. Hivyo basi, usimulizi unajitokeza kuwa muhimu sana katika maisha kwa ujumla.

Ufafanuzi wa Mohammed (1995) unaeleza chimbuko la usimulizi kuwa fasihi ya kusimuliwa. Usimulizi hurejelea jinsi hadithi inavyowasilishwa na hivyo inajikita katika kiwango cha diskosi, ambayo kulingana na Genette (1980:93):

"*Ni ile hali ya kuendeleza hadithi katika uwasilishaji wa simulizi*." (Tafsiri yangu)

Wataalamu mbalimbali wameibuka na maelezo tofauti kuhusu usimulizi. Chatman (1990) anafafanua usimulizi kama hali ya kutoa simulizi. Kwa mujibu wa *Kamusi ya Fasihi* (2003), usimulizi ni uelezaji wa matukio katika hadithi. Mlacha (1991) kwa upande wake anaeleza usimulizi kama uhusiano uliopo baina ya msimulizi na hadithi yenyewe.

Kuna wataalamu vilevile ambao wamegawa usimulizi katika aina tofauti. Kwa mfano, Hawthorn (1985) alihakiki aina iitwayo usimulizi maizi. Anaeleza usimulizi maize kuwa kongwe kuliko simulizi nyinginezo. Aghalabu, matukio katika usimulizi huu huwa hayamhusu msimulizi: yaani haishiriki lakini akiwa muumba wake, anaelewa kila kitu kinachotendeka hadithini.

Mbali na usimulizi maizi, pia kuna usimulizi wa nafsi ya tatu. Katika usimulizi huu, mwandishi anasimulia akitumia nafsi ya tatu lakini anajikita zaidi katika mhusika mmoja tu. Anajibana na kujipunguzia anayoyafahamu kwa kudhihirisha ufahamu wa mhusika mmoja pekee yake. Kulingana na Mohammed (1995), usimulizi huu humpa mhusika mmoja nafasi kubwa katika usimulizi, na kwamba, sio sharti masimulizi yote yatoke mdomoni mwa msimulizi. Mara nyingi, haya hujitokeza kupitia dayalojia kati ya mhusika na wahusika wengine, ama kupitia uzungumzi nafsia wa mhusika mwenyewe. Mohammed (keshatajwa) anafafanua aina nyingine ya usimulizi: ule wa nafsi ya kwanza. Anafafanua usimulizi huu kuwa ule unaotumia wingi wa viambishi vya nafsi ya kwanza "ni" katika umoja na "tu" katika wingi. Vilevile, anaeleza kuwa kiwakilishi huru

“mimi” hutumiwa kwa mno. Hata hivyo, anaonya kuwa msimulizi anapotumia kiwakilishi huru na viambishi vya nafsi ya kwanza kwa wingi, huenda wakaichosha hadhira, iwe hai au tuli.

Kazi nyingi za kitaaluma ambazo zimefanywa hapo awali kuhusu mada ya usimulizi zimejihusisha na fasihi andishi. Usimulizi umetafitiwa katika nyanja za tamthilia, hadithi fupi na ushairi andishi. Tafiti za Vonyoli (2004), Magaju (2004) na Bakari (2008) zilijihusha na fasihi andishi. Utafiti wa Arege (2012) ndio ulioegemea katika fasihi simulizi kwa kuzingatia utenzi wa *Rasi ‘lghuli*. Utafiti huo ulizingatia wakati-hadithi, uhusika pamoja na viwango vya usimulizi. Kwa hivyo, kuna haja ya kutafiti uwanja wa usimulizi kwa kurejelea kipera cha nyimbo katika fasihi simulizi.

Dhana za wakati na mahali zina umuhimu mkubwa katika masimulizi. Barry (1995) anafafanua kuwa matukio husimuliwa katika wakati na mahali fulani. Kadhalika, matukio yanapaswa yafuatane kimfululizo kulingana na kutokea kwao kiwakati. Kwa hivyo, kwa mujibu wa utafiti huu, usimulizi ni uelezaji wa matukio katika hadithi.

Hivyo basi, ni muhimu kubainisha nafasi ya usimulizi katika uhakiki wa nyimbo kwa kuzingatia utunzi, ufasiri, uwasilishaji na uhakiki wa nyimbo ambazo zimesheheni mbinu ya usimulizi.

1.1 Wasifu wa Bahati Bukuku

Msanii ndiye huwa kiini cha kazi yoyote ya kisanaa. Hii ni kwa kuwa yeye ndiye muumba wa kazi hiyo. Hivyo, kuna haja ya kumwelewa msanii, maisha yake, utamaduni uliomlea pamoja na kanuni za kitamaduni zilizomwathiri ili kuweza kuhakiki kazi yake kikamilifu.

Katika mahojiano yaliyofanywa mnamo tarehe 19/01/2017, kati ya Bahati Bukuku na mwelekezi wa kipindi, Sangu Joseph, katika stesheni ya runinga ya *East Africa TV (EATV)* nchini Tanzania, kipindi cha *Kikaangoni*, Bahati Bukuku alieleza kuhusu safari ya maisha yake, pamoja na muziki wake. Alizaliwa katika mkoa wa Mbeya nchini Tanzania mnamo mwaka wa 1981. Jina lake halisi

ni Lusako Bukuku ila aliandikishwa shuleni kama Bahati Bukuku. Alipata elimu yake ya msingi katika shule ya Rungwe, mwaka wa 1988, Rungwe, Mbeya, kujiunga na kiwango cha chekechea. Baada ya miaka miwili katika shule ya chekechea, Bahati Bukuku alijiunga na shule ya msingi ya Muungano.

Maisha ya shule ya msingi ndiyo yalikuwa msingi wa kipaji alicho nacho Bahati Bukuku cha uimbaji. Bahati Bukuku alitoa madai kuwa kuimba kulikuwa kipaji chake alichozaliwa nacho. Mazoea yake ya uimbaji yalizidi alipokuwa katika shule ya chekechea. Walimu wake walipenda sana kumchagua ili aweze kuimba gwarideni. Kipaji hiki cha uimbaji kilikuzwa hasa katika shule ya msingi. Majukumu mengi ya kuimba alipewa yeye. Vilevile, Bukuku aliweza kuhusika pakubwa katika tamasha mbalimbali za mziki katika mashindano kati ya shule yake pamoja na shule zingine jirani. Uzoefu katika uimbaji wake ulizidi kunawiri hadi kuamini kuwa kuimba kungechukua nafasi kubwa katika maisha yake.

Bahati Bukuku hakuweza kuendeleza masomo yake ya shule ya upili kwani wazazi wake wasingeweza kumudu kumwendelezea masomo yake. Hali hii haikumkatisha tamaa yake ya muziki kwani aliweza kuendeleza kipaji chake.

Kipaji cha uimbaji cha Bahati Bukuku kimemfanya kuimba nyimbo nyingi sana. Nyimbo alizoimba ziko katika albamu nne; *Dunia haina huruma, Nani aitikise dunia, Yashinde mapito na Nimesamehewa dhambi*. Katika albamu hizi nne, nyimbo alizoimba Bukuku ni kama; *Dunia haina huruma, Majaribu, Maamuzi, Lazima usamehe, Heshima ya dhahabu, Magonjwa yote, Nimesamehewa, Wewe ni baba, Atakushangaza, Siri ya mafanikio, Abneli, Ahabu, Songa mbele, Nani aitikise dunia, Mbeba maono, Kampeni, Mosala, Muathirika wa ndoa, Tendeka, Jehovah, Barthimayo, Nabii nani, Shujaa, Tupatupa, Unatisha na Waraka*.

1.2 Suala la utafiti

Vipengele vya usimulizi vimefanyiwa utafiti mpana, haswa katika fasihi andishi. Kwa mfano, Wafula (1989); Vonyoli (2004); Magaju (2004); Bakari (2008). Utanzu wa fasihi simulizi ambao umehakikiwa ni wa ushairi simulizi uliohakikiwa na Arege (2012) akitafiti usimulizi katika Utenzi wa *Rasi 'lghuli*. Baadhi ya tanzu za fasihi simulizi zimetungwa na kuwasilishwa kwa kutumia mbinu ya usimulizi kama mtindo. Hata hivyo, uwanja huu haujahakikiwa kindani ikilinganishwa na fasihi andishi. Kwa hivyo nyimbo zilizoimbwa kwa kutumia usimulizi kama mtindo zinapaswa kufanyiwa utafiti mpana.

Utafiti huu ulichunguza vipengele vya masimulizi katika nyimbo teule za Bahati Bukuku. Vipengele vya usimulizi vilivyohakikiwa ni kama; mianzo maalum, mfuatano wa matukio, kuwepo kwa kilele cha usimulizi pamoja na tamati maalum ya usimulizi.

Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa kuonyesha wazi jinsi mbinu ya usimulizi katika nyimbo imejitokeza katika nyimbo za Bahati Bukuku. Vilevile, utafiti huu ulilenga kuonyesha jinsi usimulizi unavyoweza kuwasilisha maudhui katika fasihi ya nyimbo. Utafiti huu aidha ulifafanua jinsi sauti za usimuliaji na mahusiano ya wakati wa usimulizi zilivyojidhihirisha katika nyimbo teule za Bahati Bukuku.

1.3 Maswali ya utafiti.

Maswali ya utafiti ni kama yafuatayo;

1. Je, ni kwa njia gani mbinu ya masimulizi imejitokeza katika nyimbo za Bahati Bukuku kwa kuzingatia ploti na wakati?
2. Je, mbinu ya usimulizi imechangia vipi kufanikisha maudhui katika nyimbo za Bahati Bukuku?

3. Je, sauti ya usimuliaji na mahusiano ya wakati wa usimulizi zinabainika vipi katika nyimbo teule za Bahati Bukuku?

1.4 Malengo ya utafiti

Utafiti huu uliongozwa na malengo yafuatayo;

1. Kueleza jinsi mbinu ya usimulizi imejitokeza katika nyimbo za Bahati Bukuku kwa kuzingatia ploti na wakati.
2. Kudhihirisha namna usimulizi ulivyosaidia kuibua maudhui.
3. Kufafanua jinsi sauti ya usimuliaji na mahusiano ya wakati wa usimulizi zinavyobainika katika nyimbo teule za Bahati Bukuku.

1.5 Sababu za kuchagua mada ya utafiti

Ingawa mtindo wa usimulizi umefanyiwa utafiti mpana, tahakiki nyingi zimezingatia tanzu za fasihi andishi. Utafiti wa Arege (2012) ndio uliweza kuhusisha usimulizi katika fasihi simulizi, kwa kuhakiki ushairi. Mtindo wa usimulizi haujahakikiwa kwa kina, hasa katika fasihi simulizi, ikizingatiwa kuwa tanzu mbalimbali za fasihi simulizi, ikiwemo maigizo, nyimbo na semi, huhusisha matumizi ya mbinu ya usimulizi. Hivyo basi, nyimbo, kipera cha utanzu wa ushairi simulizi, zilizoimbwa kwa mtindo wa usimulizi, zilipaswa kuhakikiwa kiundani.

Kuna baadhi ya wasanii ambao kati ya nyimbo walizoimba, chache ziliweza kutumia mtindo wa usimulizi. Wasanii kama Sharry Martins, Jemimah Thiong'o, Christina Shusho na Bonny Mwaitege wameweza kutunga na kutoa rekodi zilizotumia usimulizi kama mtindo. Hata hivyo, rekodi hizo hazingeridhisha malengo ya utafiti huu kwani nyimbo walizoimba zenye usimulizi ni chache mno kutumiwa kwa minajili ya utafiti. Nyimbo alizoimba Bahati Bukuku kwa kutumia mbinu ya usimulizi kama mtindo ni toshelevu, takribani kumi na moja kati ya rekodi thelathini

ambazo amerekodi. Idadi hiyo ya nyimbo ni toshelevu, na inayoweza kutumiwa katika utafiti wa kina.

Nyimbo, kama tanzu zingine za Fasihi Simulizi, zina dhima mbalimbali katika jamii, kwa mfano, kuadilisha, kuonya, kuelekeza, kuburudisha na kadhalika. Nyimbo za kidini hutekeleza majukumu haya yote. Kwa mfano, wimbo wa Bahati Bukuku wa *Dunia haina huruma* una dhima ya kuelimisha kuhusu umuhimu wa msamaha katika jamii pamoja na kuonya dhidi ya tabia ya kutoa uamuzi kabla ya kutathmini jambo kwa undani. Hivyo basi ni muhimu kuzitafiti nyimbo za Bahati Bukuku ili kubainisha manufaa ya nyimbo hizi katika jamii ya wasikilizaji wa nyimbo za kidini.

Utafiti huu pia ulifanywa ili kubainisha sura za kifomyula za usimulizi zinazodhihirika katika nyimbo teule zenye sifa za kisimulizi zilizoimbwa na Bahati Bukuku. Katika utangulizi wa nyimbo zake, mitindo tofauti imetumika. Iwapo kuna tofauti za kiutaratibu wa uanzilishi wa nyimbo hizo, utafiti huu ulizibainisha moja baada ya nyingine.

Utafiti huu pia ulinuia kuziba pengo ambalo halijaweza kuzibwa na tafiti za awali. Tafiti za awali zinazohusishwa na nyimbo, kwa mfano: Wambua (2001), Mutwiri (2005), Mwanza (2007), Rajweyi (2009), Mwikali (2011) na Simiyu (2015), zilizingatia tamathali tofautitofauti kama jazanda katika nyimbo, fani katika nyimbo na ufaafu wa maana katika tafsiri ya nyimbo. Vilevile katika usimulizi, tafiti za awali, kwa mfano: Vonyoli (2004), Magaju (2004), Bakari (2008) na Arege (2012), zimezingatia usimulizi wa kimazingaombwe, usimulizi kama chombo cha kuibua maudhui, usimulizi wa kiuhalisia ajabu, na jinsi unavyotumika na waandishi kuibua maudhui. Utafiti huu kwa hivyo ulinuia kuziba pengo ambalo halijazibwa na tafiti za awali kwa kuzingatia mada yenye malengo tofauti ikilinganishwa na yale ya awali.

1.6 Upeo na mipaka ya utafiti

Utafiti huu ulifanya uchunguzi mbinu ya usimulizi katika nyimbo za Bahati Bukuku. Bukuku ni mwimbaji ambaye hupendelea kuwasilisha maudhui katika nyimbo zake akitumia usimulizi kama mbinu muhimu. Kati ya nyimbo zaidi ya thelathini ambazo amerekodi, kumi na tatu kati yazo zimetumia usimulizi kama mtindo wa uwasilishaji. Kati ya nyimbo alizorekodi zenye usimulizi, utafiti ulitumia nyimbo kumi ili kuafikiana na malengo ya utafiti huu. Aidha, ingawa kuna mbinu nyingine ambazo zimetumiwa katika nyimbo zake, mbinu ya usimulizi ndiyo iliyojitokeza kuwa maarufu kwa nyimbo zake zilizovuma sana.

Utafiti ulizingatia nyimbo kumi pekee zilizowasilishwa kisimulizi zenye muundo uliohitajika kufanikisha malengo ya utafiti ya kufafanua maudhui, mfuatano wa matukio, dhana ya wakati wa usimulizi, sauti ya usimuliaji na mahusiano ya wakati wa usimulizi. ingawa nyimbo zilizowasilishwa kiusimulizi ni zaidi ya kumi, kuna baadhi ya nyimbo ambazo hazingefanikisha uhakiki wa malengo lengwa.

1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada

Kazi zilizoandikwa kuhusu mada zilishughulikiwa kwa misingi miwili: kwa kuzingatia yaliyoandikwa kuhusu nyimbo, ambacho ndicho kipera kilichotawala utafiti huu pamoja na yaliyoandikwa kuhusu usimulizi, ambayo ndiyo mbinu kuu iliyotumiwa katika utafiti huu.

1.7.1 Yaliyoandikwa kuhusu nyimbo

Nyimbo ni kipera muhimu cha utanzu wa ushairi simulizi. Kabla ya maandishi kuanza kutumika, wanajamii walitegemea vipera kama nyimbo kuendesha shughuli zao mbalimbali kama; upanzi wa mimea na mavuno, sherehe mbalimbali, dini na kadhalika. Umuhimu wa nyimbo haijapungua, kwani ata baada ya uvumbuzi wa maandishi, nyimbo zingali na dhima kubwa sana, ikiwemo katika utafiti

Umuhimu wa nyimbo hupatikana kupitia maudhui na mtindo. Haya ni kwa mujibu wa Finnegan (1970) aliyefanya utafiti kuonyesha umuhimu wa nyimbo katika jamii za Afrika Mashariki na Kati na jinsi dhima ya nyimbo hizi inavyobainika. Utafiti wake ni muhimu kwa utafiti huu kwani ulitambua mchango wa mtindo katika kuelewa maudhui ya nyimbo za Kiafrika.

Utafiti wa Nkonge (1988) ulijikita pakubwa katika suala la mtindo na maudhui. Nkonge alitafiti mtindo na maudhui katika nyimbo za Joseph Kamaru. Ingawa alimtumia msanii tofauti katika utafiti wake, utafiti wake ulifaa huu, haswa katika uchanganuzi wa maudhui. Utafiti wa Nkonge ulitofautiana na huu kwani alihakiki mtindo kwa ujumla ilhali utafiti huu ulishughulikia kipengele mahsusi cha masimulizi.

Katika uchunguzi wa Kieti (1989), alijihusisha na taswira na mazingaombwe kama yanavyotumiwa kuwasilisha ujumbe wa mwimbaji. Alibaini majina yaliyotumiwa yalikuwa na maana fiche, majina ya wanyama yalihuishwa na yale ya vitu visivyo na uhai yakapewa sifa za binadamu. Utafiti wake ulitofautiana na huu kwa kuwa utafiti huu ulitumia nyimbo za kisasa.

Watafiti Ntarangwi (1990) na Yalwala (1991) walifanya tafiti zilizokuwa na mshabaha katika kiwango cha maudhui kwani wote wawili walihakiki maudhui katika nyimbo. Tafiti hizi zilibaini wazi mitindo ya kubaini maudhui kutoka kwa nyimbo, ingawa walihakiki nyimbo za wasanii wawili tofauti ambao ni Remi Ongala na John Mwale mtawalia. Mchango wa watafiti hawa katika maudhui yalifaidi utafiti huu kwani lengo mojawapo la utafiti huu lilikuwa uhakiki wa maudhui.

Uhusiano kati ya uteuzi wa lugha kwa kuzingatia vipengele vya kimtindo na maudhui ulihakikiwa na mtafiti Wambua (2001). Alifanya utafiti uliohusu mtindo na matumizi ya lugha katika nyimbo za Kakai Kilonzo. Alionyesha wazi uhusiano mkubwa uliopo kati ya matumizi ya lugha na uhakiki wa maudhui katika nyimbo zake. Utafiti wa Wambua ulifaa utafiti huu kwa upande wa lugha na

maudhui. Tafiti hizi ni tofauti kwa vile yeye alitafiti mtindo kwa jumla ilhali kazi hii ilijikita katika kipengele mahsusi cha usimulizi.

Kijumla, nyimbo huwa na umuhimu mkubwa katika jamii, zikiwemo kuburudisha, kuhifadhi historia ya jamii, kushutumu maovu na kadhalika. Uhakiki wa nyimbo kulingana na utendakazi wake ulihakikiwa na Mutwiri (2005) aliyefanya utafiti kuhusu nyiso za Watigania kwa kuangazia utendakazi wake. Umuhimu wa nyiso za Watigania zilielezwa kwa utendeti. Utafiti wake ulitofautiana na huu kwani utafiti huu ulijikita katika kipengele cha mtindo cha usimulizi na wake ulizingatia utendakazi pekee.

Mitindo ya utunzi na uwasilishaji wa nyimbo hutegemea pakubwa swala la rika. Utunzi wa nyimbo za rika mbalimbali hutofautiana pakubwa katika suala la lugha na maudhui. Utafiti kuhusu mtindo wa nyimbo za watoto wa shule za chekechea ulihakikiwa na Mwanza (2007) ambaye katika utafiti wake, alishughulikia vipengele vya kimtindo katika nyimbo za watoto wa shule za chekechea. Aidha, maudhui ya nyimbo hizo za watoto yalihakikiwa. Utafiti wa Mwanza na utafiti huu zina uhusiano kwani zote zimeegemea katika mtindo na maudhui. Hata hivyo, tafiti hizi mbili zilitofautiana katika kiwango cha aina za nyimbo zilizohakikiwa. Aidha, Mwanza alijumlisha mtindo ilhali utafiti huu ulishughulikia kipengele mahsusi cha masimulizi katika nyimbo.

Mbali na nyimbo zilizotungwa na kuwasilishwa moja kwa moja na baadaye kutafitiwa, kuna zile ambazo zilikopwa kwa kubadilisha lugha asili. Nyimbo zenye mfano kama huu zilifanyiwa utafiti na Mwaniki (2011) aliyehakiki matumizi ya lugha katika nyimbo tohozi za Salim Junior. Katika utafiti wake, Mwaniki alichunguza mabadiliko ambayo yameibuka katika nyimbo katika jamii ya Wakikuyu kisha akachunguza utohozi wa Salim Junior. Kwa kuwa utafiti wa Mwaniki ulizingatia baadhi ya vipengele vya kimtindo, uliweza kufaa utafiti huu. Utafiti wa Mwaniki ulitofautiana na

huu kwa kuwa haukuzingatia nyimbo za msanii mwenyewe, bali zile tu alizotohoa kutoka kwa wasanii wengine.

Utafiti wa Simiyu (2015) uliangazia jinsi tanzu mbalimbali za Fasihi Simulizi zinavyoweza kuingiliana katika ngazi mbalimbali. Alihakiki Mwingilianotanzu katika fasihi simulizi ya Kiafrika kama *Embalu* na *Mwaka Kongwa*. Utafiti wake ulifaa utafiti huu katika kujua jinsi mbinu ya uandishi inavyoweza kusaidia katika kuzua maudhui katika kipera cha nyimbo.

Uchunguzi huu unaonyesha wazi kuwa tafiti nyingi zimefanywa kuhusu kipera cha nyimbo. Vipengele vilivyorejelewa ni pamoja na tamathali za usemi, utohozi, wahusika, maudhui pamoja na dhamira ya nyimbo zilizotafitiwa. Tafiti zilizofaa utafiti huu hata hivyo ni zile zenye uzingativu katika kipengele cha mtindo.

1.7.2 Yaliyoandikwa kuhusu Usimulizi

Usimulizi katika kazi ya fasihi unaweza kuainishwa kwa kuangazia vipengele maalum vya kazi ya fasihi kama vile wahusika wa kazi mahsusi, mtindo, maudhui pamoja na historia ya kazi hiyo. Utafiti mwingi umefanywa ukihusisha usimulizi kama mtindo katika kazi za kifasihi.

Kuna usimulizi wa kijazanda ambao ulijadiliwa na Wafula (1989). Alihakiki kazi za Shaaban Robert; *Kusadikika (1951), Adili na Nduguze (1952), Kufikirika (1991), Utubora Mkulima (1968) na Siku za Watenzi wote (1968).* Wafula aliangazia jinsi Shaaban Robert anavyotumia jazanda katika usimulizi wa riwaya zake. Alihakiki matumizi ya masimulizi ya kijazanda au kimajazi kama mtindo na wala si kimuundo. Utafiti wa Wafula (1989) ulitofautiana na utafiti huu kwa misingi kuwa utafiti wake ulihakiki jazanda kaatika masimulizi ilhali kazi hii inahakiki usimulizi wenyewe kama mbinu.

Kuhusu mchango wa usimulizi katika kuibua maudhui, Vonyoli (2004) anafafanua kuwa usimulizi au hadithi ndicho chombo cha kuibua maudhui. Katika kutafiti riwaya za Mkangi; *Mafuta (1984)* na *Walenisi (1995),* Vonyoli alichunguza matumizi ya masimulizi kwa ujumla katika ubunifu wa maudhui katika nathari bila kuangalia nafasi yake kimuundo katika riwaya. Utafiti wa Vonyoli (2004) ulifaidi utafiti huu katika misingi ya maudhui kwani lengo mojawapo la utafiti huu ni kudhihirisha nafasi ya usimulizi katika kuibua maudhui.

Usimulizi unaweza kuwa wa kiuhalisia au wa kiulimbwende. Utafiti wa Magaju (2004) ulichunguza kuhusu usimulizi wa uhalisia ajabu. Alizama zaidi kutaka kujua jinsi usimulizi wa uhalisia ajabu unavyotumika na watunzi kuibua maudhui. Utafiti wa Magaju (2004) ulifaa utafiti huu kwa vile utafiti huu ulikuwa na lengo moja la kutambua mchango wa mbinu ya usimulizi katika kujadili maudhui. Utafiti wa Magaju una mshabaha na utafiti wa Bakari (2008) kwani tafiti hizi mbili zinajikita katika swala moja la usimulizi wa kiuhalisia ajabu. Hata hivyo, kwa upande wake, Bakari (2008) anafafanua jinsi ya kuhakiki riwaya zilizojikita katika usimulizi wa kiuhalisia ajabu. Kulingana na maelezo yake, usimulizi wa uhalisia ajabu huleta utata katika uelewa wa matini lakini ujuzi wa usemezano kwa msomaji, humwezesha kuhusisha kazi za fasihi na maisha ya kawaida. Alijadili umuhimu wa usemezano kutoa masimulizi ya uhalisia ajabu kutoka kwa uajabu wake hadi kwa ukawaida wa maisha ulimwenguni. Maelezo ya utafiti wa Bakari yalifaa katika uhakiki wa wimbo wa *Maamuzi* ambao una matukio ya kiuhalisia ajabu lakini yanayoelekezwa kwa njia ya kawaida ya maisha ya kisasa.

Usimulizi vilevile umehakikiwa kwa kurejelea ushairi simulizi katika fasihi simulizi. Utafiti wa Arege (2012) ulizingatia Utenzi wa *Rasi 'lghuli* . Katika utafiti huu, Arege alijadili vipengele muhimu vya usimulizi; Wakati- Hadithi, Uhusika pamoja na Viwango vya usimulizi. Vilevile,

maudhui tofauti katika utendi huo yaliweza kuhakikiwa kwa undani. Vipengele hivi alivyojadili vilikuwa na dhima kuu katika utafiti huu.

Suala la maudhui katika simulizi zinazowasilishwa kupitia maigizo katika mashindano ya kitaifa ya shule na vyuo vikuu lilitafitiwa na Opondo (2014). Katika makala yake, tofauti za kikabila na kimila zinajitokeza wazi kupitia simulizi zilizowasilishwa mashindanoni. Makala haya yalionyesha tofauti zilizojitokeza kati ya maigizo ya shule na vyuo vya mjini ikilinganishwa na shule na vyuo vya mashambani. Makala haya yalifaa utafiti huu katika misingi ya maudhui na uwasilishaji wa maudhui, kwani utafiti huu vilevile umehakiki jinsi maudhui yanavyoibuliwa na mbinu za usimulizi. tafiti hizi mbili zinatofautiana kitanzu kwani utafiti wa Opondo (keshatajwa) umehakiki maigizo ilhali utafiti huu umehakiki nyimbo.

Baadhi ya tafiti zimefanywa kuhusu mihimili ya nadharia ya naratolojia, kwa kujikita katika vipengele vyake kadhaa. Wafula na Wanjala (2017) walihakiki mhimili wa wakati kwa kurejelea kipengele cha mpangilio walipochambua riwaya ya kiingereza ya Chinua Achebe ya *Things Fall Apart.* Katika makala yao, wanabaini kuwa kazi nyingi za awali za Chinua Achebe zilihusishwa na vipengele vya kijumla, kama vile: muundo, matumizi ya lugha na maudhui. Hata hivyo, Wafula na Wanjala (keshatajwa) walijihusisha na uchambuzi wa kipengele cha mpangilio huku wakihakiki jinsi kipengele hiki cha wakati kimejidhihirisha katika riwaya tajwa. Uhakiki wao ulifaa uhakiki huu katika msingi wa mhimili wa wakati katika nadharia ya naratolojia, ambao vilevile ulihakikiwa katika utafiti huu kwa kurejelea nyimbo teule za msanii Bahati Bukuku.

Kwa hivyo, jinsi inavyojitokeza, uchunguzi mwingi umefanywa ulioegemeza usimulizi katika kuleta mchango katika riwaya na ushairi simulizi wa Kiswahili kwa kuzingatia maudhui, mtindo na wahusika. Hata hivyo, waliorejelea usimulizi waliurejelea kama mtindo, tofauti na utafiti huu uliourejelea usimulizi kama mbinu ya uandishi

1.8 Msingi wa nadharia

Nadharia ya naratolojia ndiyo ilikuwa msingi wa utafiti huu. Inaaminika kuwa muasisi wake wa kwanza alikuwa Aristotle. Kazi za kinaratolojia ziliibuka 1966 kule Ufaransa ingawa neno "Naratolojia" liliibuliwa miaka mitatu baadaye na Tzvetan Todorov (1969). Naratolojia ilijihusisha na kuchunguza muundo wa masimulizi kwa kugawa vipengele vya simulizi kisha kuzingatia uamilifu na uhusiano.

Wataalamu wa mwanzoni walioibukia kazi za kinaratolojia ni kama Lord Raglan na Vladimir Propp (1968). Wafuasi wengine wa nadharia hii ni kama vile; Prince (1973), Barthes (1975), Gennete (1980) na Chatman (1990).

Vipengele muhimu katika nadharia ya naratolojia ni Simulizi, Usimulizi na Ploti. Nadharia hii husisitiza kipengele cha kusimulia hadithi katika kazi zozote za kifasihi, andishi au simulizi. Kazi nyingi za fasihi simulizi hupokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine, na hivyo kufanikisha usimulizi kati ya vizazi hivi. Masimulizi huundwa kwa njia ya kuonyesha usimulizi wa mfuatano wa matukio yenye mahusiano. Matukio katika masimulizi yanaweza kuwasilishwa kwa namna mbalimbali. Kama anavyodokeza Genette (1980:25) kuna mambo matatu muhimu ya kuzingatia katika simulizi:

i. Kauli iliyodhamiria kulieleza tukio au matukio fulani.
ii. Mfuatano wa matukio halisi au ya kubuni.
iii. Tendo lenyewe la kusimuliwa au kisimulizi.

Kwa hivyo, wahakiki wengi wamekubaliana kwamba katika simulizi, lazima kuwe na utambwaji wa hadithi kwa njia mbalimbali. Aidha, mfuatano wa matukio katika simulizi huweza

kuwasilishwa kwa njia mbalimbali. Jinsi kuu ni ile ya uelezaji na uonyeshaji. Plato anatumia dhana *daigesio* kwa maana ya uelezaji na *mimesia* kwa maana ya uonyeshaji.

Kipengele kingine muhimu cha nadharia hii ni wakati. Wahakiki wa nadharia hii kama vile Genette (1980) na Rimmon- Kenan (1983), wanabainisha kati ya wakati-hadithi na wakati-matini. Wakati-hadithi imechukuliwa kuonyesha wakati ule unaotumika katika hadithi kuanzia mwanzo hadi mwisho. Wakati-matini huchukuliwa kuwa wakati inayochukua matini fulani kusomwa. Kipengele cha wakati huweza pia kuangaliwa kwa kuvichunguza vigezo vingine kama mpangilio, muda na idadi marudio. Vipengele hivi vinakuwa muhimu katika uhakiki unaolenga kuchunguza mfuatano wa kiwakati au kwa kutofungamana nao. Ikiwa yatasimuliwa kiwakati, msuko wa hadithi huwa na mpangilio sawa. Muda nao huurejelea uhusiano katika hadithi. Tukio linaweza kuchukua kipindi kirefu au kifupi. Idadi marudio nayo hurejelea mara ambazo matukio hutokea katika hadithi.

Uhusika pia huangaliwa kama kipengele muhimu katika uhakiki wa kinaratolojia. Wahusika huchunguzwa kutokana na hulka zao katika kazi ya kisanaa, kutokana na anachosema msanii kuhusu mhusika huyo, matendo ya mhusika yanayoonekana moja kwa moja katika kazi pamoja na wanachosema wahusika wengine kumhusu mhusika mrejelewa. Aidha, maneno, matendo, sura, mazingira walimo, mandhari, hali yao na mengineyo humdokeza mhusika.

Manfred (2005) anadokeza hali na dhamira kama viambajengo muhimu katika nadharia ya naratolojia. Hali huzingatia matendo, amri, matarajio, na uwezekano fulani katika simulizi. Nafsi neni pia imeangaziwa kama kiambajengo muhimu katika usimulizi. Swali la kimsingi huhusiana na nafsi neni. Hata hivyo sauti inachukuliwa pia kama uzungumzi au toni ya kipekee inayojitokeza katika matini. Hadithi inahitajika kuwa na mada, funzo, uwezo wa kuonyesha tajriba na kuonyesha kupangika kwa matukio yake kwa njia inayofaa.

Kipengele kingine muhimu ni kile cha hali ya masimulizi, sauti ya msimulizi na mazaji. Sauti hii hujenga uhusiano na anayesimuliwa. Yeye ndiye anayetoa mtazamo wa masimulizi, mfuatano, na kuchagua ni nini cha kuwacha katika masimulizi na pia kutoa dhamira. Pia kuna mazaji ambayo yaweza kuwa ya kukubali, kuonyesha furaha, huzuni ambayo pia inachangia hali ya masimulizi.

Suala lingine muhimu katika uhakiki wa kinaratolojia ni usemi. Usemi wa masimulizi ni yale yaliyosemwa au matini inayotokana na tendo la usimulizi. Dolozel (1973) anaeleza kuwa matini yoyote ya kisimulizi ni mfungamano na mabadiliko ya usemi wa mhusika. Kimsingi, simulizi inaweza ikawekwa katika sehemu mbili: usemi wa msimulizi na usemi wa wahusika inayoeleza maneno na matendo ya msimulizi kumhusu mhusika.

Kwa mujibu wa nadharia hii, mtambaji ana nafasi kubwa katika simulizi, jambo linalofanikisha uelewa wa kazi yake na wasikilizaji au wasomaji wake. Genette (1980) anaeleza kwamba katika uhakiki wa matini, ni vyema kutambua anayeona na mzungumzaji ili kuweza kupata ni nini hasa kiini cha simulizi. Katika masimulizi, tunaweza kuchunguza yanayosemwa na mhusika mkuu, mhusika mjenzi au msimulizi iwapo ni mmoja kati ya wahusika ambao wamo kwenye hadithi au iwapo ni msimulizi bila kuhusika katika hadithi.

Mbali na mihimili iliyotajwa awali, maudhui pia inajitokeza kuwa muhimu sana katika masimulizi. Hakuna usimulizi ambao unaweza kufanikishwa pasipo kuwepo na mawazo makuu yanayowasilishwa kupitia masimulizi yenyewe. Malengo ya usimulizi pamoja na wahusika wanaotumiwa na mtunzi wa hadithi hutegemea pakubwa katika maudhui yanayowasilishwa na mtunzi huyo katika kazi yenyewe.

Sauti ya usimuliaji ni kipengele kingine chenye umuhimu mkubwa katika masimulizi ya aina yoyote. Hadhira itaelewa nafsi inayotumiwa katika usimulizi iwapo sauti ya usimuliaji

umefanikishwa. Kuna masimulizi ambayo huwasilishwa katika nafsi ya kwanza, ambapo aghalabu msimuliaji ni mhusika mmoja wapo katika masimulizi. Vilevile, masimulizi huweza kutolewa katika nafsi ya pili ambayo huweza kuhusisha sifa za nafsi ya kwanza nay a tatu. Katika usimuliaji wa nafsi ya tatu, msimulizi anaweza kuwa nje ya masimulizi, huku akieleza matukio kwa ubingwa mkubwa na ujuzi wa hali ya juu.

Mahusiano ya wakati wa usimulizi ni kiambajengo kingine chenye umuhimu mkubwa katika nadharia hii. Kipengele hiki ni tofauti na kile cha wakati. Katika kipengele hiki cha usimulizi, kunahakikiwa iwapo kitendo kilitendeka kwa wakati uliopita, wakati uliopo, wakati ujao ama iwapo kuna mchangamano wa matukio wa nyakati tofauti katika matini moja.

Utafiti huu uliongozwa na mwananaratolojia Gennete (1980) ambaye alijiegemeza katika hatua za usimulizi. Mawazo ya Gennete yatasaidia katika uhakiki wa usimulizi kama mtindo katika nyimbo za Bahati Bukuku. Mihimili muhimu vilevile itahusishwa na mawazo ya Gennete.

Mihimili ya nadharia hii ni;

(a) Kitendo cha utambwaji.

Kitendo cha utambwaji kinachowezesha kuelewa jinsi matendo tofauti katika nyimbo za Bahati Bukuku zinasaidia katika uelewa wa anachosimulia katika nyimbo zake.

(b) Mfuatano wa matukio katika hadithi.

Mhimili huu ulifaa katika kuhakiki jinsi Bahati Bukuku alivyotumia misuko tofautitofauti katika kusimulia matukio katika nyimbo zake zenye matumizi ya masimulizi katika nyimbo.

(c) Wakati/Muda unaotumika katika simulizi.

Mhimili huu ulifaa katika kuelezea jinsi Bahati Bukuku alivyopanga kazi yake kiwakati kufafanua athari ya wakati kwa matukio yanayosimuliwa katika kazi yake.

(d) Maudhui katika usimulizi

Mhimili huu ulisaidia katika kufafanua baadhi ya maudhui ambayo ilijitokeza katika nyimbo zilizoteuliwa kutumiwa katika utafiti huu.

(e) Sauti ya usimuliaji

Mhimili huu ulichangia katika kutambua iwapo simulizi lengwa katika nyimbo za Bahati Bukuku zilitumia sauti zinazopaswa katika usimuliaji, kwa mfano, sauti ya msimuliaji mwenyewe ambaye ndiye mhusika mkuu ama sauti ya msimuliaji ambaye kimsingi yuko nje ya usimulizi lakini ni mwenye ujuzi kwa yanayotukia.

(f) Mahusiano ya wakati wa usimulizi

Mhimili huu ulikuwa wa msaada katika kuchanganua nyakati zilizotumiwa katika simulizi lengwa, na kuchunguza iwapo vitendo vilitendeka katika wakati upi.

Nadharia ya naratolojia hivyo basi ilifaa pakubwa katika utafiti huu. Baadhi ya mihimili, inayofungamana na mawazo ya Gennete (1980), kwa mfano: ploti, wakati, sauti ya usimuliaji na mahusiano ya wakati wa usimulizi, ilitumika katika kuhakiki mtindo wa usimulizi katika nyimbo za Bahati Bukuku. Utafiti huu ulitegemea mihimili kama: Kitendo cha utambwaji kilichotuwezesha katika kuelewa vipengele muhimu vya ploti na wakati, mhimili wa maudhui uliochangia katika kufafanua maudhui yaliyowasilishwa katika nyimbo teule, kigezo cha sauti ya usimuliaji kilichowezesha kuelewa nafsi mbalimbali zilizotumiwa katika simulizi lengwa pamoja na kigezo cha mahusiano ya wakati kilichowezesha ufafanuzi wa nyakati mbalimbali za usimulizi zilizotumiwa katika nyimbo lengwa.

1.9 Mbinu za utafiti

Utafiti huu ulifanywa kwa muundo maalum kuzingatia mahitaji ya chuo. Muundo wake ulihusisha: kufafanua usuli wa mada, suala la utafiti, kuorodhesha maswali na malengo ya utafiti, kuonyesha sababu za kuchagua mada, kufafanua upeo na mipaka ya utafiti, kujadili yaliyoandikwa kuhusu mada pamoja na kufafanua msingi na mihimili ya nadharia husika. Wasifu wa msanii Bahati Bukuku pia ulifafanuliwa ili kumwelewa msanii vyema.

Utafiti huu ulifanywa maktabani. Hii ni kwa sababu raslimali muhimu zenye vipengele vya nadharia teule pamoja na mapitio ya kazi vilipatikana katika maktaba. Kothari (2005) ananakili kuwa mtafiti anahitaji mbinu za utafiti zinazotoa matokeo sahihi na maelezo ya utendeti kulingana na mada inayohusika.

Nyimbo zote zenye sifa lengwa zilisampiuliwa ili kutumiwa katika utafiti huu. Mtafiti alitafuta albamu zote zinazosheheni nyimbo za Bahati Bukuku. Mtafiti vilevile alitoa nyimbo zilizoimbwa hivi karibuni zisizo katika albamu kwenye mtandao. Nyimbo hizi zilisikilizwa na kuhakikiwa kulingana na malengo ya utafiti. Nyimbo hizi vilevile ziligeuzwa kimaandishi ili kusaidia katika uchanganuzi wa undani wa nyimbo hizi kulingana na malengo ya utafiti.

Mtafiti vilevile alifanya utafiti maktabani kwa kusoma maandishi yoyote yaliyohusiana na maswali ya utafiti, makala iliyochapishwa na ile ya mtandaoni na tasnifu mbalimbali za awali zilizoandikwa zenye uwiano na mada ya utafiti. Aidha, vitabu pamoja na maandishi mengine kuhusu nadharia ya naratolojia yalisomwa kwa kina ili kusaidia katika kuelewa nadharia hiyo na kuitumia kwa njia faafu.

Vilevile, mchango na maoni ya wataalamu mbalimbali wa fasihi kuhusu mada ya utafiti yalikuwa ya manufaa zaidi katika utafiti huu.

1.9.1 Sampuli

Kwa mujibu wa Mertens (1998), sampuli ni kijikundi kidogo kutoka kwa kundi nzima. Usampulishaji kwa upande mwingine ni mbinu inayotumika kuchagua kijikundi kidogo kati ya kundi nzima la kufanyiwa utafiti. Kwa hivyo, mtafiti alichagua tu kijikundi chenye sifa alizonuia kutumia katika utafiti wake. Bahati Bukuku amerekodi nyimbo zaidi ya thelethini ila ni nyimbo kumi pekee zilizotungwa na kurekodiwa kwa kutumia mbinu ya usimulizi. Katika utafiti huu, mtafiti alijikita katika nyimbo zenye mbinu ya usimulizi pekee. Hivyo basi, sampuli lengwa ilikuwa nyimbo zifuatazo za Bahati Bukuku; *Maamuzi*, *Abneli, Ahabu, Barthimayo, Dunia haina huruma*, *Lazima usamehe, Mbeba maono, Unatisha*, *Tupatupa* na *Waraka*. Mbinu ya usampulishaji iliyotumiwa ni ya kimaksudi. Mayaka, Aswani na Matinde (2013) wanaeleza kuwa katika mbinu hii ya usampulishaji, sampuli lengwa huteuliwa kwa misingi ya malengo ya utafiti ili mtafiti aweze kuafikia malengo yake.

1.9.2 Ukusanyaji wa data

Hatua ya mwanzo ya ukusanyaji wa data ilihusu uchaguzi wa nyimbo zilizohitajika katika utafiti kati ya nyimbo zote alizorekodi. Nyimbo hizi zilipatikana katika kaseti. Nyimbo alizorekodi hivi karibuni zilitolewa mtandaoni. Nyimbo hizi zilisikilizwa na kuhakikiwa kulingana na malengo ya utafiti. Nyimbo hizi vilevile ziligeuzwa kimaandishi ili kusaidia katika ukusanyaji wa data zinazohitajika kuwiana na malengo ya utafiti.

Matini iliyoandikwa kwa kuzingatia miundo na maumbo ya kiusimulizi ilifanywa maktabani. Mtafiti alisoma na kunakili makala yanayohusiana na nadharia teule ya naratolojia katika utafiti wake. Data pia ilikusanywa kwa kusoma majarida, makala ya mtandaoni pamoja na tasnifu za awali zilizoandikwa kwa kutumia nadharia ya Naratolojia. Mtafiti alinakili maandishi yote muhimu yaliyomsaidia katika utafiti huu.

Mihimili muhimu ya nadharia ya naratolojia iliyochangia katika uhakiki wa kazi hii ilihusishwa na mawazo ya mwananaratolojia Genette (1980). Mihimili hii ni; kitendo cha utambwaji iliyosaidia kubaini maudhui ibuka kutoka kwa simulizi, mfuatano wa matukio iliyosaidia katika kutambua ploti mbalimbali za simulizi husika na wakati/muda unaotumika katika simulizi iliyosaidia katika kuhakiki jinsi simulizi rejelewa zimeshughulikia suala la mawanda ya wakati. Mwisho, data za aina hizi mbili zilioanishwa pamoja katika utafiti huu.

1.9.3 Uchanganuzi wa data

Data iliyokusanywa kutoka katika nyimbo teule ilipangwa kulingana na malengo ya utafiti ili kuipa mpangilio faafu uliorahisisha kuhusisha data pamoja na malengo ya utafiti na kujaribu kujibu maswali ya utafiti. Data rejelewa ilichanganuliwa kulingana na vipengele vifuatavyo;

(a) Maudhui yaliyoibuka katika nyimbo teule.

(b) Uzingativu katika vipengele vya ploti na wakati.

(c) Sauti ya usimuliaji pamoja na mahusiano ya wakati wa usimulizi.

1.9.4 Uwasilishaji wa matokeo

Matokeo ya utafiti huu yaliwasilishwa kwa mtindo wa kimaandishi wa aya jinsi mbinu ya masimulizi inavyojitokeza katika nyimbo za Bahati Bukuku. Hivyo basi, data za kiuthamano ndizo zilitumika kuwasilisha matokeo ya utafiti huu. Gray (2007) anafafanua kuwa data za kiuthamano zina utajiri mkubwa wa maelezo yanayofafanua matukio. Vilevile mtafiti alihakiki maudhui pamoja na kutilia maanani jinsi vipengele vya sauti ya usimuliaji pamoja na mahusiano ya wakati wa usimulizi vilijitokeza katika nyimbo teule za utafiti.

SURA YA PILI

USIMULIZI KATIKA NYIMBO TEULE ZA BAHATI BUKUKU

2.0 Utangulizi

Lengo la sura hii ni kuchunguza jinsi usimulizi ulivyojitokeza katika nyimbo za mwimbaji Bahati Bukuku. Utafiti umeanza kwa kutoa ufafanuzi wa dhana ya usimulizi kwa kuwarejelea wataalamu mbalimbali. Katika usimuliaji wa simulizi, kuna vipengele muhimu ambavyo huchangia katika kufanikisha muundo halisi wa simulizi hizo. Sura hii ya utafiti ilijikita katika vipengele viwili muhimu vinavyofanikisha muundo wa simulizi, ambavyo ni Ploti na Wakati.

Uchanganuzi wa ploti ulirejelea matumizi ya vipengele vyake muhimu kama; utangulizi maalum, tamati maalum, nafasi ya mhusika mkuu katika usimulizi pamoja na kilele cha usimulizi. Katika kuzingatia vipengele hivi vya ploti, utafiti huu unanuia kufafanua baadhi ya maoni ya wataalamu kuhusu vipengele hivi katika tungo pamoja na kutolea mifano mwafaka katika nyimbo teule.

Kwa upande mwingine, uchanganuzi wa wakati kama kipengele cha usimulizi ulirejelea vipengele vyake muhimu vya umara, muda pamoja na mpangilio. Kwa kuzingatia kipengele cha Umara, utafiti huu ulichanganua aina tatu za Umara, ambazo ni usimulizi rudufu, usimulizi banifu pamoja na usimulizi mosi.

Kwa upande mwengine, kipengele cha Muda kilihakikiwa kwa kuchanganua sehemu zake nne; muhtasari, udondoshi, onyesho na mtuo. Kipengele cha mwisho cha wakati cha mpangilio kitahakikiwa kwa kurejelea aina zake; analepsia (mbinu rejeshi) na prolepsia (mbinu elekezi).

2.1 Dhana ya Usimulizi

Kamusi ya Fasihi (2003) inaainisha usimulizi kama uelezaji wa matukio katika hadithi. Vilevile, kwa mujibu wa Barry (1995), usimulizi ni mtaala wa jinsi simulizi huleta maana. Anaeleza kuwa kazi nyingi za kifasihi mara nyingi huwa na kisa muhimu ambacho kinasimuliwa na msimulizi.

Usimulizi umetokana na fasihi simulizi ambayo ndiyo fasihi kongwe. Fasihi simulizi ndiyo ilichangia kuwepo kwa fasihi andishi, kwani ilikuwepo hata kabla ya maandishi kuwepo. Kama anavyohoji Mohammed (1995, uk.82), " Asili ya simulizi ni katika fasihi simulizi ambapo msimulizi yupo mbele ya hadhira hai ambayo inamuona, inamsikiliza, inajiunga pamoja naye katika usimulizi na hata kuwa na nafasi ya kumgusa msimulizi."

Kama anavyodokeza mwana-nadharia Genette (1980), kauli ya kisimulizi au kimaandishi ilivyodhamiria kulieleza tukio au matukio fulani, msuko halisi au ya kibunilizi pamoja na tendo lenyewe la kusimuliwa ndivyo vigezo vikuu katika usimulizi.

2.2 Ploti

Kwa mujibu wa maoni ya Njogu na Chimera (1999), ploti ni mtiririko wa vitendo na namna vitendo hivyo vinavyozuana. Maoni mengine kuhusu ploti yanatolewa na Wamitila (2003) anayeifafanua kama muundo wa hadithi. Anaendeleza kuwa ploti ni mpangilio wa matukio ya hadithi kuanzia mwanzo kwenye kitangulizi hadi mwisho wa usimulizi. Katika sehemu hii ya kitangulizi, panazuka mvutano wa hadithi ambao unaendeleza mgogoro kati ya wahusika walioko, kuwepo kwa taharuki, harakati zao hadi kwenye kilele cha hadithi au upeo na hatimaye mwisho wake.

Kwa kutilia maanani maoni ya wataalamu hawa, utafiti huu umefikia uamuzi kwamba ploti ni dhana muhimu katika fasihi ambayo hudhihirisha mtiririko wa matukio katika simulizi, kuanzia mwanzo hadi mwisho. Sura hii itahakiki ploti katika nyimbo teule za msanii Bahati Bukuku kwa kurejelea vipengele vyake muhimu kama; utangulizi maalum, tamati maalum, kilele au upeo na nafasi ya mhusika mkuu katika usimulizi. Kwa kurejelea vipengele hivi muhimu vya ploti, mifano maridhawa imetolewa ili kutathmini jinsi vipengele hivi vya ploti vimeathiri uwasilishaji wa

simulizi katika nyimbo teule. Ingawa suala la ploti limehusishwa sana na tungo za kinathari kama riwaya, tamthilia na hadithi fupi, ni muhimu vilevile kutambua kuwa ploti ni sehemu muhimu sana ya nyimbo zenye sifa za kihadithi.

2.2.1 Utangulizi maalum

Sehemu ya utangulizi wa simulizi ni muhimu sana kwani ndicho kipengele kinachodokeza mwanzo wa simulizi. Katika tathmini yake, Wamitila (2003) anafafanua kuwa simulizi huwasilishwa kwa hadhira kwa 'utendaji' ambao unaweza kuhusishwa na sifa kadhaa. Anaeleza sifa hizi kama mbinu na mikakati ya usimulizi au utambaji wa hadithi. Mbinu hizi anaziainisha kama muhimu sana katika shughuli za utambaji wa hadithi. Mojawapo ya mbinu hizi ni kuwa na uanzaji maalum katika utambaji huo. Anafafanua kuwa katika utambaji huwa kuna vitangulizi fulani maalum ambavyo aliviita fomyula ya utangulizi. Katika tathmini yake, fomula hizi maalum za utangulizi wa simulizi huwa na dhima kama; kuwavutia wasikilizaji na kuvuta makini yao, kumtambulisha mtambaji kwa hadhira, kuashiria mwanzo wa hadithi pamoja na kuweka mipaka wazi kati ya ulimwengu halisi na ule wa masimulizi.

Kwa mujibu wa Wamitila (keshatajwa), hadithi za kijadi zilikuwa na mtindo maalum wa kutangulizwa. Kwa mfano, *Paukwa pakawa , sahani ya mchele , kiboko cha mtoto mkorofi* na kadhalika. Hata hivyo, simulizi katika nyimbo teule za Bahati Bukuku zimeweza kukiuka mpangilio huu. Badala ya kuanza kwa kitangulizi hiki maalum, mwimbaji anaanza kwa hitimisho. Kwa mfano;

Mfano 1: *Maamuzi*

Maamuzi yako , matokeo ya kesho,
Amua vyema upate mema wewe
Maamuzi yako matokeo ya kesh
Amua vyema upate mema wewe

Alikuwepo mama mmoja wacha niseme
Jina lake aliitwa Tundo
Alisumbuliwa na ugumba miaka mingi
Ndoa yake ilikuwa matatani...

Usimulizi ndani ya wimbo huu wa *Maamuzi* umetangulizwa kwa mtindo wa msanii binafsi. Hii ni kwa sababu ya kukiuka fomyula maalum inayopasa kutanguliza hadithi yoyote ile. Hata hivyo, mwanzo huu umejitokeza kuwa muhimu sana kwani ulidhamiria kumtayarisha msikilizaji kwa yale yaliyomo katika usimulizi.

Vilevile, utangulizi huu umeibua mwanzo wa mgogoro unaojitokeza katika usimulizi wa mama mmoja aliyeitwa Tundo, aliyesumbuliwa na tatizo la kutofanikiwa mwana kwa miaka mingi. Baada ya kutafuta msaada kwingi pasi na kufanikiwa, Tundo anafanya uamuzi kwenda Kongo kwa mganga mashuhuri ili aweze kumsaidia kupata uwezo wa kupata mwana. Maamuzi yake yanaelekea kuwa na faida kwani Tundo aliweza kupata mwana kwa msaada wa mganga huyu, na akajifungua mtoto aliyemuita Sinona. Hata hivyo, hali zilianza kumbadilikia Tundo kwani mwili wake ulianza kubadilika. Ngozi yake ikawa kama magamba ya nyoka. Cha kushangaza ni kuwa Sinona alipozaliwa, alikuwa na meno yote kama mtu mzima.

Basi rafikize Tundo walimtembelea na kumwomba akaende kuombewa kanisani ili apate suluhu kwa shida alizokuwa akipitia baada ya kumpata Sinona. Anapofika kanisani na kuombewa, mtoto wake anabadilika na kuwa joka kubwa. Kumbe Sinona, aliyepatikana kwa nguvu za kiganga, hakuwa binadamu halisi. Hii ndiyo sababu za Tundo kuwa na matatizo mengi kama; uchungu mwilini, ngozi yake kubadilika, matiti yake kuvimba na kadhalika. Hivyo basi, kwa kutanguliza wimbo huu kwa hitimisho, anatayarisha hadhira kwa yale ambayo yamo katika hadithi, yanayoambatana na maamuzi anayochukua mhusika Tundo.

Mfano 2: *Tupatupa*

… Alikuwepo baba jina lake Tupatupa

Ebu ngoja kwanza,tulia nikwambie

Mfano huu wa utangulizi una mshabaha mkubwa na jinsi mafanani walivyotanguliza visa vya usimulizi moja kwa moja baada ya fomula ya utangulizi. Wamitila (2003) anaeleza kuwa simulizi hutangulizwa kwa vifungu fulani vya maneno kama ‘aliondokea’ au ‘hapo zamani za kale’. Hivi huwa vifungu vya maneno ambayo hurudiwa na huwa kama kaida fulani. Wamitila (keshatajwa) anaviita vifungu hivi vya maneno *virai-kaida*.

Kama inavyojitokeza katika utangulizi wa wimbo wa *Tupatupa*, msanii anatumia virai-kaida katika kutanguliza. Ingawa fomyula mahsusi ya kutanguliza hadithi haipo, mtindo binafsi aliotumia una umuhimu kwani unamtanguliza mhusika mkuu ambaye vitendo vyote katika usimulizi vilimzingira yeye.

Mzee Tupatupa analewa na kugongwa na gari kubwa kisha anaaga dunia. Baadaye anamtokezea malaika ambaye anamwambia achague ni wapi anapotaka kuenda, kati ya mbinguni na jehanamu. Malaika anamweleza kuwa siku yake ilikuwa nzuri kwani atapata nafasi adimu ya kutembelea mbinguni na jehanamu. Mzee Tupatupa anaelekea jehanamu na kupata hali ni shwari. Kulikuwa na wanawake warembo kuliko aliowaona duniani, vinywaji tele na raha mstarehe. Alipokutana na shetani, alipendezwa naye na kushangaa mbona walimwengu walimdhani shetani kuwa mtu mbaya. Alipopewa nafasi ya kutembelea mbinguni, alipata hali ni tofauti, kwani hakukuwa na vinywaji wala wanawake. Badala yake aliwaona watu waliokuwa wamevalia nguo nyeupe huku wakiimba na kuabudu.

Mzee Tupatupa hakupendezwa sana na aliyoyaona mbinguni, ndiposa akajaza kitabu cha wageni na kuomba kurudishwa jehanamu. Malaika alimsindikiza hadi jehanamu. Alipofika kule alishangaa jinsi mambo yalivyokuwa tofauti na awali, kwani aliona moto mkubwa ukiwachoma

watu. Mzee Tupatupa alishangazwa na jinsi shetani alivyokuwa akitisha kwa wekundu na mapembe. Hapo ndipo shetani, kwa ukatili mkubwa, alipomweleza kuwa kwa mara yake ya kwanza, alikuwa akifanya kampeni tu, ili kumvutia Tupatupa. Huo ukawa mwisho wa mzee Tupatupa.

Mbali na wimbo wa *Maamuzi* pamoja na *Tupatupa*, msanii Bahati Bukuku ametanguliza wimbo wa *Abneli* kitaharuki kwa kueleza mambo ambayo yanamshangaza katika maisha. Utangulizi wake unanata makini ya hadhira kwani umedhamiria kufafanua yaliyomo na yanayoelezwa na ufunguzi huo. Utangulizi huu vilevile umeweza kusaidia kwa uwasilishaji wa maudhui ya utamaushi kwani maneno anayotumia katika ufunguzi wake yanaoana moja kwa moja na yanayoelezwa ndani ya wimbo. Kwa mfano;

Mfano 3: ***Abneli***

Mbona huyu amefia hapa?
Kwa nini ?
Mbona huyu amenyongwa ?
Nashangaa ?
Nyumba za wageni zimejaa wizi…
Kwa nini ?
Taarifa za habari hakuna mapya…
Nashangaa!

Utangulizi huu pia ni muhimu kwani unadhihirisha toni ya wimbo huu unaosheheni usimulizi wa mhusika Abneli. Kwa mujibu wa Wamitila (2003), toni hufungamana kwa kiasi kikubwa na maswala anayoyazungumzia msanii. Kwa kuwa maneno anayoyatumia Bahati Bukuku katika utangulizi wake yanadhihirisha utamaushi wa msanii, hadhira inaangaziwa moja kwa moja kuhusu toni ya usimulizi utakaofuata. Hivyo basi, ingawa fomula maalum ya ufunguzi wa hadithi haujaweza kutumiwa, ni wazi kuwa utangulizi wake unakiuka mipaka ya kiusimulizi umeweza kusheheni umuhimu kwa upande mwingine.

2.2.2 Tamati Maalum

Kwa mujibu wa maoni ya Dundes (1999), simulizi zinapaswa kutamatishwa kwa upeo wa chini. Kulingana na tathmini hii ya Dundes, usimulizi haufai kuanza ghafla wala kukamilika ghafla, bali ni sharti uhitimishwe baada ya kuonyesha upeo wa chini wa aina ya kipekee. Hali ya kuwepo kwa tamati maalum pia inasisitizwa na Wamitila (2003) ambaye anaainisha fomula inayopatikana katika sehemu ya mwisho wa hadithi kama kimalizio. Wamitila (keshatajwa) vilevile anaorodhesha baadhi ya umuhimu wa kuwepo kwa kimalizio katika usimulizi kama; kuashiria kumalizika kwa utambaji, kuwa kama kitangulizi cha shughuli nyinginezo, kuashiria kupewa nafasi kwa mtambaji anayefuata pamoja na kuwa njia ya kuitoa hadhira katika makini ya uzingativu wa masimulizi yaliyotamatika.

Katika kutamatisha, nyimbo za Bahati Bukuku zinakamilika katika upeo wa chini. Bukuku amedhamiria kutamatisha kwa kutoa mafunzo nje ya simulizi katika nyimbo zake. Katika wimbo wa *Abneli*, msanii anatoa wosia kwa hadhira kujihadhari dhidi ya marafiki na pia maadui kwani duniani hakuna aliye na ufahamu kuhusu mipango ya yeyote. Anaeleza kuwa, “moyo wa binadamu umekunja ngumi” kumaanisha kuwa binadamu yu tayari kuleta madhara yasiyojulikana. Akitamatisha, msanii anasisitiza umuhimu wa msamaha katika kila jambo ili kuondoa vifo visivyotarajiwa na majanga mengine. Kwa mfano;

Mfano 4: ***Abneli***

Nyakati hizi tulizo nazo
Alama za nyakati zinaonyesha
Wanadamu wamechoka suluhu
wanaona maamuzi kuwa ni kifo
Jihadhari nao marafiki
Sio kila kicheko kinamaanisha furaha
Wengine wakichukia hucheka sana
Sio kila kicheko kinamaanisha upendo
Wengine wanataka wakusogeze tu

Wengine wanataka wakuweke karibu ili iwe sababu ya
Kutoa roho yako.

Tamati hii, kwa hivyo, ni ushauri kwa hadhira wawe waangalifu katika mahusiano yao, kwani binadamu anaweza kumdhuru mwenzake wakati wowote.

Mfano 5*: Dunia haina huruma*

Kumbe Mungu anaweza kusamehe
Kumbe Mungu anaweza kukuita tena
Kumbe Mungu anaweza kujibu maombi
Ndilo nililojifunza leo
Yesu wangu anajibu
Tena yeye anasikia
Pia tuombe bila kukoma
Nataka kutengeneza na Mungu
Lazima nitengeneze na Mungu
Nataka kutengeneza na Mungu
Lazima nitengeneze na Mungu

Wimbo wa *Dunia Haina Huruma* umetamatishwa pia kwa upeo wa chini. Vilevile, Bukuku amemshukuru Mungu kwa yote aliyomtendea baada ya kupitia mambo mengi magumu katika usimulizi wa wimbo huo. Kwanza, anabaini kuwa kumbe mume wake amekuwa na mke mwengine baada ya mke huyo kumpigia msimulizi kumjuza kuhusu kifo cha mumewe. Baadaye anabaini kuwa mume wake hajafa, bali yumo kwenye chumba cha wagonjwa mahututi, na anahitaji matibabu ya dharura.

Msimulizi anajaribu kwa kila hali kuwasihi jamaa na marafiki wamsaidie ili aweze kumtibu mumewe ila wote wanampuuza. Hapo anaamua kufanya mapenzi na daktari ili mumewe apate msaada, jambo linalopelekea msimulizi kuwa mjamzito. Baada ya muda mrefu, anaamua kumweleza mumewe kuhusu uzazi wa mwana wao, jambo linalosababisha msimulizi aitwe kijijini kwa kesi iliyomkabili ya kumwendea mumewe kinyume. Alipofika kule, wale waliompuuza msimulizi alipotaka msaada ndio wanaomhukumu kwa kosa alilotenda. Hata hivyo, mzee mmoja mwenye hekima anajitokeza na kuwasihi wamsamehe msimulizi kwani wote hawakukosa doa.

Haya yote aliyoyapitia msimulizi ndiyo yanasababisha kuwa na wingi wa shukrani kwa Mungu. Tamati ya wimbo huu inajitokeza kama funzo kwa msimulizi. Hakuamini kuwa Mungu angeweza kujibu maombi. Hata hivyo,baada ya kufanikiwa katika kurejesha penzi katika familia yake, anaamini kuwa Mungu kweli anaweza kujibu maombi na kumsamehea yeyote yule.

Kijumla, simulizi katika nyimbo hizi zimeonyesha mianzo na miisho maalum. Mfumo huu wa kimuundo na maumbo tengamano hata hivyo, haujatumika moja kwa moja kwa kutumia mifumo na fomula maalum za kutanguliza ama kutamatisha simulizi.

2.2.3 Nafasi ya mhusika mkuu katika usimulizi

Kwa mujibu wa Dundes (1999), akiirejelea nadharia ya Miundo na Maumbo tengamano katika kuhakiki masimulizi ya jadi, alieleza kuwa katika mfululizo wa matukio “mhusika mkuu” atajitokeza kwanza ilhali yule ambaye msimulizi anamwibulia hisia za huruma atajitokeza mwisho. Hivyo basi, mhusika mkuu hana budi bali kuhusika katika vitushi vingi katika tungo la kifasihi.

Katika usimulizi wa wimbo wa *Dunia haina huruma*, mhusika mkuu anajitokeza kuwa msimulizi. Hii ni kwa sababu matukio yote kuanzia mwanzo hadi mwisho yanamzunguka yeye. Kwanza kabisa, msimulizi ndiye anayehadithia matukio yake ambayo yote yanamhusu. Msimulizi vilevile anajitokeza pindi tu baada ya utangulizi wa usimulizi wake. Kwa mfano;

Mfano 6: *Dunia haina huruma*

Ni asubuhi na mapema
Simu ya mkononi inaita
Naitazama kwa makini
Ni namba za mume wangu
Sauti ya mwanamke inasikika
Inayorarua moyo wangu
Moyo wangu unafura hasira
Kwa taarifa ninazopata
“Hallo, nenda mwimbini kachukue mzoga wako.”...

Katika migogoro yote inayofanyika katika usimulizi huu, msimulizi ndiye pekee anakabiliana na hali ngumu ya kusuluhisha migogoro hiyo. Kwa mfano, msimulizi anapigiwa simu na kujuzwa kuhusu mauko ya mumeo, na anapouliza ni nani anampigia simu, anapokea jibu lenye ujeuri mkubwa. Uchungu wake unaanzia pale kwani hakufahamu kuhusu uwepo wa mke mwingine katika maisha yake.

Mfano 7: *Dunia haina huruma*

"Mimi ni mke mwenzio, kama hutaki potezea."

Anapoenda hospitalini na kumpata mume wake katika hali mbaya , msimulizi anawasihi ndugu na jamaa wa mume wake msaada lakini wanapeana visababu vinavyompa uchungu zaidi. Kwa mfano;

Mfano 8: *Dunia haina huruma*

Ninawapigia ndugu wa mume wangu
Yaliyomsibu mume wangu
Wote wananisusia...
Nawatafuta marafiki wa mume wangu
Na kwanza ninapofika hapo
Wanaanza kunipa masharti
Yanayorarua moyo wangu...

Mashemeji wamegoma kutoa msaada...
Nawatafuta mawifi kwa mara nyingine
" Tungeweza kukusaidia lakini wale wenzangu wacheza shengele watakuja siku ya jumamosi, kwa hivyo nimewaambia na siwezi kughairi kwa sababu wameshona sare."

Baada ya kukosa msaada kutoka kwa ndugu na jamaa, msimulizi anaamua kufanya mapenzi na daktari ili mume wake apewe matibabu. Hata hivyo, maamuzi yake ndiyo yanamfanya mume wake kukosa imani naye alipogundua ukweli. Kwa mfano;

Mfano 9: *Dunia haina huruma*

...niliamua kumwangukia daktari...
...mume wangu ile siku ulipocharazwa mapanga

Yule daktari aliyekuwa anakuuguza
Ndiye mwenye huyu mtoto
mume wangu alinitazama tu
akaondoka mbele yangu...

Baada ya kumweleza mume wake ukweli, alikasirika na kuelekea kijijini kutoa mashtaka kwa kosa alilofanya mkewe. Cha kutamausha kwa msimulizi, wale mashoga na mashameji aliowapigia simu wamsaidie mume wake alipokuwa katika hospitali, ndio waliokuwa tayari kumhukumu, ingawa walimsusia alipohitaji msaada wao.

Mfano 10: ***Dunia haina huruma***
Asubuhi na mapema nikaitwa kijijini
wakinisisitiza kwa hasira
"Kuja na mtoto wako akiwa hai."
Nilipofika kijijini niliwakuta mawifi zangu
Kila niliyemsalimu hakuweza kunijibu...

Niliowaomba msaada ndio walionihukumu
"Mtoto wako lazima auawe maana sisi hatumtambui
mtoto haramu katika familia yetu..."

Ingawa msimulizi anapitia hali ngumu asiyoweza kudhibiti, mzee mmoja anajitokeza na saluhu la kudumu linalookoa maisha ya mwanawe msimulizi.

Mfano 11: ***Dunia haina huruma***
...mzee mmoja mwenye busara alisimama na kusema
" Iwapo kuna yeyote ambaye hana dhambi, na awe wa kwanza kupiga mapanga."
Wote wakatazamana
Hakuna aliyeniangalia.

Hivyo basi , kuwepo kwa msimulizi katika utangulizi wa mgogoro, kilele cha mgogoro na suluhu ya mgogoro kunaonyesha wazi nafasi yake kubwa na muhimu katika usimulizi huu.

Katika wimbo wa *Tupatupa,* mhusika mkuu anajitokeza kuwa Mzee Tupatupa. Mzee huyu anajitokeza kuanzia mwanzo wa usimulizi hadi mwisho. Anapotanguliza usimulizi, msimulizi

anamtaja mhusika huyu moja kwa moja ili ibainike wazi kuwa mhusika ndiye ataongoza vitushi vyote katika usimulizi.

Mfano 12: *Tupatupa*

...Alikuwepo baba jina lake Tupatupa
Ebu ngoja kwanza, tulia nikwambie

Maelezo ya awali yanajitokeza akiwa hai ambapo usimulizi unamsawiri mhusika Tupatupa kama mhusika mkware ili kufanya hadhira ielewe kabisa kuhusu chanzo cha mgogoro unaojitokeza katika usimulizi. Kwa mfano;

Mfano 13: *Tupatupa*

Alikuwepo baba jina lake Tupatupa
Alikuwa tajiri tena mwenye sura nzuri
Kila aliyemwona alijua mambo sawa
Mzee Tupatupa alipoona wadada
Kila aliyemwona alijua amepona
Mambo yake yalikuwa hivi,
"Mtoto mzuri,malkia,malkia,malkia,mrembo
kama wewe unatembea chini?Mimi nikikuoa nitakununulia
ndege uifanye kama daladala. Nitakuwa nakupeleka
huko Kariako,wakati mwingine Masaki,nitaifanya
dunia iwe kijiji kidogo kwako."

Kwa kuzingatia maneno aliyoyasema mhusika Tupatupa wakati alipowaona wadada, sifa ya ukware inajitokeza wazi. Maneno "Mtoto mzuri, malkia, malkia, mrembo kama wewe unatembea chini? Mimi nikikuoa nitakununulia ndege..." yanafafanua msingi wa ukware wake, ambao mbali na kuutumia duniani, uliathiri tabia zake alipoenda jehanamu kwa mara ya kwanza.

Baadaye, chanzo cha kifo chake kinaelezwa. Mtunzi aliambatanisha aina ya maisha yake pamoja na kifo chake ili kusaidia uelewaji zaidi wa maamuzi atakayofanya mbeleni mhusika huyu.

Jinsi anavyosawiri akiwa hai, ndivyo tabia na mienendo yake inavyojitokeza katika jehanamu ambapo anapendezwa na wanadada aliokutana nao kule. Kwa mfano;

Mfano 14: *Tupatupa*

...Tupatupa siku moja alilewa
Aliona taa mbili zinakuja
Siku hiyo ilikuwa siku mbaya kwake
Aliona taa mbili zinakuja mbele
Aliona bila shaka hawa ni madereva wawili wa bodaboda wanashindana
Jamani kumbe hakuwa dereva wa bodaboda
Ila lilikuwa gari la kubeba mchanga, yaani lori
Yule dereva wa lori alijaribu kuhepa
Lakini kwa kuwa mzee Tupatupa alikuwa kalewa
Akaendelea kusimama katikati ya barabara
Akitaka kuonyesha wale vijana kwamba yeye ni mwanamume,
Na kizito wa eneo hilo.
Dereva wa lori alijitahidi kukwepa
Lakini ilishindikana
Mzee Tupatupa aligongwa
Akapoteza fahamu palepale...

Jehanamu siku hiyo kulipendeza
Kulikuwa na wasichana warembo ata kuliko wale wa duniani...

Mtunzi vilevile anamtumia mhusika Tupatupa kufafanua mandhari ya mbinguni na ile ya jehanamu ili kuweka wazi sababu za Mzee Tupatupa kuchagua na kupendelea jehanamu kuliko mbinguni. Maamuzi yake yanamtia mashakani kwani anajuta baada ya ukweli kujitokeza kumhusu shetani ambaye alimhadaa hapo mbeleni. Kwa mfano;

Mfano 15: *Tupatupa*

...Kwa kweli Jehanamu siku hiyo kulivutia sana ...
...Hayo ndiyo maneno ambayo alijinadi nayo siku hiyo shetani...
...Kwa kweli siku hiyo shetani alijieleza kwa ufasaha...
"...Hapana, jana kulikuwa na starehe, jana kulikuwa na wanawake wazuri..."

...Mzee Tupatupa
Muda umekwisha
Sasa twende Mbinguni
Alipofika Mbinguni akakuta malaika
Wao wanaimba
Tena wanasujudu.

Kwa hivyo, kuwepo kwa mzee Tupatupa katika sehemu zote za usimulizi kunampa nafasi kubwa kuliko wahusika wengine hadithini, kwa mfano Shetani, Malaika, Yesu pamoja na wanawake wale aliowapenda sana Tupatupa.

2.2.4 Kilele cha usimulizi

Kwa mujibu wa Senkoro (1982), katika kazi yoyote ya kifasihi au kisanaa, huwa kuna upeo wa chini na wa juu. Katika tathmini yake Senkoro, upeo wa chini ni pale ambapo haja na matazamio ya msomaji, msikilizaji ama mtazamaji haikidhiwi. Maoni mengine kuhusu upeo wa chini yanatolewa na Wamitila (2003) ambaye anarejelea upeo huu wa chini kama ufunguzi. Katika uwasilishaji wake, Wamitila (keshatajwa) anaeleza kuwa kazi za kifasihi huwa na sehemu tatu muhimu ambazo lazima ziwepo ili kufanikisha uwasilishaji wa kazi hizo. Wamitila anataja sehemu ya kwanza kuwa Ufunguzi, ambapo mwandishi anapaswa kuyaonyesha mambo yanayoathiri matukio mapema. Kwa mfano;

Mfano 16: ***Maamuzi***

Alikuwepo mama mmoja ngoja niseme
Jina lake aliitwa Tundo
Alisumbuliwa na ugumba miaka mingi
Ndoa yake ilikuwa matatani
Hata mawifi zake wote hawakumpenda tena
Tundo aliamua kwenda kwa waganga
Alizunguka huku na kule kutafuta msaada
Aliona bora aende kwa waganga tundo

Kwa kurejelea tathmini ya Wamitila (2003) kuhusu ufunguzi, mfano uliotolewa unathibitisha wazi mwanzo wa migogoro aliyokuwa nayo mhusika Tundo. Tatizo lake la utasa linatajwa, na ni tatizo hili ambalo linaathiri maamuzi yake yote katika sehemu zinazofuata hadithini. Utasa ndio uliomlazimu aende Kongo kutafuta waganga ili wamsaidie na uwezo wa kupata mtoto, kwani

maisha yake Tundo yalikuwa yameanza kuharibika kwa kutopendwa na mawifi zake pamoja na ndoa yake kuwa matatani.

Sehemu ya pili muhimu katika kufanikisha kazi ya kifasihi, kwa mujibu wa Wamitila (2003), ni Upeo. Wamitila (keshatajwa) anafafanua kuwa upeo ni kile kilele cha tendo au matendo yanayopatikana katika kazi ya fasihi. Wamitila (keshatajwa) anaeleza kwamba upeo unafaa kutosheleza matarajio au kuyageuza kwa mshtukizo pamoja na kufumbata ukamilifu au utoshelezi wa tukio. Kwa mfano, baada ya Tundo kusumbuliwa na tatizo la utasa na kuelekea kwa mganga kule Kongo ili kutafuta msaada, hatimaye alifanikiwa kupata mtoto aliyemuita Sinona. Kilichoshangaza ni kuwa, alipozaliwa Sinona, alikuwa na meno kama ya mtu mzima. Baada ya muda, Tundo alianza kuugua kwa maradhi asiyoyaelewa kwa sababu ya Sinona, kwa mfano, maumivu makali wakati alipokuwa anamnyonyesha Sinona pamoja na ngozi yake Tundo kubadilika na kufanana na magamba ya nyoka. Kwa mfano;

Mfano 17: *Maamuzi*

Maajabu aliyokuwa nayo mtoto yule
Alikuwa amezaliwa na meno
Maajabu aliyokuwa nayo Sinona
Alizaliwa na meno kama mtu mzima…

Lakini alipokuwa akinyonyesha mtoto yule
Ghafla aliung'ata mwili wake Tundo
Mwili ukapoa wote upande mmoja
Lilikuwa ni tatizo lililomsumbua Tundo…

Rangi ya ngozi yake Tundo
Iligeuka ikawa gamba la nyoka mwili wake mzima…

Siku moja Tundo alitembelewa na rafikize pale nyumbani, na kwa kumuona alivyokuwa akiteseka, wanamsihi Tundo aende akaombewe kanisani. Kitendo cha upeo kinajitokeza wakati alipokuwa akiombewa Tundo, Sinona anabadilika na kuwa Chatu. Kitendo hiki kinawashtua waliokuwepo pale kwani kilikuwa cha kuajabia. Kwa mfano;

Mfano 18: *Maamuzi*

Muhubiri akamwambia Tundo
Mshushe mtoto wako hapa kwenye madhabao
Akaomba kwa Imani sana
Mtoto akageuka chatu mara ile
Eti Sinona sio mtoto, kumbe Sinona ni Chatu
Kumbe Sinona sio mtoto
Kumbe Sinona ni joka kubwa…

Watu wote kwenye mkutano wakakimbia
Waandishi wa habari wakapiga picha
Ni kweli unaweza kushangaa
Lakini ndiyo yalimpata Tundo…

Kwa kurejelea kitendo hiki cha Sinduna kubadilika na kuwa chatu, inambainikia msikilizaji sababu za Tundo kupitia matatizo aliyokumbana nayo baada ya kujifungua mwana Sinona. Baada ya hatua ya upeo, Wamitila (2003) anaainisha hatua ya Ufumbuzi. Hii ni ile sehemu ambapo msuko unafumbuliwa na suluhisho la mgogoro uliokuwepo kupatikana. Anafafanua kuwa, katika sehemu ya ufumbuzi, tukio linakamilika. Wimbo wa *Maamuzi* unadhihirisha ufumbuzi pale alipoitwa mume wake Tundo na kwa kuyaona yaliyotendeka, akakubali kuwa halikuwa jambo la busara kumwendea mganga ili tatizo la utasa litatuliwe. Kwa mfano;

Mfano 19: *Maamuzi*

Wahubiri walimtuma nenda kamwite mme wako
Mume alipokuja akaambiwa
Huyo ndiye mtoto wako Sinona
Yule baba alilia sana
Akasema mganga mbaya
Yule baba alilia kwa uchungu
Akasema kumbe ni mganga
Yule baba alilia sana
Akasema Mungu wangu ee nisamehe
Akalia kwa uchungu huku na huku
Kumbe mganga alitudanganya Tundo
Kumbe Sinona sio mtoto…

Ufafanuzi zaidi wa Senkoro (1982) unaendeleza kuwa tukio la kilele huwa limeimarika na la kuvutia au kunata sana urazini na makini ya hadhira, kwani taharuki ya kutojua sababu za migogoro ya mhusika fulani inajibiwa. Hadhira inayosikiliza au kusoma inatakiwa kuitambua au kuiandika hadithi hiyo tena kutokana na kumbukumbu za kilele cha usimulizi huo. Ujenzi wa ploti ya hadithi hiyo huwa umefungika katika tukio hilo.

Mfano 20: *Ahabu*

Ilifika wakati Elia akasema
Waitwe manabii wote mia na hamsini
Na ijulikane upo Mungu unayeishi
Kama Baali ni Mungu basi leo
Tutamwabudu
Na kama Mungu yupo basi leo tutamjua
Mmh Ahabu, Ooh Ahabu
Wakajikusanya mabaalia wote
Mia nne na hamsini wakaandaa sadaka yao
Ya kuteketezwa
Elia akawaambia Iteni Mungu
Lakini Mungu wa Baali hakushuka tena
Elia akawaambia Muamusheni
Mungu wa Baali hakuamuka
Baali hakuamuka na wala hakuwasaidia
Elia akasimama tena
Akaandaa sadaka yake
Akawaambia leteni maji
Sadaka yangu imwagiliwe
Akajipiga kifua chake
Na ujulikane Mungu wa Elia
Moto kutoka mbinguni ulishuka
Ulibeba sadaka ya Elia kila kitu
Wale miungu wa Baali wote
Walitetemeka

Kilele cha wimbo wa *Ahabu* kinabainika kuwa wakati moto mkubwa unashuka kutoka mbinguni na kuteketeza dhabihu ya nabii Elia. Kilele hiki kilidhamiria kuamua Mungu wa kweli na mungu asiye wa kweli kuabudiwa. Msingi wa usimulizi huu unapatikana katika *Bibilia Takatifu*,

(Wafalme wa Kwanza 17:1-45*)*. Moto mkubwa unashuka na kuteketeza dhabihu ya Elia, hata baada ya Elia kueleza kuwa sadaka yake imwagiwe maji. Alisisitiza hili kwani alitaka kuonyesha kuwa nguvu za Mungu wake zilikuwa zaidi na hata zilizoweza kudhibiti ukali wa maji yaliyomwagwa.

Kilele hiki vilevile kinajitokeza mwisho baada ya manabii wa Baali kujaribu kuteremsha moto kutoka kwa miungu yao bila ya mafanikio. Iwapo Elia angeanza kwa kuomba basi haingekuwa na maana kwa manabii wa Baali kupanga dhabihu yao kwani ingekwisha bainika aliye Mungu wa kweli. Hii ndiyo sababu kilele hiki kinajitokeza kama kipengele muhimu sana katika msuko wa usimulizi wa wimbo huu.

Inavyobainika, vipengele hivi vya utangulizi na tamati, kilele pamoja na nafasi ya mhusika mkuu vimeweza kufanikisha uhakiki wa kipengele cha ploti kwa kurejelea nyimbo teule za msanii Bahati Bukuku.

2.3 Kipengele cha Wakati

Kwa mujibu wa Rimmon-Kenan (1983), wakati unajitokeza kuwa kipengele muhimu cha usimulizi. Rimmon-Kenan alitoa ufafanuzi uliohusu wakati-hadithi na wakati matini. Mbinu hii imeweza kudhihirika pakubwa katika nyimbo teule za Bahati Bukuku. Wahusika pamoja na matukio yanapatikana katika dhana hii ya wakati. Utafiti huu ulilenga kuchanganua vipengele vya wakati kama Umara, muda na mpangilio. Kazi hii, kwa hivyo, imeshughulikia jinsi kipengele cha wakati kinavyodhihirika katika nyimbo teule za Bahati Bukuku kwa kuhakiki uhusiano uliopo baina ya hadithi na matini kwa kutilia maanani vipengele vilivyotajwa vya wakati.

2.3.1 Kipengele cha Umara

Dhana hii inarejelea idadi ya mara tukio limeweza kutokea katika hadithi na matini. Tukio moja linaweza kujirudia katika matini kwa kujitokeza katika sehemu tofauti za matini moja. Kwa mfano, Genette (1980), anayerejelea dhana ya Umara kama idadi marudio, anaeleza kuwa umara ni mahusiano kati ya simulizi na daigesia. Tukio haliwezi kutendeka tu, bali pia linaweza kutendeka tena na tena au kurudiwa. Aidha, kauli ya kisimulizi haiwezi kutolewa tu bali pia kutolewa au kuandikwa tena na tena au kurudiwa mara nyingi katika matini hiyo hiyo.

Tathmini ya Wamitila (2002) kuhusu Umara inawiana na maoni ya Genette (1980) kwamba ni dhana inayorejelea mara ambazo matukio hutokea katika hadithi. Wamitila ameainisha usimulizi mosi, usimulizi rudufu na usimulizi banifu kama aina za Umara. Hivyo basi, utafiti huu ulichanganua jinsi aina hizi za umara zimeweza kujitokeza katika nyimbo teule za Bahati Bukuku.

2.3.1.1 Usimulizi mosi

Aina hii ya Umara hutokea wakati tukio limetokea mara moja na kusimuliwa mara moja tu katika hadithi. Aina hii ya usimulizi imedhihirika katika wimbo wa *Tupatupa* ambapo kifo cha Tupatupa kimesimuliwa mara moja pekee na kujitokeza mara moja pekee katika matini. Baada ya kusimuliwa kwa kifo chake, matukio yaliyofuata hayakuwa na uhusiano wa aina yoyote na tukio hilo. Kwa mfano;

Mfano 21: *Tupatupa*

Tupatupa siku moja alilewa
Aliona taa mbili zinakuja
Siku hiyo ilikuwa siku mbaya kwake
Aliona taa mbili zinakuja mbele
Aliona bila shaka hawa ni madereva wawili wa bodaboda wanashindana
Jamani kumbe hakuwa dereva wa bodaboda
Ila lilikuwa gari la kubeba mchanga, yaani lori
Yule dereva wa lori alijaribu kuhepa
Lakini kwa kuwa mzee Tupatupa alikuwa kalewa

Akaendelea kusimama katikati ya barabara
Akitaka kuonyesha wale vijana kwamba yeye ni mwanamume,
Na kizito wa eneo hilo.
Dereva wa lori alijitahidi kukwepa
Lakini ilishindikana
Mzee Tupatupa aligongwa
Akapoteza fahamu palepale...

Inavyobainika katika vitushi vyote vya wimbo huu wa *Tupatupa*, mhusika Tupatupa aliweza kuhusika katika ajali alipogongwa na Lori kisha akafa. Matukio yote yaliyofuata tukio hili la ajali lililomkumba Tupatupa hayakuwa na uhusiano wowote na kifo chake. Hivyo basi, kwa kuwa tukio hili halikudhihirika kwingine, ni wazi kuwa kipengele cha usimulizi mosi kimeweza kudhihirika. Katika usimulizi wa mhusika kipofu Barthimayo, katika *Bibilia Takatifu*, (Marko 10:46-52), maisha yake Barthimayo yanabadilika baada ya kuponywa na Yesu na kutoka upovuni. Kitendo cha kuponywa kutoka kwa kuwa kipofu hadi aweze kuona kinajitokeza mara moja na kusimuliwa mara moja. Kwa mfano;

Mfano 22: *Barthimayo*

Barthimayo kipofu aliketi kando ya barabara
Akisubiri wapitaji ili wamhurumie
Yesu alipopita ndipo kamhurumia
Historia ya maisha yake
Yote ilibadilika

Maneno ya dondoo hili la wimbo wa *Barthimayo* yanadhihirisha kuwa historia ya maisha ya Barthimayo iliweza kubadilika baada ya kupokea uponyaji kutoka kwa Yesu. Hii inadhihirisha kuwa kitendo cha uponyaji hakikujirudia tena katika maisha yake, na kiliweza kutendeka mara moja pekee.

2.3.1.2 Usimulizi rudufu

Huu ni usimulizi ambao huhusisha tukio likitokea mara moja lakini linasimuliwa zaidi ya mara moja katika matini. Kwa mfano, katika wimbo wa *Tupatupa*, dereva wa lori lililomgonga Tupatupa alijaribu kuliepusha gari ili lisimgonge Tupatupa. Tukio hili lilikuwa la mara moja. Hata hivyo, katika ubeti wa pili wa wimbo huu, tukio la kujaribu kuliepusha gari lisimgonge Tupatupa limeendelezwa mara mbili. Kwa mfano;

Mfano 23: *Tupatupa*

... Yule dereva wa lori alijaribu kuhepa
Lakini kwa kuwa mzee Tupatupa alikuwa kalewa
Akaendelea kusimama katikati ya barabara
Dereva wa lori alijitahidi kukwepa
Lakini ilishindikana**...**

Hivyo basi, kwa kuwa tukio moja la kukwepa limeendelezwa mara mbili, dhana ya usimulizi rudufu imeweza kudhihirika. Mfano mwingine wa usimulizi rudufu umejitokeza katika wimbo wa *Maamuzi*. Baada ya kupewa ushauri wa kwenda kanisani kuombewa, Tundo alihudhuria ibada. Kitendo cha Tundo kuitwa mbele na mhubiri limesimuliwa mara mbili katika beti mbili tofauti ingawa lilijitokeza mara moja pekee. Kwa mfano;

Mfano 24: *Maamuzi*

... Alipokuwa mhubiri akihubiri
Alimwona Tundo mbele yake
Akamwambia mama njoo mbele
Tundo akasogea akijua muujiza umefika

Akamwambia Tundo njoo mbele
Tundo akijua Mungu amesikia
Mchungaji akauliza
Mhubiri akauliza**...**

Mhusika Tundo alipoitwa na mhubiri, alienda mbele akijua muujiza wake umefika. Kitendo cha kuenda mbele ya kanisa kinajitokeza mara moja pekee ila kinaendelezwa mara mbili na mwandishi.

2.3.1.3 Usimulizi banifu

Huu ni usimulizi ambao huibuka wakati tukio linalojitokeza mara kadhaa linasimuliwa mara moja katika matini. Katika wimbo wa *Ahabu*, unaosheheni usimulizi wa Waisraeli wakati wa utawala wa mfalme Ahabu, katika *Bibilia Takatifu*, (Wafalme wa kwanza, 17:1-45), Waisraeli walimuudhi Mungu kwa njia mbalimbali, ila katika usimulizi wa wimbo wa Ahabu, hali hii imeendelezwa mara moja pekee katika matini. Kwa mfano;

Mfano 25: *Ahabu*

Wakati wa utawala wake Ahabu
Israeli walimtenda Mungu
Israeli waligeukia njia mbaya**...**

Kijumla, usimulizi unadokeza kuwa wakati wa mtawala Ahabu, Israeli iligeukia mienendo mbaya. Kitendo cha kugeukia mienendo mbaya kimeendelezwa mara moja pekee. Hata hivyo, Israeli ilikuwa imemuudhi Mungu kwa njia kadha. Kwa mfano, katika *Bibilia Takatifu*, (Wafalme wa kwanza;16, 17, 18, 19 na 20), baadhi ya maudhi ya Waisraeli kwa Mungu yalikuwa; kuidhinisha ndoa kati ya Waisraeli na wahusika kutoka mataifa mengine, kuabudu miungu ya Baali badala ya kumwabudu Mungu wa mbinguni, kuongezeka kwa manabii wa uongo wa Baali na kadhalika. Hata hivyo, maudhi haya hayakuendelezwa moja baada ya nyingine na mwasilishaji wa wimbo unaosheheni usimulizi huu, bali yamejumuishwa katika mshororo mmoja unaosema kuwa Israeli waligeukia njia mbaya. Mfano huu unadhihirisha matumizi ya usimulizi banifu.

Usimulizi banifu vilevile unajitokeza katika wimbo wa *Dunia haina huruma.* Wakati msimulizi alipofika kijijini ili kujibu maswali yaliyohusiana na mwanawe, baada ya mume wake kutambua siri kuwa mtoto hakuwa wake, aliwapata mawifi zake katika kikao wakimsubiri. Kulingana na msimulizi, kila mmojawapo wa mawifi hawa alikuwa akimtazama kwa dharau. Kitendo cha

kutazamwa na mawifi hawa kilitendeka tofauti, hatua baada ya hatua, msimulizi alipokuwa akiwatazama mmoja baada ya mwingine. Kwa mfano;

Mfano 26: ***Dunia haina huruma***

Nilipofika kijijini, nikawakuta mawifi zangu
Kila niliyemsalimia hakuweza kunijibu
Mashemeji walionipenda nao pia
Nilifanya vivyo hivyo, kila aliyenitazama,
alinitazama kwa dharau.

Msimulizi hakuwa na uwezo wa kuwatazama mawifi na mashemeji wote kwa wakati mmoja, bali mmoja baada ya mwingine. Hata hivyo, hali hii inaendelezwa mara moja tu katika matini.

2.3.2 Kipengele cha Muda

Muda ni uhusiano wa kiwakati katika hadithi. Hupima kipindi kilichochukua tukio kutokea. Wamitila (2002) anaeleza muda kama dhana inayorejelea uhusiano katika hadithi. Hufungamana na wakati anaochukua mtu fulani kusoma hadithi fulani, jambo ambalo ni gumu kuhakiki kwa sababu ya tofauti kati ya wasomaji tofauti tofauti katika matini. Rimmon-Kenan (1983) anapendekeza muda uangaliwe kupitia wakati-hadithi ambao hupimwa kiwakati, kuanzia sekunde hadi miaka, na wakati matini ambao hupimwa kikurasa. Genette (1980), ameugawa muda katika vigezo vinne; Muhtasari, udondoshi, onyesho na mtuo.

2.3.2.1 Kigezo cha Muhtasari

Katika muhtasari, kasi ya usimulizi huharakishwa. Hili hujitokeza kwa kufupisha kisa kirefu ambacho kilichukua muda mwingi katika usimulizi kwa maneno machache. Katika wimbo wa *Barthimayo,* msanii Bahati Bukuku ananuia kutoa ushauri katika wimbo kwa kufupisha kisa kirefu katika *Bibilia Takatifu*, (Marko 10:46-52), kwa kutumia ubeti mmoja pekee wa wimbo. Kwa mfano;

Mfano 27: *Barthimayo*

Barthimayo kipofu aliketi kando ya barabara
Akisubiri wapitaji ili wamuhurumie
Yesu alipopita ndipo kamhurumia
Historia ya maisha yake
Yote ilibadilika...

Matukio yanayomzingira Barthimayo yalikuwa mengi. Barthimayo alikuwa na uzoefu wa kuketi kando ya barabara ili apokee huruma na michango kutoka kwa wapita njia. Katika utunzi wa usimulizi huu, msanii Bahati Bukuku hajihusishi kutaja matukio yote yanayomzingira Barthimayo kabla ya siku alipopita Yesu. Vilevile, wakati alipokuwa akipita Yesu, kuna matendo mengi yaliyotokea kabla amfikie Yesu. Hata hivyo, haya yote hayaelezwi na mwandishi. Badala yake, anaenda moja kwa moja kwa kile alichokidhamiria kuwasilisha. Anasimulia matukio yote kwa ubeti mmoja wenye mishororo minne. Kwa kuwasilisha matendo yaliyofupishwa kwa ubeti mmoja, kigezo cha muhtasari kinabainika.

Kuna matumizi ya muhtasari katika usimulizi wa Yusufu katika wimbo wa *Mbeba Maono.* Hadithi ya Yusufu katika *Bibilia Takatifu*, (Mwanzo 37 na Mwanzo 44), iliyojenga msingi wa wimbo huu, ni ndefu kwani inasimulia maisha ya Yusufu, hadi alipouzwa utumwani, alipofungwa gerezani, alipofafanua ndoto ya Waziri Mkuu wa Misri hadi alipokuwa Waziri Mkuu mwenyewe. Kwa mfano;

Mfano 28: *Mbeba maono*

Ndoto ya Yusufu,alipowaambia ndugu zake
Maono ya Yusufu alipowaambia ndugu zake
Kwamba ameona wakimwabudu,wakimsujudu
Ndoto ya Yusufu, ndicho kilikuwa chanzo
Ndoto ya Yusufu kilikuwa ni chanzo cha vita vyake...
Ndoto ya Yusufu kweli ilichelewa
Akatupwa gerezani,ndoto ilichelewa
Lakini mwisho wa siku ndoto ilitimia

Wale waliomuuza utumwani ndio waliomwangukia tena...

Katika wimbo wa *Mbeba maono,* mtunzi amefupisha matendo yaliyochukua muda mrefu, kwa maneno machache katika wimbo. Kwa kuwa muda wa kuwasilisha ni mchache, msanii anafupisha matendo ya miaka mingi katika ubeti wa wimbo mmoja, hivyo kubainisha matumizi ya muhtasari.

2.3.2.2 Kigezo cha Udondoshi

Hiki ni kigezo kingine muhimu cha kudhihirisha muda. Udondoshaji hudhihirika wakati kasi ya masimulizi iko juu sana. Katika hali hii, wakati-hadithi huendelea ilhali wakati-matini hauendelei. Kwa hivyo, kuna hali ya kutosimuliwa kwa baadhi ya matukio. Kwa mujibu wa Genette (1980), udondoshaji hujitokeza kwa njia mbili; Udondoshaji bayana na udondoshaji uso kikomo.

2.3.2.2.1 Udondoshaji bayana

Katika udondoshaji bayana, matini huonyesha wazi kiasi cha muda ambao umeachwa nje katika simulizi. Msimulizi anabainisha wazi kiasi cha muda ambao umepita kabla ya tukio lingine kujitokeza. Aina hii ya udondoshaji inajitokeza katika wimbo wa *Dunia haina huruma*. kwa mfano;

Mfano 29: *Dunia haina huruma*

...Mume wangu alinitazama tu
Akaondoka mbele yangu
Asubuhi na mapema nikaitwa kijijini
Wakanisisitiza kwa hasira
“Kuja na mtoto wako akiwa hai.”

Katika mfano huu, inabainika wazi kuwa msimulizi alimweleza mumewe ukweli kuhusu uzazi wa mtoto wao siku iliyopita, mume wake akaondoka na kwenda kijijini siku hiyo na kilichofuata ni kuwa msimulizi anapokea habari asubuhi na mapema aelekee kijijini akiwa na mtoto wake. Matukio ya baada ya kutoka kwa mumewe msimulizi yanadondoshwa bayana hadi matukio ya kijijini siku iliyofuata, hivyo kudhihirisha matumizi ya udondoshaji ulio wazi.

2.3.2.2.2 Udondoshaji usio wazi/kikomo

Hii ni aina ya udondoshaji inayotokea pale ambapo muda unaorejelewa haujitokezi au kudhihirika waziwazi. Hii ina maana kuwa muda wa mabadiliko haujatajwa au kuwekwa dhahiri. Udondoshaji huu unadhihirika katika wimbo wa *Lazima Usamehe*. Kwa mfano;

Mfano 30: *Lazima usamehe*

Nilikuwa na rafiki yangu mzuri
Aliyeugua ugonjwa wa ajabu
Kwa huruma zangu nikamhurumia
Nikatumia muda wangu mwingi
Nikazunguka huku na kule kutafuta madktari
Nikatembea huku na kule kutafuta uzima wake
Lakini Mungu sio mwanadamu
Niliposema Mungu mponye,
Alinihurumia

Akaachilia uzima moyoni mwake akawa mzima
Nikatafuta ata wachungaji nao wakamwombea
Lakini Mungu si mwanadamu
Alinisikia
Alisikia
Cha kushangaza alipopona,malipo yangu
Aligeuka adui yangu
Amekuwa msiba wangu...

Mfano huu wa wimbo wa *Lazima usamehe* unahadithia kuhusu uhusiano kati ya msimulizi pamoja na rafikiye wa muda mrefu. Rafiki huyu aliweza kusumbuka kwa ajili ya ugonjwa kwa muda mrefu sana. Ilimbidi msimulizi kumshughulikia rafikiye kama impasavyo rafiki mwema wakati wa tatizo. Msimulizi aliweza kumtafutia rafikiye msaada kwingi ila hakupona. Msimulizi vilevile alimlilia Mungu ili rafikiye aweze kupona. Baada ya kupona, msimulizi anaomboleza kuwa rafikiye alimgeuka kwa vyote na kusahau msaada aliompa. Ndiposa anaapa kuwa hawezi kumsamehe kwa vyovyote. Kwa kurejelea muktadha huu, kwanza, haijitokezi bayana muda halisi uliopita kwa rafikiye msimulizi kuugua. Vilevile, haijitokezi waziwazi muda haswa wa Mungu kumponya

rafikiye msimulizi baada yake kumtafutia msaada kutoka kwa watumishi wa Mungu ili waweze kumwombea. Aidha, kingine kisichobainika wazi ni ule muda aliochukua rafikiye msimulizi, baada ya kupona, kumgeuka. Hadhira haina uhakika iwapo ilichukua siku moja, wiki, mwezi na kadhalika. Hivyo basi, inavyojitokeza, utafiti huu umebainisha matumizi ya udondoshaji usio wazi katika wimbo wa *Lazima usamehe*.

2.3.2.2.3 Udondoshaji batini

Kwa mujibu wa Genette (1980), udondoshaji batini hudhihirika pale muda katika hadithi haujasemwa. Msomaji anaposoma matini, hubaini mwenyewe kwamba kati ya tukio moja na lingine katika matini, kuna muda fulani ambao umepita. Matukio ambayo yanafuatana kiwakati yanapodhihirisha mwanya, basi udondoshaji batini unadhihirika. Katika wimbo wa *Tupatupa*, kuna udondoshaji batini kati ya muda ambao mhusika Tupatupa anagongwa na lori hadi anapojiwa na malaika kuulizwa anapotaka kwenda, mbinguni ama jehanamu. Kwa mfano;

Mfano 31: *Tupatupa*

...Dereva wa lori alijitahidi kukwepa
Lakini ilishindikana
Mzee Tupatupa aligongwa
Akapoteza fahamu
Malaika akatokea
Akamuuliza Tupatupa
Kuna njia mbili mbele yako
Unataka kwenda wapi?...

Kwa mujibu wa dondoo hili, inabainika kuwa kati ya tukio la kwanza la Mzee Tupatupa kugongwa na lori na tukio la pili la malaika kutokea, kuna mwanya, ingawa mwanya wenyewe haujaelezwa moja kwa moja.

2.3.2.2.4 Udondoshaji dhahiri

Udondoshaji huu unaweza kuwa wazi au usio wazi. Katika aina hii ya udondoshaji mpito wa wakati unadhihirika, ama uende usidhihirike moja kwa moja. Udondoshaji unaodhihirika unajitokeza katika wimbo wa *Tupatupa* ambapo inaelezwa wazi kuhusu siku kitendo cha kuvutia kwa jehanamu kilitendeka kwa kudhihirisha wakati moja kwa moja;

Mfano 32: *Tupatupa*

...Kwa kweli Jehanamu siku hiyo kulivutia sana ...
...Hayo ndiyo maneno ambayo alijinadi nayo siku hiyo shetani...
...Kwa kweli siku hiyo shetani alijieleza kwa ufasaha...
"...Hapana, jana kulikuwa na starehe, jana kulikuwa na wanawake wazuri..."

Kwa upande mwingine, huenda muda usidhihirike moja kwa moja. Kwa mfano, katika wimbo huu wa *Tupatupa*, muda wa Tupatupa kutoka Jehanamu na kwenda Mbinguni haujidhihirishi. Kwa mfano;

Mfano 33: *Tupatupa*

...Mzee Tupatupa
Muda umekwisha
Sasa twende Mbinguni
Alipofika Mbinguni akakuta malaika
Wao wanaimba
Tena wanasujudu.

2.3.2.3 Kipengele cha Onyesho

Kwa mujibu wa Wamitila (2002), onyesho ni njia ambayo huleta uigizaji katika matini yoyote ile. Dayolojia ndiyo njia bora ya kudhihirisha onyesho katika matini. Wahusika katika usimulizi huonyeshwa moja kwa moja mbele ya hadhira wakizungumza. Onyesho hudhihirisha usawa kati ya wakati-hadithi na wakati-matini, kwani kama inavyojitokeza katika matini, matukio yanajidhihirisha kiwakati kupitia dayolojia. Rimmon-Kenan (2002) anaongeza kusema kuwa dayolojia ndiyo njia mwafaka ya kudhihirisha onyesho.

Baadhi ya nyimbo za Bahati Bukuku zilizoteuliwa kwa utafiti huu zinadhihirisha kipengele cha onyesho. Kwa mfano, katika wimbo wa *Tupatupa,* kunajitokeza maneno ambayo Mzee Tupatupa aliyasema kila alipowaona wadada/wanawake ambao aliwapenda sana;

Mfano 34: *Tupatupa*

"Mtoto mzuri,malkia,malikia,mrembo kama
wewe unatembea chini?Mimi nikikuoa
nitakununulia ndege uifanye kama daladala.
Nitakuwa nakupeleka huko Kariako,wakati
mwingine Masaki,nitaifanya dunia iwe
kijiji kidogo kwako."

Maneno haya ya mhusika Tupatupa yanadhihirisha ukware aliokuwa nao kila alipowaona wanawake. Onyesho pia linajitokeza katika dayolojia kati ya Tupatupa na shetani kama ifuatayo;

Mfano 35: *Tupatupa*

Tupatupa: Kule duniani watu wanasema eti
wewe una mapembe.
Shetani: Mimi ni *beautiful* na ni *handsome*,
nikimkamata mke wa mtu ni lazima
aisahau ndoa yake, na nikimkamata mme
wa mtu ni lazima aisahau familia yake.

Dayolojia hii inabainisha maovu ya mhusika shetani. Vilevile, inabainisha kampeni za shetani anapotaka kumvutia binadamu, kama inavyodhihirika mwishoni mwa wimbo mwimbaji anapoanza kufafanua sababu za shetani kuwa mzuri sana mwanzoni ila kumgeuka Tupatupa baadaye na kuwa katili mbele yake. Vilevile, dhana ya onyesho imeweza kudhihirika katika wimbo wa *Dunia haina huruma*. Msimulizi anadhihirisha majibu aliyopokea kutoka kwa wahusika wengine kila alipowaomba msaada kwani mume wake alikuwa katika hali mbaya sana hospitalini. Kwa mfano;

Mfano 36: *Dunia haina huruma*

...Ninamwomba daktari
Daktari naomba nisaidie
Mume wangu akipona

Gharama zote tutalipa
Na kama la hajapona
Utachukuwa gari langu
“Kwa kweli mama ningekusaidia,
lakini hizo gari aina ya 4B, kwa
kawaida zinakula sana mafuta.”
...Mashemeji wamegoma kutoa msaada
Maneno wanayoniambia,
“Samahani shemeji,ningeweza kukusadia,
lakini ninaenda kutazama mpira ulaya.”
Ninawatafuta mawifi kwa mara nyingine
“Kwa kweli wifi si unajua, ningeweza kukusaidia
lakini wenzangu wote wacheza shengele watakuja
siku ya Jumamosi, kwa hivyo nimewaambia na siwezi
kughairi kwa kuwa wameshona sare.”

Wimbo wa *Waraka,* vilevile unadhihirisha dhana ya onyesho, kupitia malilio ya Esther kwa mfalme wake kuhusu mpango wa Hamani wa kuwaangamiza wayahudi wote. Kwa mfano;

Mfano 37: *Waraka*

...Esther kwa machozi akamwambia,” Eh! Bwana wangu,
ninaomba subira, mimi na Wayahudi wote, tumetangaziwa
kuuawa na huyu adui wangu mtesi, naye ni Haman
...Mfalme akasimama akamtazama malkia
Kwa ghadhabu akageuka akamtazama Hamani
Akasema,” Mtoeni nje Hamani! Nenda mvike sanda nyeusi akafie
huko.”

Onyesho aghalabu hudhihirisha matukio yenye mvuto kwa hadhira. Hudhihirisha maudhui, sifa za wahusika pamoja na mbinu tofauti za uandishi. Umuhimu wa wahusika vilevile huweza kubainika kwa kupitia onyesho.

2.3.2.4 Mtuo

Dhana hii hujitokeza katika hadithi wakati msimulizi anaingiza maelezo ya pembeni, ambayo huenda yana uhusiano au yanaweza kukosa uhusiano na hadithi, katika hadithi yake. Wamitila (2003) anafafanua mtuo kama dhana inayoeleza jinsi ya kudhihirika kwa wakati au kasi-hadithi. Mtuo hupatikana kutokana na maelezo au mawazo ya pembeni ya msimulizi. Mawazo mengine

kuhusu mtuo yanaendelezwa naye Genette (1980) kwamba mtuo hutokea pale ambapo msimulizi huacha kwa muda mtiririko wa hadithi na kutoa maelezo ambayo wakati mwingine hayana uhusiano na hadithi au hata hayahitajiki. Mfano wa mtuo unadhihirika katika wimbo wa *Tupatupa,* kama ifuatavyo;

Mfano 38: *Tupatupa*

Tupatupa siku moja alilewa
Aliona taa mbili zinakuja
Siku hiyo ilikuwa siku mbaya kwake *Tupatupa*
Aliona taa mbili zinakuja mbele

Maelezo “Siku hiyo ilikuwa siku mbaya kwake Tupatupa” yanajitokeza kama ya ziada tu ambayo hayako katika mtiririko wa hadithi, ila msimulizi anaambatanisha katika hadithi kudhihirisha janga ambalo lilimsubiri Tupatupa. Mfano mwingine unadhihirika katika wimbo wa *Dunia haina huruma*, wakati msimulizi anapofika katika wodi ya wagonjwa mahututi, alipokuwa amelazwa mume wake. Kwa mfano;

Mfano 39: *Dunia haina huruma*

Ninamkuta mpenzi wa roho yangu
Amepoteza fahamu, hawezi hata kunitazama
Hilo ndilo patano letu mume wangu
Na hapa ndipo jijini Mbeya mpenzi wangu
Haya mapanga ndiyo zawadi yangu mume wangu...

Katika dondoo hili, msimulizi anatua usimulizi wake kwa mume wake ambaye hawezi hata kumtazama, kisha msimulizi anaanza kujizungumzia kinafsi kuhusu hali ya mambo yanayomkumba. Hii inadhihirisha mtuo katika wimbo huu.

2.3.3 Mpangilio

Matukio katika simulizi hupangwa kiwakati. Genette (1980) anaeleza kuwa mpangilio ni uhusiano baina ya mfuatano wa matukio katika hadithi. Hufafanua jinsi matukio yanavyohusiana katika kutendeka. Mfuatano wa kiwakati, hata hivyo, unaweza kukiukwa kulingana na jinsi mtunzi wa

hadithi alivyopanga hadithi yake. Kwa mfano, kuna mfuatano wa moja kwa moja, ilhali kuna wakati ambapo matukio ya mwanzo yanajitokeza mwisho, ilhali ya mwisho yanarudi mwanzoni. Hali hizi huzua urejeshi na uelekezi mtawalia. Hali ya matukio kusimuliwa kiwakati hujulikana kama Anakroni. Utafiti huu ulichanganua matumizi ya aina mbili za anakroni, ambazo ni analepsia (mbinu rejeshi) na prolepsia (mbinu elekezi).

2.3.3.1 Analepsia

Hii ni mbinu ambapo masimulizi ya matukio yaliyotokea nyuma yanasimuliwa kabla ya yale yaliyotangulia kutendeka. Kwa mujibu wa Wamitila (2003), mbinu rejeshi hutumiwa na waandishi kueleza matukio yaliyotokea nyuma ya wakati wa hadithi. Naye Rimmon-Kenan (2002) anasema kuwa analepsia ni usimulizi wa tukio katika hadithi ambapo tukio la mbele linasimuliwa kabla ya yale yaliyotendeka kabla yake. Hutegemea anayesimulia kuhusu analepsia inarejelewa. Genette(1980:48) anaorodhesha aina za analepsia kama; analepsia ya nje, analepsia ya ndani, analepsia mseto, analepsia tawasifu na analepsia wasifu.

2.3.3.1.1 Analepsia ya nje

Kulingana na uchanganuzi wa Wamitila (2003), hii ni mbinu ya usimulizi inayohusisha matukio ambayo yako nje ya wakati wa mwanzo wa hadithi. Aidha, anavyodokeza Genette (1980), analepsia ya nje ni masimulizi ya matukio ya kabla ya kuanza kwa hadithi. Kwa mfano, katika utangulizi wa hadithi ya mhusika Tupatupa katika wimbo wa *Tupatupa*, msimulizi anafafanua kuhusu tabia za Mzee Tupatupa za kuwapenda sana wanawake. Hii inajitokeza kabla ya Tupatupa kugongwa na gari na kuaga dunia. Vilevile, maelezo haya yanasaidia katika kuelewa kwa nini Tupatupa alipendezwa sana na Jehanamu alipopatembelea na kukutana na wasichana warembo ambao hawakuwepo Mbinguni. Kwa hivyo, hata kabla ya kuanza rasmi kwa kisa kinachosimuliwa, sifa ya ukware wa Tupatupa unadhihirisha wazi kupitia analepsia ya nje kama ifuatavyo;

Mfano 40: *Tupatupa*

Alikuwepo baba jina lake Tupatupa
Alikuwa tajiri tena mwenye sura nzuri
Kila aliyemwona alijua mambo sawa
Mzee Tupatupa alipoona wadada
Kila aliyemwona alijua amepona
Mambo yake yalikuwa hivi
"Mtoto mzuri, malkia,malkia,malkia,mrembo
kama wewe unatembea chini?Mimi nikikuoa
nitakununulia ndege uifanye kama daladala.
Nitakuwa nakupeleka huko Kariako,wakati mwingine
Masaki,nitaifanya dunia iwe kijiji kidogo kwako."

2.3.3.1.2 Analepsia ya ndani

Analepsia ya ndani ni masimulizi ya matukio yanayotokea baada ya kuanza hadithi lakini hayasimuliwi wakati yalipotendeka. Husimuliwa baadaye katika hadithi. Maoni ya Wamitila (2003) yanafafanua analepsia ya ndani kama rejeshi ambayo huhusisha matukio yaliyopita lakini yasiyokuwa ya kabla ya wakati ianzapo hadithi. Hali hii inadhihirika katika wimbo wa *Dunia haina huruma*, ambapo, baada ya kutafuta msaada ili aweze kupata matibabu ya mume wake na kukosa, msimulizi aliamua kufanya mapenzi na daktari ili aweze kupata msaada. Mapenzi kati yao yalisababisha msimulizi kupata ujauzito. Hata hivyo, sehemu ya ujauzito wenyewe haijahadithiwa wala habari za ujauzito kudhihirishwa. Badala yake, hadhira inatambua baadaye kuwa tayari kuna mtoto aliyekuwa ni zao la mapenzi kati ya msimulizi na daktari, wakati msimuilizi alipoamua kumweleza mumewe ukweli kuhusu uzazi wa mtoto huyo. Kwa mfano;

Mfano 41: *Dunia haina huruma*

...Niliamua kumwangukia daktari...
..."Mume wangu,ile siku ulipocharazwa mapanga,
yule daktari aliyekuwa anakuuguza ndiye mwenye
mtoto huyu."

Ni wazi, kwa mujibu wa dondoo hili, kuwa haikubainika popote kuwa msimulizi amepata ujauzito, ila inajitokeza baadaye kuwa msimulizi ana mtoto.

2.3.3.1.3 Analepsia mseto

Kama jina linavyotambulisha, aina hii ya analepsia ni mseto wa analepsia ya nje na ya ndani. Hii ina maana kuwa inasimulia matukio yaliyotendeka kabla ya mwanzo wa hadithi na kisha kuvuka mwanzo wa hadithi hiyo. Kwa mujibu wa Genette (1980), analepsia mseto ni masimulizi ya matukio ya kabla ya mwanzo wa hadithi na ambayo huendelea hadi kuvuka mwanzo wa simulizi.

Katika wimbo wa *Maamuzi*, analepsia hii inabainika kwani mtunzi wa simulizi katika wimbo huu anaanza kwa kueleza kuhusu tatizo lake Tundo lilivyokuwa limemsumbua kwa muda mrefu. Hadhira inajua uhusiano kati ya Tundo na mawifi zake hata kabla mwanzo wa matukio usimulizi huu, ambao ulikuwa mbaya kwa sababu ya kutokuwa na uwezo wa kujifungua mwana. Vilevile inabainika kuwa kabla ya mwanzo wa usimulizi, Tundo aliwahi kutembea huku na kule kutafuta msaada. Kwa mfano;

Mfano 42: *Maamuzi*

Alikuwepo mama mmoja ngoja niseme
Jina lake aliitwa Tundo
Alisumbuliwa na ugumba miaka mingi
Ndoa yake ilikuwa matatani
Hata mawifi zake wote hawakumpenda tena
Tundo aliamua kwenda kwa waganga
Aliona bora aende kwa waganga Tundo...

Kwa kurejelea usimulizi huu, mwanzo wake mkamilifu ni uamuzi wake kwenda kwa waganga. Hata hivyo, msimulizi anaanzia matukio ya kabla ya hapa na kuoanisha matukio ya kitambo na ya wakati huo.

2.3.3.1.4 Analepsia wasifu

Analepsia wasifu hutoa taarifa kuhusu matukio yaliyopita kuhusu mhusika mwingine ambaye hayupo katika masimulizi hayo wakati yanaendelea, tukio jingine au hadithi nyingine ambayo haihusiani na mkondo wa hadithi inayosimuliwa wakati huo. Kwa mfano, katika wimbo wa *Dunia*

haina huruma, msimulizi alipoamua kumweleza mume wake ukweli kuhusu uzazi wa mwana wao, anamtaja daktari ambaye hakuwepo katika mfululizo wa matukio yalivyotanguliza kilele cha hadithi hiyo. Kwa hivyo, inabainika kuwa tukio jingine la daktari huyu linaathiri mtiririko wa usimulizi huo kuanzia pale. Inajitokeza ifuatavyo;

Mfano 43: *Dunia haina huruma*

"Mume wangu, ile siku ulipocharazwa mapanga,
yule daktari aliyekuwa anakuuguza ndiye mwenye
mtoto huyu."

2.3.3.1.5 Analepsia tawasifu

Hutoa taarifa kuhusu matukio yaliyopita, kuhusu mhusika anayesimuliwa. Aghalabu hutumia usimulizi wa nafsi ya kwanza kuambatana na neno "mimi" au kiambishi cha nafsi "ni" kwa kiwango kikubwa. Aina hii ya analepsia inadhihirika katika wimbo wa *Lazima Usamehe*. Msimulizi anasimulia kuhusu tukio la kumsaidia rafiki yake ambaye alimgeuka baadaye;

Mfano 44: *Lazima usamehe*

Nilikuwa na rafiki yangu mzuri
Aliyeugua ugonjwa wa ajabu
Kwa huruma zangu nikamhurumia
Nikatumia muda wangu mwingi
Nikazunguka huku na kule kutafuta madaktari
Nikatembea huku na kule kutafuta uzima wake
Lakini Mungu sio mwanadamu
Alinisikia
Kwa kuwa Mungu si mwanadamu,alimponya
Cha kushangaza alipopona,malipo yangu
Aligeuka adui yangu
Amekuwa msiba kwangu...

Matukio ya dondoo hili yalikwisha kutokea zamani kabla ya wakati hadithi inasimuliwa. Kupitia usimulizi huu, hadhira inabaini sababu za uchungu wa msimulizi kumhusu rafikiye.

2.3.3.2 Prolepsia

Huweza vilevile kuitwa mbinu elekezi. Prolepsia ni mbinu ya usimulizi ambapo msimulizi husimulia matukio yanayotukia baadaye lakini anayasimulia sasa katika hadithi. Mbinu hii huweza kuleta matukio ambayo huenda yakatokea baadaye hata kabla ya kusimulia matukio ya sasa. Kwa mujibu wa Wamitila (2003) prolepsia ni dhana inayotumiwa kueleza hali ambapo mwandishi anatupa picha ya matukio ya mbele katika hadithi. Mbinu hii hufanikisha taharuki kwani hadhira hutaka kujua sababu ya hali hiyo inayoonyeshwa. Kwa mujibu wa Toolan (1990), prolepsia ni mbinu ambayo kimsingi inachujua taharuki ya hadithi inayosimuliwa kwa kuwa inasimulia matukio kabla ya ulazima wake wa kiwakati. Prolepsia imeainishwa kama; prolepsia ya ndani, prolepsia ya nje, prolepsia mseto, prolepsia tawasifu na prolepsia wasifu.

2.3.3.2.1 Prolepsia ya ndani

Prolepsia ya ndani ni mbinu ya kusimulia matukio ambayo yatatendeka baadaye katika hadithi kabla hadithi yenyewe haijafika mwisho.Ni kwamba matukio yanayosimuliwa ni mojawapo ya matukio katika hadithi. Prolepsia ya ndani haijajitokeza katika wimbo wowote wa Bahati Bukuku.

2.3.3.2.2 Prolepsia ya nje

Prolepsia ya nje inasimulia tukio au matukio ambayo yatatokea katika kipindi cha baada ya hadithi bila kuhitilafiana na hadithi ya kwanza. Wamitila (2008) anafafanua kuwa msomaji ataisoma hadithi hiyo hadi mwisho bila kushuhudia kisa au tukio linalotangulizwa au kuelekezwa kwa kuwa liko nje ya mipaka hiyo ya hadithi. Aina hii ya prolepsia inadhihirika katika wimbo wa *Ahabu.* Baada ya miujiza yake, Elia anaangamiza manabii wote wa Baali. Kwa hasira, Jezebeli, akatuma ujumbe kwamba siku iliyofuata majira kama hayo, atakuwa amemuangamiza Elia. Hili ni tukio ambalo lingejitokeza baada ya hadithi, kwani katika usimulizi huu, hadhira haikumbani na kifo cha Elia. Mfano huu unajitokeza ifuatavyo;

Mfano 45: *Ahabu*

...Moto kutoka mbinguni ulishuka
Ulibeba sadaka ya Elia kila kitu
Wale miungu wa Baali wote
Walitetemeka, Elia aliwaua wote hawakuweza
Kumsongelea, Jezebeli akatuma ujumbe
Nenda kamwambie Elia, Kesho majira kama haya
Roho ya Elia itakuwa mikononi mwangu
Maneno ya Jezebeli yalimnyima usingizi.
Elia akakimbia...

Usimulizi huu, kama inavyojitokeza katika dondoo hili, unaisha Elia akitoroka baada ya kupata habari ya kupangiwa kifo chake. Inasalia kuwa taharuki kwa hadhira iwapo Jezebeli alimuua Elia au la.

2.3.3.2.3 Prolepsia mseto

Prolepsia mseto inaweza kusimulia tukio au matukio ambayo yatatokea kabla au hata baada ya simulizi ya kwanza. Unaweza kujitokeza kama prolepsia ya nje au ya ndani. Kwa mfano;

Mfano 46: *Abneli*

Mbona huyu amefia hapa? Kwa nini?
Mbona huyu amenyongwa? Nashangaa!
Nyumba za wageni zimejaa wizi... kwa nini?
Taarifa za habari hakuna mapya, nashangaa!

Kwa kurejelea mfano huu, haya yote yanayohadithiwa yanajitokeza kabla ya simulizi ya kwanza. Usimulizi wa mhusika Abneli unafuata sehemu hii ya usimulizi. Inabainika kuwa, kabla ya kuanza rasmi kwa usimulizi unaolengwa, kuna mhusika ambaye ameaga dunia bila sababu, kuna yule ambaye amenyongwa, nyumba za wageni zimejaa wizi pamoja na taarifa za habari kukosa mapya. Hali hizi za kutamausha zinajenga msingi wa usimulizi unaotamausha. Hivyo basi, prolepsia mseto inadhihirika.

2.3.3.2.4 Prolepsia tawasifu

Hii ni aina ya prolepsia ambayo hutoa taarifa juu ya matukio ambayo yangetokea ama juu ya mhusika, tukio au hadithi inayosimuliwa katika wakati wa sasa wa hadithi. Aina hii ya prolepsia Genette (1980) ameiita *Homodiegetic prolepsis.* Prolepsia tawasifu imedhihirika katika wimbo wa *Dunia haina huruma*, msimulizi alipokuwa akitafuta jinsi mume wake atakavyotibiwa, alijariba kumwahidi daktari ili aweze kumsaidia mume wake. Kwa mfano;

Mfano 47: *Dunia haina huruma*

...Daktari naomba nisaidie
Mume wangu akipona
Gharama zote tutalipa
Na kama hajapona
Utachukua gari langu...

Dondoo hili ni prolepsia tawasifu kwa sababu bado mume wa msimulizi hajatibiwa wala kupona, na vilevile bado daktari hajachukua gari la msimulizi. Lakini msimulizi anamweleza daktari kuwa ikiwa mume wake atapona, basi daktari angeweza kuchukuwa gari lake. Vilevile hatujui iwapo daktari angelikubali gari hilo au la.

2.3.3.2.5 Prolepsia wasifu

Prolepsia wasifu hutoa taarifa juu ya matukio yanayokuja ama juu ya mhusika mwingine, tukio jingine au hadithi nyingine mbali na mhusika, tukio au hadithi inayosimuliwa katika wakati wa sasa wa hadithi. Aina hii ya prolepsia imejitokeza katika wimbo wa *Ahabu*, Elia alipotaka kudhihirisha Mungu wa kweli kati ya Mungu wake na miungu ya Baali. Kwa mfano;

Mfano 48: *Ahabu*

...Kama Baali ni Mungu basi leo tunamwabudu
Na kama Mungu yupo basi leo tutamjua...

Hapa kinachosimuliwa kinahusu ni yupi Mungu wa kweli na tendo la kumwabudu au kumjua halijatokea katika wakati wa usimulizi.

2.4 Hitimisho

Sura hii imejadili jinsi usimulizi ulivyoweza kujitokeza katika nyimbo teule za Bahati Bukuku kwa kurejelea vipengele viwili muhimu, ploti na wakati. Imebainika kwamba vipengele hivi ni muhimu katika kufanikisha usimulizi. Kipengele cha ploti kimejadiliwa kwa kujikita katika vijipengele vinavyosaidia kuijenga, navyo ni, utangulizi na tamati maalum, nafasi ya mhusika mkuu katika usimulizi pamoja na kilele cha usimulizi.

Mbali na ploti, wakati ni kipengele muhimu kilichojadiliwa katika sura hii ya utafiti. Umuhimu wake umedhihirika wazi kwani matukio yote hutendeka kiwakati. Kuna vipengele vya wakati vilivyotumika ilhali vingine havijaweza kutumika.Katika kuhakiki wakati, vipengele vilivyojadiliwa ni pamoja na idadi marudio, muda na mpangilio.

Vijipengele muhimu vya idadi marudio vilivyojadiliwa ni kama usimulizi mosi, usimulizi rudufu na usimulizi banifu. Aidha, vijipengele vya muda viliweza kujadiliwa na ni kama muktasari, mtuo, onyesho na udondoshi. Kipengele cha mwisho chini ya wakati kilichojadiliwa katika sura hii, mpangilio, kiliibua vijipengele kama; Analepsia na Prolepsia. Aina za Analepsia na Prolepsia vilevile zimeweza kujadiliwa zikiwemo; wasifu, tawasifu, za ndani, za nje na mseto.Vipengele hivi vyote vimeweza kusaidia katika kuelewa dhana ya usimulizi inavyojitokeza katika nyimbo za Bahati Bukuku na katika kazi za kifasihi kwa ujumla. Sura inayofuata inahusu uchanganuzi wa maudhui na uwasilishaji wake katika nyimbo za Bahati Bukuku.

SURA YA TATU

MAUDHUI KATIKA NYIMBO TEULE ZA BAHATI BUKUKU

3.0 Utangulizi

Sura hii inalenga kuhakiki jinsi mbinu ya usimulizi inavyosaidia katika kuwasilisha maudhui katika nyimbo teule za mwimbaji Bahati Bukuku. Utafiti umeanza kwa kutoa ufafanuzi wa dhana ya maudhui kwa kurejelea maoni ya wataalamu mbalimbali ambao wamechangia kuhusu dhana hii muhimu katika usimulizi. Vilevile, sura hii imehakiki baadhi ya maudhui yanayopatikana katika nyimbo hizi teule, kwa mfano, Imani ya dini, Unafiki, Msamaha, Nafasi ya marafiki katika maisha ya mja, Ushirikina, Anasa na Nafasi ya mwanamke katika jamii. Mifano maridhawa itatolewa ili kudhihirisha jinsi maudhui haya yalivyoweza kuwasilishwa katika nyimbo hizi teule.

3.1 Maudhui na uwasilishaji wake katika nyimbo za Bahati Bukuku

Maudhui ni ujumbe wa jumla unaojitokeza katika kazi ya fasihi. Katika kuwasilisha dhamira ya kazi yoyote ya fasihi, maudhui hushirikishwa moja kwa moja. Kwa mujibu wa mwana-naratolojia Manfred (2005), dhamira, ambao ni mhimili muhimu wa nadharia ya naratolojia, huchangia pakubwa katika kuibua maudhui katika simulizi. Madai ya Manfred (keshatajwa) yanafanana na na yale ya Wamitila (2003) ambaye anaainisha umuhimu wa dhamira katika simulizi kama kipengele kinachochangia kuwepo kwa maudhui. Anafafanua kuwa maudhui ni jumla ya yaliyomo katika hadithi hiyo, yanayoibuka katika kuendeleza dhamira. Kwa hivyo, mwanafasihi anapotaka kuafikia lengo lake kwa hadhira, ni lazima maudhui yaelezwe kwa utendeti. Njogu na Chimera (1999:21) wanasema;

> Maudhui ni mawazo ya jumla, mawazo mapana yanayowasilishwa katika wakati maalum kadri kazi inavyoendelea.

Njogu na Chimerah (1999) wanaendeleza kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya maudhui na mtindo. Mtindo ambao hutumiwa katika kubuni na kuwasilisha fasihi ndio humwezesha msanii kuwasilisha maudhui yake. Ubunifu wa mtunzi na uwezo wa kuteua mbinu bora ndiyo vifaa vinavyomwezesha kuwasilisha ujumbe wake. Haya hutokana na uwezo wake wa kudhibiti lugha na idadi ya maneno aliyonayo katika ubongo wake. Uwezo huu ndio unaomwezesha kuteua na kupanga maneno kwa njia ya ufasaha na hivyo kujitofautisha na wengine ambao huenda pia wamejadili mada hiyo.

Msanii huchagua aina za mada anazotaka kujadili katika kazi yake na kuchagua maneno ya kujadili mada hizo. Mada zinazoteuliwa na msanii fulani huwa zinajadiliwa kutokana na msimamo wake katika maisha. Kwa hivyo, mara nyingi msanii hujadili maudhui kulingana na imani yake na mkabala wake kuhusu mada inayohusika.

Kwa mujibu wa Stanzel (1984), msimulizi wa nafsi ya tatu ana uwezo wa kutambulisha maudhui katika simulizi. Hii ni kwa sababu anaposimulia, msimulizi yuko nje ya usimulizi na ana uwezo wa kuangazia maudhui anayoyaona moja kwa moja. Msimulizi huyu wa nafsi ya tatu huwakilisha fikra na mihemko ya wahusika ambayo huwasilisha maudhui ya usimulizi.

Griffith (2010) anaeleza kuwa usimulizi hujumuisha vipengele kadhaa ambavyo hufanikisha uwasilishaji wa maudhui. Vipengele hivi ni kama: uhusika, ploti na mandhari. Vipengele hivi humwasilishia msomaji au msikilizaji wa usimulizi kiini cha usimulizi huo. Maudhui huwasilishwa kupitia kile wanachosema wahusika, kile wanachokifanya, wanachokifikiria pamoja na kupitia matendo yao katika simulizi. Griffith (keshatajwa) anaendeleza kuwa maudhui pia hutambuliwa kupitia mfuatano wa matukio pamoja na mandhari inayotumiwa na mtunzi katika kuwasilisha simulizi.

3.2. Aina za maudhui katika nyimbo teule za Bahati Bukuku

Bahati Bukuku aliimba nyimbo zilizoshughulikia aina mbalimbali za maudhui kama ifuatayo;

3.2.1 Imani ya Dini

Imani ni mambo anayoyakubali mtu kuwa ni ya kweli na anayopaswa kuyaheshimu, hasa katika dini. Bahati Bukuku alishughulikia maudhui ya dini kwa kiwango kikubwa. Katika simulizi za nyimbo zake, kuna nguvu za kiungu ambazo zimejitokeza kushinda nguvu zingine zote, zikiwemo za miungu au zile zinazotawaliwa na binadamu.

Katika wimbo wa *Maamuzi*, Bukuku anahadithia katika wimbo wake kuhusu mwanamke mmoja kwa jina Tundo. Mwanamke huyu alikaa muda mrefu bila ya kufanikiwa kupata mwana. Kwa sababu ya ukosefu wa mwana, alienda kwa mganga mmoja maarufu nchini Kongo ili aweze kufanikiwa kupata mwana. Hapa, tunaona jinsi maoni ya Griffith (2010) kuhusu mandhari kama chanzo cha maudhui yanavyodhihirika. Mandhari ya uganga yanashikamana na imani ya mhusika Tundo anayeenda kwa mganga ili kupata msaada anaotaka.

Matokeo ya kumtembelea mganga huyo yakawa ni kupata mtoto, ila, aliyempata hakuwa mtoto halisi bali Chatu. Siku moja marafiki wa Tundo wanapomtembelea na kugundua kuwa Tundo alikuwa akiugua sana mwilini mwake, wanamwomba aende akaombewe na watumishi wa Mungu kanisani. Kwa mujibu wa imani ya dini ya marafiki wa Tundo, ambao ni wakristo, mandhari ya kanisani ndipo Tundo angepata msaada wa kuombewa ili shida yake isuluhishwe. Kwa kutathmini haya, inajitokeza wazi jinsi mandhari ni muhimu sana katika uwasilishaji wa maudhui katika usimulizi.

Baada ya kuombwa aende kanisani akaombewe, Tundo anakubali. Anapofika kanisani, mtumishi anamweleza Tundo asonge mbele ili aweze kumwombea. Kutanabahi, mtoto Sinona anabadilika na kuwa Chatu baada ya maombi. Wengi wanashangazwa kwa miujiza hiyo. Tazama mfano huu;

Mfano 1: *Maamuzi*

Alikutana na mganga mmoja nchini Congo
Akampa dawa za kutosha Tundo
Tundo alizaa mtoto wa kiume
Jina lake alimwita Sinona.
Maajabu aliyokuwa nayo mtoto yule
Alikuwa amezaliwa na meno
Alizaliwa na meno kama mtu mzima
Ghafla alimngata mwili wake Tundo
Mwili wake ukapoa wote upande mmoja…

…Akamwambia Tundo njoo mbele
Tundo akijua Mungu amesikia
Mchungaji akauliza,
Umebeba nini mgongoni mwako?
…Mshushe mtoto wako hapa kwenye madhabaho
Mtoto aligeuka Chatu mara ile
Eti Sinona sio mtoto, kumbe Sinona ni joka kubwa

Kulingana na uwasilishaji wa usimulizi huu katika wimbo wa *Maamuzi* , ilikuwa tu baada ya mchungaji kuomba ndipo ikabainika wazi kuwa Sinona si mtoto bali alikuwa ni joka kubwa ambalo ndilo lilisababishia Tundo madhara mengi, yakiwemo kung'atwa mwili, kupooza upande mmoja wa mwili pamoja na kubadili ngozi yake kuwa magamba kama ya nyoka. Vilevile, kwa kutaja jina la Mungu, inaonyesha wazi kuwa yanayowasilishwa katika usimulizi huu yalikuwa ya kidini. Maudhui ya imani ya dini pia yanaonyesha masaibu ya Tundo yanatokana na kuasi mafunzo ya dini ya kutotembelea waganga. Kipengele cha mandhari kimejitokeza kuwa muhimu sana katika uchanganuzi wa maudhui ya dini katika wimbo wa *Maamuzi*.

Maudhui ya dini vilevile yamejitokeza katika wimbo wa *Ahabu* unaopatikana katika *Maandiko Matakatifu* (1952) katika kitabu cha Wafalme wa Kwanza 17:1-45. Wimbo huu unasimulia nyakati za mfalme Ahabu na jinsi ndoa yake na mke Jezebeli ilivyofanya Israeli kumtelekeza Mungu wao na kuanza kuiabudu miungu ya Baali na Asherah. Elia, nabii wa kweli wa Mungu, akataka kuwaonyesha bayana ni nani Mungu wa kweli, hivyo akawaeleza manabii wa Baali watengeneze madhabaho na waombe miungu yao ilete moto. Hata hivyo, moto haukuwaka. Wakati Elia alipomwomba Mungu wake moto mkubwa uliwaka na kuteketeza dhabihu. Hivi ilionyesha kuwa Mungu wa Elia ndiye mwenye nguvu kushinda miungu ya Baali na Asharah.

Mfano 2: *Ahabu*

…Waitwe manabii wote mia na hamsini
kama Baali ni mungu basi leo tutamwabudu
Na kama Mungu yupo basi leo tutamjua
Wakajikusanya mabaalia wote wakaanda sadaka yao ya kuteketezwa
Lakini mungu wa Baali hakushuka, hakuamuka
Elia akasimama
Akaandaa sadaka yake
Akawaambia leteni maji
Sadaka yangu imwagiliwe
Akajipiga kifua chake
Moto kutoka mbinguni ulishuka
Ulibeba sadaka ya Elia kila kitu
Wale miungu wa Baali wote walitetemeka

Katika sehemu hii, inabainika kuwa Mungu wa Elia ndiye mwenye nguvu ikilinganishwa na miungu ya Baali. Hii ni kwa sababu Elia alimwita Mungu aliyeteremsha moto ingawa sadaka yake ilikuwa imeloa ilhali miungu ya Baali haikuteketeza sadaka zozote za manabii wa Baali. Kuwepo na miungu ya Baali na Mungu wa kweli kunadhibitisha dini tofauti ambazo zilikuwa katika mgogoro wa kubainisha aliyekuwa Mungu wa kweli. Vilevile, nguvu za kidini zinabainika wakati

moto mkubwa unashuka kutoka mbinguni na kuteketeza sadaka ya Elia, jambo ambalo halikutendeka wakati manabii wa Baali walipokuwa wakiomba miungu yao.

Kwa kuzingatia mfano huu katika wimbo wa *Ahabu*, wahusika katika usimulizi wanachangia kuwepo kwa maudhui ya dini. Matukio makuu katika usimulizi yamezingira nafasi ya wahusika hawa katika kumgundua Mungu wa kweli kati ya Mungu wa Elia na miungu ya Baali na Asherah. Mhusika Elia anahusika katika kuwaita manabii wa Baali ili waombe miungu yao isababishe moto kuchoma dhabihu yao. Hata hivyo, manabii hawa wanashindwa kuteremsha moto kutoka kwa miungu yao kwani miungu yao si ya kweli. Nabii Elia anapoandaa sadaka yake na kumwomba Mungu wake, moto mkubwa unashuka kama inavyoelezewa katika *mfano 2*. Hivyo basi, maudhui ya Imani ya dini inajidhihirisha kutokana na fikra pamoja na matendo ya Nabii Elia.

Katika usimulizi mfupi wa wimbo wa *Barthimayo,* nguvu za kiungu vile vile zinaonekana kupitia uponyaji wa kipofu Barthimayo. Nguvu hizi za kiungu zilitokana na mhusika Yesu aliyemgusa Barthimayo macho na akaweza kuona. Kipofu huyu aliteseka kwa miaka mingi katika hali yake. Barthimayo aliwategemea wapita njia ili waweze kumhurumia na kumpa misaada kwani asingeweza kufanya lolote la kumpa ujira kwa sababu ya upofu wake. Hata hivyo, siku moja alipokuwa akipita Yesu, aliweza kumponya na Barthimayo akaweza kuona tena. Kwa hivyo, uhusika una nafasi kubwa katika kuibua maudhui ya Imani ya dini katika wimbo wa *Barthimayo*

Mfano 3: *Barthimayo*

Yesu alipopita
Ndipo kamuhurumia
Historia ya maisha yake
Yote ilibadilika.

Uponyaji huu unaotekelezwa kwa nguvu za kiungu unabainisha kuwa Yesu aliweza kufanya maajabu yasiyoweza kutendwa katika uhasilia.

Nguvu zinazoandamana na Imani ya dini vilevile zinajitokeza katika wimbo *Unatisha* unaopatikana katika *Maandiko Matakatifu* (1952) katika kitabu cha Kutoka 14:23-31. Wimbo huu unasheheni simulizi ya safari ya Waisraeli kutoka Misri kuelekea katika nchi ya ahadi, Kaanani. Waisraeli walipokuwa katika safari yao ya kuelekea katika nchi ya Canaan, huku wakifuatwa na Wamisri, wanafika katika Bahari ya Shamu ambapo hawana uwezo wa kuvuka hadi ng'ambo ya pili. Nguvu za Mungu wa Israeli zilionekana wakati Mungu alimwelekeza Musa anyoshe fimbo yake kuielekeza katika bahari ya Shamu ambayo ilitawanyika kuwili na Waisraeli wakaweza kupita.

Mfano 4: *Unatisha*

Jeshi la Farau linakuja
Madui wanasongea
Ukamuuliza Musa una nini?
Musa akasema nina fimbo

Fimbo hiyo ndiyo aliyoelekezea Bahari ya Shamu na ghafla maji yalitawanyika, na Waisraeli wakaweza kuvuka, hiyo kuokolewa kutoka katika mikono ya jeshi la Farau.

Katika Imani ya dini ya Kikristo, Inaaminikana kuwa hatima ya maisha ni mbinguni au kuzimu. Haya yanajitokeza katika wimbo wa *Tupatupa* ambao unasimulia kumhusu mhusika Tupatupa ambaye alitembelea Mbinguni na Jehanamu ili kufanya uteuzi wa ni wapi atakapopendelea. Tamaduni za dini nyingi, kwa mfano Kikristo na Kiislamu, hufunza kuhusu mema na mabaya, na hatima ya mema na mabaya, ambayo ni mbinguni na kuzimu mtawalia. Maelezo ya mbingu na kuzimu yanatofautiana kutoka dini moja hadi nyingine. Mzee Tupatupa anaelekea jehenamu na kuwapata wanawake wazuri, vinywaji vingi na maisha yanayopendeza. Anapoenda mbinguni, anatanabahi kugunduwa kuwa shughuli zote ni za kusifu na kuabudu Mungu. Ndipo anaamua

kurudi jehanamu na ni kule ndiko anatambua ukweli kuwa alihadaiwa kuhusu uzuri wa Jehanamu kwani kulikuwa na moto mkubwa pamoja na mateso mengi.

Mfano 5: *Tupatupa*

Bwana huyo akaingia jehanamu
Alichokiona jehanamu kulikuwa si cha kawaida
Akaona jehanamu kuna wanawake wazuri
Akaona ngoma nyingi zinapigwa
Akakuta kila aina ya kinywaji
Kwa kweli siku hiyo jehanamu kulivutia sana
Malaika akamwambia
Mzee Tupatupa
Muda umekwisha
Sasa twende mbiguni
Alipofika kule akapata malaika
Wao wanaimba
Tena wanasujudi

Mbinguni na Jehanamu huwa imani ya baadhi ya dini kuhusu hatima ya maisha ya waja. Wale ambao hutenda mema kwa mujibu wa dini zao huelekea mbinguni kusiko na mateso. Wale ambao wanatenda mabaya, huelekea jehanamu, kunakoaminika kuwa na vilio na mateso. Haya ni kwa mujibu wa wimbo wa *Tupatupa.* Katika wimbo wa *Tupatupa* mwimbaji anamithilisha maovu na kampeni za shetani ilhali mema ni kampeni za Mungu.

Mandhari katika usimulizi wa *Tupatupa* ina nafasi kubwa sana katika kuwasilisha maudhui ya Imani ya dini. Mandhari ya Mbinguni na yale ya Jehanamu yanaambatana na imani za dini kuwa wanaotenda mema huelekea Mbinguni ilhali wanaotenda mabaya huelekea Jehanamu baada ya kuaga dunia. Mhusika Tupatupa anatumiwa katika usimulizi huu kubaini mandhari zote mbili na kinachotarajiwa kwa wenye kutenda mema na yale mabaya.

3.2.2 Unafiki

Unafiki ni hali ya kujifanya kuwa ni rafiki, na hali ni adui. Unafiki ni mojawapo kati ya maudhui ambayo yameweza kushughulikiwa katika simulizi zinazopatikana katika nyimbo za Bahati Bukuku. Katika wimbo wa *Dunia haina huruma* unafiki unajitokeza kwa njia kadhaa zikiwemo unafiki wa mumewe msimulizi, unafiki wa ndugu na jamaa na unafiki wa mawifi zake msimulizi. Wahusika katika wimbo huu ndio wanaochangia katika kuwepo kwa maudhui ya unafiki. Matendo yao pamoja na fikra zao kumrejelea msimulizi ndiyo yanayodhihirisha uwepo wa maudhui ya unafiki. Kwa mfano, msimulizi anapowaomba msaada ili mume wake atibiwe, wanampa visababu vya kibinafsi kuonyesha wazi kuwa huwenda wasimpe msaada wowote. Hata hivyo, wao ndio wanaojitokeza kumhukumu wa kwanza baada ya kuamua kuhusiana na Daktari kimapenzi ili mumewe atibiwe.

3.2.2.1 Unafiki wa mumewe msimulizi.

Inabainika wazi kuwa kando na msimulizi, mume wa msimulizi vilevile alikuwa na kimada ambaye hakujulikana kwa msimulizi. Kimada huyu ndiye aliyepiga simu kwa kiburi kingi kumjuza msimulizi kuhusu kifo cha mumewe, pamoja na alipokuwa amelazwa. Hii ndiyo sababu moyo wa msimulizi unararuka anaposikia ni sauti ya mwanamke ambayo inazungumza ilhali ni namba ya mume wake iliyohusika katika kupiga simu;

Mfano 6: *Dunia haina huruma*

Ni asubuhi na mapema
Simu ya mkononi inaita
Naitazama kuwa makini
Ni namba ya mume wangu
Sauti ya mwanamke inasikika
Inayorarua moyo wangu
Moyo wangu unafura hasira
Kwa taarifa ninazopata

‘Hello, nenda mwimbini kachukue mzoga wako’
Namuuliza ni nani mwenzangu
Ananijibu kwa kejeli
“Mimi ni mke mwenzio kama hutaki potezea”

Hali hii inaonyesha wazi kuwa mumewe msimulizi hakuwa mwaminifu. Unafiki wa mumewe msimulizi unaendelea katika kikao, baada ya kumwita msimulizi aende kujitetea kwa kosa lililomkabili la kumpata mtoto nje ya ndoa. Hii ilikuwa baada ya msimulizi kuamua kufanya mapenzi na daktari ili mume wake aweze kutibiwa hospitalini, baada ya kujaribu kutafuta msaada kutoka kwa ndugu, jamaa na marafiki, bila mafanikio yoyote. Usherati huo na daktari ndio uliosababisha msimulizi kupata mimba isiyo ya mumewe.

Mfano 7: *Dunia haina huruma*

Nikageuka pembeni mwangu nikamwona
Mume wangu, ananitazama kwa hasira
Asiweza kunihurumia

Tabia hii ya mumewe msimulizi ni ya kusikitisha kwani usherati aliofanya mke wake pamoja na daktari ulikuwa ili kuokoa maisha yake ambayo ndugu, marafiki na jamaa zake walikuwa wamepuuzilia mbali.

3.2.2.2 Unafiki wa kimada wa mumewe msimulizi

Baada ya msimulizi kupigiwa simu asubuhi na mapema, sauti ya mwanamke inamweleza msimulizi aende mochari akachukuwe maiti ya mume wake. Baadaye anajidai kuwa mke mwenza. Kwa mfano;

Mfano 8: *Dunia haina huruma*

“Hello nenda ukachukuwe mzoga wako”
“Mimi ni mke mwenziyo kama hutaki potezeya”

Iwapo kwa kweli mwanamke aliyepiga simu alikuwa mke mwenza wa msimulizi, yeye pia angehusika katika usalama wa mume wa msimulizi. Hata hivyo hakuweza kuhusika, na akamwambia msimulizi kuwa aelekee akachukue mzoga wake, hivyo basi kuonyesha kutojali kwake wala huzuni ya aina yoyote.

3.2.2.3 Unafiki wa ndugu na jamaa

Katika wimbo huu, ndugu na jamaa wa mumewe msimulizi hawakutaka kuhusika katika matibabu ya mumewe msimulizi. Wakati ambapo msimulizi aliwapigia simu ili atafute msaada kwao ili mumewe aweze kupokea matibabu, walikwepa kumsaidia kwa kutoa visababu. Hata hivyo, inapofika wakati wa kuhukumu msimulizi, wao ndio wanaojitokeza kwenye kikao kumlaumu msimulizi kwa kufanya mapenzi na daktari na kumzaa mtoto asiye wa mumewe, bila kubaini kuwa msimulizi aliyafanya hayo ili mumewe aweze kutibiwa. Kinaya ni kwamba, iwapo msimulizi asingefanya mapenzi na daktari, huenda kikao hiki hakingekuwepo kwa sababu huenda mumewe msimulizi angeaga dunia. Tazama mfano ufuatao;

Mfano 9: *Dunia haina huruma*

Nawatafuta ndugu na jamaa
Waliokuwa kwenye simu yangu
Ili niwaambie tarifa hizi
Zinazoraruwa moyo wangu.
Ninawapigia ndugu wa mume wangu
Yaliyosibu mume wangu
Wote wananisusia

Nawatafuta rafiki wa mume wangu
Na kwanza ninapofika hapo
Wanaanza kunipa masharti
Yanayorarua moyo wangu
“Samahani shemeji, ningeweza kukusaidia lakini naeda kuangalia mpira Ulaya”

Inajitokeza waziwazi jinsi ndugu zake mwathiriwa wanavyopuuza mwathiriwa kwa kususia simu ya msimulizi anapotaka kuwaomba usaidizi, ikilinganishwa na jinsi wanavyotaka kumhukumu msimulizi wakati wa kikao.

3.2.2.4 Unafiki wa mawifi wa msimulizi

Mawifi wa msimulizi vilevile wanadhihirisha unafiki wanapokataa kumsaidia mwathiriwa, kwa kupendelea sherehe ya kitamaduni ikilinganishwa na usalama wa mumewe msimulizi.

Mfano 10: ***Dunia haina huruma***

> Nawatafuta mawifi kwa mara nyingine
>
> "Kwa kweli wifi si unajua tungeweza kukusaidia lakini wenzangu wote wacheza shengele watakuja siku ya Jumamosi. Kwa hivyo, nimewaambia na siwezi kughairi kwa sababu wameshona sare.''

Ingawa mawifi wanakataa kumsaidia msimulizi alipowahitaji, wanajitokeza kuwa mstari wa mbele kumhukumu msimulizi katika kikao. Wanatoa madai kuwa msimulizi alijihusisha na mapenzi na daktari, pasipo kujua kuwa alifanya hivyo ili kumwokoa mumewe.

Mfano 11: ***Dunia haina huruma***

> Nilipofika kijijini niliwakuta mawifi zangu
> Kila niliyemsalimia hakuweza kunijibu
> Kila aliyenitazama, alinitazama kwa dharau
> "Kama unataka kukaa na mtoto wetu, mtoto wako ni lazima auwawe maana sisi hatumtambui mtoto haramu katika familia yetu."

Tendo hili la kumbadilikia msimulizi hata baada ya kujaribu kuwaomba msaada ili mumewe atibiwe linadhihirisha unafiki katika upande wa mawifi. Msimulizi alipowaomba mawifi hawa msaada ili amtibu mumewe, wote walimpa vijisababu vya kutomsaidia. Hivyo basi, si bora kwao

kumhukumu msimulizi kwa kuwa walikuwa katika nafasi nzuri sana ya kumsaidia hata kabla msimulizi kuamua kufanya mapenzi na daktari ili mumewe apate matibabu.

Mbali na wimbo wa *Dunia haina huruma*, unafiki vilevile unajitokeza katika wimbo wa *Tupatupa*. Usimulizi katika wimbo huu unamdhihirisha shetani kama mnafiki mkubwa. Mzee Tupatupa alipokwenda Jehamanu kwa mara ya kwanza, anapata mazingira mazuri, wanawake wazuri, vinywaji vizuri pamoja na tabasamu kutoka kwa Shetani. Hata hivyo alipodai kurudi tena Jehanamu baada ya kutopendezwa na mandhari ya Mbinguni, anapata mazingira tofauti yanayomwangamiza. Tazama mfano huu;

Mfano 12: *Tupatupa*

Alipofika jahanamu mzee Tupatupa
alichokiona jahanamu kilikuwa si cha kawaida
akaona Jehanamu kuna wanawake wazuri
akaona ngoma nyingi zinapigwa
akakuta kila aina ya vinywaji…
Akatokea Shetani akiwa na tabasamu nzuri…
Shetani akacheka akasema
"Mimi ni *beautiful* na *handsome*"…

…Akatokea sasa Shetani
Akiwa na mapembe halisi
Kichwa chake kinadondosha damu za wanadamu
Akasema "hapana"
Sauti ikasikika kutoka kwenye moto
"Sikiliza mzee Tupatupa mimi ndiye Bwana Shetani
Nilikukopesha deni hujalipa, ata kama utachelewa kudaiwa.

Unafiki wa Shetani unajidhihirisha katika safari ya pili ya Tupatupa kwenda Jehanamu, baada ya kutembelea mbinguni na kukosa kufurahishwa na mandhari ya huko. Shetani anamgeuka Tupatupa na kuwa tofauti na jinsi alivyokuwa mara ya kwanza Tupatupa alipotembelea Jehanamu.

3.2.3 Msamaha

Msamaha ni tendo la kuwia mtu radhi kwa makosa aliyoyafanya. Ni hali ya kumaliza mgogoro na mtu mwengine baada ya kukosa maelewano. Maudhui ya msamaha imedhihirika katika simulizi ndani ya nyimbo za msanii Bahati Bukuku. Katika wimbo wa *Dunia haina huruma*, baada ya mume wa msimulizi kumshutumu kwa lawama za kukosa uaminifu katika ndoa, anaamua kumsamehe na vilevile kuomba msamaha kwa kumyumbisha mke wake (msimulizi) hadi kiwango cha kukumbana ana kwa ana na kikao kilichoamrisha kuuwawa kwa mwanawe. Tazama mfano huu;

Mfano 13: *Dunia haina huruma*

Mume wangu akasimama na kuanza
kulia kwa uchungu
"Kuanzia leo hii, unisamehe mke wangu
Kuanzia leo hii, ninatubu mke wangu
Kuanzia leo hii, unisamehe mke wangu"

Kwa kurejelea mfano huu wa *Dunia haina huruma*, mhusika ambaye ni mume wa msimulizi ndiye sababu ya kuwepo kwa maudhui ya msamaha. Hii ni kwa sababu ni yeye ndiye anayeomba msamaha mbele ya kikao ili msimulizi amwie radhi. Uhusika umepewa nafasi nzuri katika kuwasilisha maudhui.

Wimbo wa *Lazima usamehe* una msingi wake katika maudhui ya msamaha. Msimulizi anahadithia kuhusu rafikiye aliyekuwa mgonjwa wa ajabu. Baada ya msimulizi kushughulika kila wakati kuhakikisha kuwa amepona, rafikiye alimgeuka na kuwa adui yake. Msimulizi anaapa kutomsamehe ila baadaye anabaini kuwa kusamehe rafikiye ndio ushindi pekee anaoweza kupata. Tazama mfano huu;

Mfano 14: *Lazima usamehe*

Nilikuwa na rafiki yangu mzuri
Aliyeuguwa ugonjwa wa ajabu
…Nikazunguka huku na kule kutafuta madaktari
Lakini Mungu si mwanadamu
Alinihurumia
Akaachilia uzima moyoni mwake akawa mzima
…Cha kushangaza alipopona, malipo yangu
Aligeuka adui yangu
Amekuwa msiba kwangu
Nasema siwezi
Siwezi kumsamehe huyu
Lazima usamehe ili Mungu akuinue
Lazima usamehe ili Mungu aseme nawe

Msimulizi anaona suluhu ya kinyongo alichokuwa nacho ni kumsamehe rafikiye. Anasisitiza kuwa ili Mungu akutane nawe ni lazima uwe na moyo wa msamaha. Tazama mfano huu;

Mfano 15: *Lazima usamehe*

Ni kweli umeumizwa wewe
Ni kweli umedharauliwa wewe
Ni kweli umekata tamaa wewe
Unasema huwezi huwezi
Huwezi, huwezi (kusamehe)
Lakini huo ndio ushindi wako
Anayeleta heshima ya jina lako
Huyo ndio kazi ya kupanda wewe
Ili Mungu akuinue ni lazima ukutane naye
Ni lazima ili Mungu akuinue

Vilevile katika usimulizi huu, maudhui yamebainika kutokana na wahusika walioshiriki, ambao ni msimulizi pamoja na rafikiye.

Aidha, wimbo wa *Abneli* unatoa maelezo yanayochangia maudhui ya msamaha. Wimbo huu unasimulia kuhusu kisa cha Abneli, katika *Maandiko Matakatifu* (1952), kitabu cha 2 Samweli 3:22-39, ambaye aliuwawa na Yoabu kama kisasi cha kifo ambacho Abneli alimsababishia Asaheli, nduguye Yoabu. Asaheli alifia vitani alipokumbana ana kwa ana na Abneli. Katika vita

hivyo, iwapo Asaheli angepata nafasi ya kumwangamiza Abneli vitani, basi angemwangamiza. Ndiposa Yoabu anamuua Abneli kama kisasi cha kumuua nduguye Yoabu vitani. Mambo haya yanatendeka katika utawala wa Daudi. Daudi anamhuzunikia Abneli kwani haoni kwanini Abneli asingesamehewa na Yoabu. Wimbo huu unasisitiza umuhimu wa msamaha kwani pasipo na msamaha hutokea majanga yasiyotarajiwa. Kwa mfano;

Mfano 16: ***Wimbo wa Abneli***

Maana neno msamaha kwa mpumbavu
Litamuuwa tu
Ila neno msamaha kwa mwerevu
Litamuinua…
Maana mwoyo wa mwanadamu sasa
Umekunja ngumi
Roho ya huruma haipo tena
Roho ya kisasi inatenda kazi

Baada ya Sauli kufa
Abneli alirudi kwa Daudi
…Akasahau Yoabu anakumbuka
Kifo alichomuuwa nduguye Asaheli wakati wa vita
Yaobu akamuuwa Abneli
Abneli hakutambua hilo
Yeye alivyotengeneza na Daudi
Akajua maadui wamekwisha

Kulingana na usimulizi huu, Daudi alishangazwa na kifo cha Abneli, ambacho hakingefanyika iwapo Yoabu angemsamehea Abneli kwa kusababisha kifo cha Asaheli vitani.

3.2.4 Nafasi ya marafiki katika maisha ya mja

Rafiki ni mtu anayependana na kuaminiana na mwengine. Nyimbo kadhaa alizotunga na kuwasilisha Bahati Bukuku zikitumia usimulizi kama mtindo zimedhihirisha nafasi ya rafiki katika maisha ya mhusika. Kuna marafiki ambao wanaweza kujenga maisha ya mhusika ilhali kuna wale ambao wanazua madhara katika maisha ya mhusika.

Wimbo wa *Maamuzi* unadhihirisha marafiki ambao wana msaada katika maisha ya mja. Baada ya kuteseka kwingi baada ya kumzaa Sinona, rafiki zake Tundo walimtembelea na kuhuzunikia sana hali iliyomkumba Tundo. Mwili wa Tundo ulikuwa umebadilika sana. Sehemu ya mwili wake ulikuwa umepooza huku ngozi yake ikibadilika na kufanana na magamba ya nyoka. Vilevile, alikuwa akihisi uchungu sana kwa kung'atwa na mwanawe, Sinona, ambaye alizaliwa akiwa na meno kama ya mtu mzima. Marafiki wa Tundo ndio walimpa wazo kuwa kuna mhubiri ambaye angeweza kumsadia ili kupoza hali yake. Baada ya kwenda kanisani alikoelekezwa na rafiki zake waliomjali, anaombewa na inabainika kuwa Sinona hakuwa binadamu, bali Chatu mkubwa. Inabainika wazi ni kwanini Tundo alipitia matatizo yale mengi aliyokuwa nayo. Tazama mfano huu;

Mfano 17: *Wimbo wa Maamuzi*

Tundo alilia akisema, mwili wangu wote
Sasa umebadilika
Rangi ya ngozi ya nyoka Tundo
Iligeuka ikawa gamba la nyoka mwili mzima
Siku moja marafiki zake wakamtembelea Tundo
"Tuna mhubiri anahubiri twende
Ukaombewe Tundo"…
Akamwambia Tundo njoo mbele
Tundo akijua Mungu amesikia…
Mhubiri akamwambia Tundo
Mshushe mtoto wako hapa kwenye madhabao
Akaomba kwa imani sana
Mtoto aligeuka Chatu mara ile.

Inabainikia Tundo kuwa mwanawe alikuwa Chatu kwa vile marafiki walimsihi wampeleke kwa mhubiri aombewe. Marafiki hawa wanajitokeza kuwa wenye msaada kwa Tundo. Iwapo marafiki hawa wa Tundo wasingemtembelea ili kumjulia hali, basi huenda Tundo asingewahi kupata msaada wowote. Marafiki hawa walikuwa wa kweli kwa Tundo kwa kuwa walimtembelea na

kumpa suluhu kwa kile kilichokuwa kikimkumba. Usimulizi huu umewatumia wahusika marafiki wa Tundo kama nyenzo ya uwasilishaji wa maudhui ya nafasi ya marafiki katika maisha ya mja.

Katika wimbo wa *Dunia haina huruma* msimulizi anaonyesha wazi nafasi finyu ya marafiki katika maisha ya mja. Marafiki wa mume wa msimulizi hawatoi msaada wowote kwa msimulizi wakati mume wake alipokuwa hospitalini katika chumba cha wagonjwa mahututi. Msimulizi alipowapigia ili waweze kumsaidia apate fedha za matibabu ya mumewe, marafiki wa mume wake wanampuuza na kukosa kumsaidia. Tazama mfano huu;

Mfano 18: *Dunia haina huruma*

Nawatafuta marafiki wa mume wangu
na kwanza ninapofika hapo
wanaanza kunipa masharti
Yanayorarua moyo wangu
Nikimtazama daktari hawezi ata kunitazama.

Mfano huu katika wimbo wa *Dunia haina huruma* unabainisha jinsi marafiki wa mume wa msimulizi walivyokuwa marafiki wasioweza kumsaidia mwenzao anayeugua. Wanampa msimulizi masharti ambayo yanaelekea kuurarua moyo wake.

Katika wimbo wa *lazima usamehe,* msimulizi anahadithia kumhusu rafiki yake aliyeanza kuugua ugonjwa wa ajabu. Ilimgharimu msimulizi muda mrefu, nguvu nyingi na juhudi ili amsaidie rafikiye dhidi ya hali ngumu iliyomkumba kwa sababu ya ugonjwa wake. Hata hivyo, anajutia sana baadaye kwani rafikiye alimgeukia na kuwa adui aliyefananishwa na msiba kwa msimulizi na ndiposa msimulizi anaapa kutomsamehea katu. Tazama mfano ufuatao;

Mfano 19: *Lazima usamehe*

Nilikuwa na rafiki yangu mzuri
Aliyeugua ugonjwa wa ajabu
Kwa huruma zangu nikamhurumia

Nikatumia muda wangu mwingi
Nikazunguka huku na kule kutafuta madaktari
Nikatembea huku na huko kutafuta uzima wake
Lakini Mungu sio mwanadamu
Alimhurumia
Akaachilia uzima ndani mwake akawa mzima
Nikatafuta ata wachungaji nao wakamwombea
Lakini mungu sio mwanadamu
Alimponya
Cha kushangaza alipona, malipo yangu
Aligeuka adui yangu
Amekuwa msiba kwangu.

Inabainika wazi kuwa hata baada ya mambo yote ambayo msimulizi alimfanyia rafikiye, bado alimgeuka msimulizi na kuwa adui yake. Wimbo huu kwa hivyo unasimulia kuhusu nafasi hasi ya marafiki katika maisha ya mja. Dhamira kuu ni kuonya dhidi ya kuwaamini marafiki kama hawa kwani huenda wakabadilika na kuwa maadui wakubwa.

3.2.5 Ushirikina

Ushirikina ni tabia ya kuamini mambo ya uchawi. Kama mwimbaji wa nyimbo za dini ya Kikristo, Bahati Bukuku amekejeli uwezo wa nguvu za kishirikina, kwa kuzihusisha na maovu yanayoleta madhara katika maisha ya mtu. Anadhamiria kuonya kuwa jibu la kukosa chochote si kuwakimbilia waganga wa kienyeji, bali kumtafuta Yesu, ambaye kulingana naye, ana uwezo wa kumtatulia mtu yeyote yule tatizo lake. Haya yanabainika katika wimbo wa *Maamuzi,* ambapo Tundo anamtafuta mganga kule Kongo ili aweze kumsaidia kusuluhisha tatizo lake sugu la kukosa mwana ambalo lilikuwa limeanza kuwakasirisha waliokuwa karibu naye. Tazama mfano huu;

Mfano 20: *Wimbo wa Maamuzi*

Alisumbuliwa na ugumba miaka mingi
Hata mawifi zake wote hawakumpenda tena
Ndoa yake ilikuwa matatani

Baada ya kupewa suluhu na mganga, anapata mtoto ambaye alianza kumletea madhara ya kiafya. Jambo la kustaajabisha ni kuwa, Sinona alizaliwa na meno kama mtu mzima. Alipomuuma Tundo, ngozi ilibadilika na akapooza upande mmoja wa mwili wake. Mwimbaji anadhamiria kuonya dhidi ya njia za mkato za kwenda kwa waganga. Tazama mfano ufuatao;

Mfano 21: *Wimbo wa Maamuzi*

Tundo aliamua kwenda kwa waganga
…Alikutana ma mganga mmoja nchini Kongo
Akampa dawa za kutosha Tundo
Tundo alizaa mtoto wa kiume
Jina lake alimwita Sinona
Maajabu aliyokuwa nayo mtoto yule
Alikuwa amezaliwa na meno
…Tundo kwa kuchelewa kwake alifurahi
Akaamini mganga amemsaidia
Lakini alipokuwa ananyonyesha mtoto yule
Ghafla aliung'ata mwili wake Tundo
Mwili ukapoa wote upande mmoja
Lilikuwa ni tatizo liliomsumbua Tundo…
…Rangi ya ngozi yake Tundo
Iligeuka ikawa gamba la nyonga mwili mzima…

Madhara anayoyapata Tundo baada ya kujifungua Sinona yanadhihirisha athari hasi za nguvu za kishirikina. Kilele cha usimulizi huu ni kubadilika kwa Sinona na kuwa Chatu baada ya waombezi kuomba. Tazama mfano huu;

Mfano 22: *Wimbo wa Maamuzi*

Mshushe mtoto wako hapa kwenye madhabahu
Akaomba kwa imani sana
Mtoto aligeuka Chatu mara ile
Kumbe Sinona sio mtoto, kumbe Sinona ni joka kubwa

Mwimbaji anashauri umuhimu wa kutafuta msaada kwa Mungu badala ya kutafuta nguvu za kishirikina ambazo hazitoi suluhu kwa matatizo ambayo yanamkumba mja.

3.2.6 Anasa

Anasa ni mambo au hali ya starehe na raha nyingi. Maudhui ya anasa yanabainika kupitia hadithi ya Tupatupa katika wimbo wa *Tupatupa*. Katika usimulizi huu, kisa kinasimuliwa kikimsawiri mzee Tupatupa kama mlevi na mpenda anasa. Mzee Tupatupa alikumbana na kifo chake kupitia ajali ya barabarani iliyosababishwa na ulevi wake mwenyewe. Tazama mfano huu;

Mfano 23: *Tupatupa*

Tupatupa siku moja alilewa
Aliona taa mbili zinakuja
Siku hiyo ilikuwa siku mbaya kwake Tupatupa
Aliona bila shaka hawa ni madereva wawili wa bodaboda, wanashindana
Jamani kumbe hakuwa dereva wa bodaboda
Ila lilikuwa ni gari la kubeba mchanga, yaani lori
Yule dereva wa lori alijaribu kuhepa
Lakini kwa kuwa mzee Tupatupa alikuwa amelewa
Akaendelea kusimama katikati ya barabara
Akitaka kuonyesha wale vijana kuwa yeye ni mwaname
Na ni kizito wa eneo hila
Mzee tupatupa aligongwa
Akapoteza fahamu palepale

Kulingana na maneno haya ya wimbo wa *Tupatupa*, kugongwa kwa Tupatupa kulisababishwa na kulewa kwake kulikompa kiburi cha kutaka atambulike kuwa mkuu sana katika eneo hilo.

Vilevile, usimulizi wa Tupatupa unadhihirisha kuwa mzee huyu aliwapenda wanawake sana. Hii inadhihirisha uzinifu wake. Tazama mfano ufuatao;

Mfano 24: *Tupatupa*

Alikuwa tajiri tena mwenye sura nzuri
Kila aliyemuona alijua mambo sawa
Mzee Tupatupa alipoona wadada…
Mambo yake yalikuwa ni hivi
Ebu ngoja leo sikia nikuambie

> "Mtoto mzuri, malkia, malkia, mrembokama wewe unatembea chini? Mimi nikikuoa, nitakununulia ndege uifanye kama daladala, nitakuwa nakupeleka huko Karioko, wakati mwingine Masaki, nitaifanya dunia ikuwe kijiji kidogo kwako;

Usemi huu wa Tupatupa unadhihirisha uzinifu wake kwa wanawake. Isitoshe, Tupatupa alipofika Jehanamu kwa mara ya kwanza alipendezwa sana kuwapata wanawake wazuri ambao hakuwahi kuwaona kama wao kote duniani. Mbali na wanawake wale warembo, kulikuwa na vileo vya aina tofautitofauti vilivyompendeza sana Tupatupa. Hii ndiyo sababu aliomba kurudishwa jehanamu baada ya kufika mbiguni kwani kule mbiguni hakuona wanawake wowote, wala raha aliyoitaka. Tazama mfano huu;

Mfano 25: *Tupatupa*

> …akaona Jahanamu kuna wanawake wazuri
> Tangia kuwa dunia kwa Tupatupa
> Hakuwahi kuona wanawake wa namna hiyo
>
> Mzee Tupatupa alipofika mbinguni…
> Jambo lililomkwaza sana mzee Tupatupa
> Kwa kuwa hakupenda mazingiza yake
> Maana yeye alijua akifika mbinguni
> Ataona wanawake wazuri
> Lakini haikuwa hivyo.

Usemi wa shetani kwa Tupatupa vilevile unadhihirisha jinsi duniani kulikuwa na matukio ya kianasa. Kwa mfano;

Mfano 26: *Tupatupa*

> Shetani akasema, "Hapana, ningekuwa na roho mbaya mimi walevi hawangeweza kununuliana makreti ya bia. Tena mimi ningekuwa na roho mbaya, wajane hawangeweza kushare mabwana. Tena mimi ningekuwa na roho mbaya, wavuta sigara hawangeweza kupeana vijisi barabarani.

> Mimi ni mkarimu bwana, naweza kukupa kreti ya bia lakini nikakunyima kibaba cha unga."

Usemi huu unadhihirisha kuwa kuna ulanguzi mkubwa wa dawa za kulevya duniani, vilevile unywaji pombe kwa kiasi kikubwa. Haya yanabainika Shetani anaposema, "… ningekuwa mbaya mimi walevi hawangeweza kununuliana makreti ya bia…mimi ningekuwa na roho mbaya, wavuta sigara hawangeweza kupeana vijisi barabarani…" maneno haya ya Shetani yanaonyesha wazi kuwa duniani kuna wingi wa matumizi ya pombe na sigara.

Matendo ya mhusika Tupatupa yanadhihirisha maudhui ya anasa na hivyo basi kumdhihirisha mhusika huyu kama kipengele muhimu sana katika uwasilishaji wa maudhui hayo.

3.2.7 Nafasi ya mwanamke katika jamii

Wanawake wanajipata kuwa na nafasi bora katika nyimbo zilizoimbwa na Bahati Bukuku. Mhusika Esther, katika wimbo wa *Waraka*, unaopatikana katika *Maandiko Matakatifu* (1952), katika kitabu cha Esther, anajitokeza kuwa na nafasi kubwa ya kuwaokoa Wayahudi kutoka kwa mikono katili ya Hamani, aliyetaka kuwaangamiza. Alipotumwa na Modekai aelekee katika malango ya Mfalme, Esther anaitikia wito wa kwenda kwa Mfalme kumjuza kuhusu utesi na mipango ya Hamani. Ndipo Mfalme kwa ghadhabu, anaamuru Hamani avikwe sanda ili afie mbali. Hivyobasi, Esther anajitokeza kuwa mkombozi wa Wayahudi. Tazama mfano huu;

Mfano 27: *Wimbo wa Waraka*

…Waraka ulioandikwa
Wayahudi wauwawe
…Esther akiwa kwenye nyumba ya kifalme
Esther akiwa ni malkia
Ndipo Modekai alirarua mavazi yake
…Akasimama mbele ya malkia
Akamwambia Esther mama naomba
Sikia ujue umekuwa Esther kwa wakati huu

Hakuna wakati mwingine waweza kutuokoa
…Esther aha alikwenda kwenye malango ya kifalme
Kinyume cha taratibu
Akamwambia eh mfalme ukiona vyema
Waweza kuniruhusu niingie malangoni pako

…Esther, kwa machozi, akamwambia eh baba yangu
Naomba subira
Mimi na Wayahudi wote
Tumetangaziwa kuuwawa
Na huyu adui wangu mtesi, naye ni Hamani

Mfalme akasimama akamtazama malkia
Kwa ghadhabu akageuka akamtazama Hamani
Akasema, mtoeni nje Hamani
Nenda mvike sanda nyeusi akafie huko

Inavyodhihirika katika dondoo hili, mwanamke Esther anajitokeza kuwa mkombozi ambaye anawahakikishia Wayahudi wote usalama kwa sababu ya jitihada zake za kuwaokoa kutokana na mipango miovu ya mhusika Hamani ambaye alikuwa amewatangazia kifo. Kwa sababu ya juhudi za Esther, wayahudi wanapona huku aliyekuwa amewatangazia kufa, Hamani, akihukumiwa kifo na mfalme. Mwanamke Esther anajidhihirisha kama mkombozi wa wengi, kwa tendo lake la kijasiri la kuwaokoa wayahudi wengine.

3.4 HITIMISHO.

Sura hii imejadili maudhui kama yanavyojitokeza katika nyimbo teule za Bahati Bukuku. Uhakiki wa maudhui umeweza kudhihirisha nafasi ya usimulizi katika kuwasilisha ujumbe unaopatikana katika nyimbo hizo teule. Uhakiki wa maudhui ulizingatia vipengele fulani ambavyo hufanikisha uwasilishaji wa maudhui katika simulizi. Vipengele vilivyotumiwa vilikuwa: uhusika, mandhari pamoja na mfuatano wa matukio. Mifano ilitolewa jinsi vipengele hivi vilichangia kujitokeza kwa maudhui hayo. Maudhui yaliyojadiliwa katika sura hii ni pamoja na: Imani ya dini, msamaha, nafasi ya marafiki katika maisha ya mja, ushirikina, anasa, nafasi ya mwanamke katika jamii

pamoja na unafiki. Maudhui ya unafiki yameelezwa kwa utendeti kwa kurejelea wahusika mbalimbali ambao walidhihirisha unafiki kwa wahusika wengine. Mifano maridhawa imeweza kutolewa ili kutetea uwasilishaji wa maudhui tajwa.

Lengo kuu la sura hii limekuwa kudhihirisha jinsi usimulizi unavyowasilisha maudhui katika nyimbo zilizosampuliwa kufanikisha utafiti huu. Sura inayofuata inahusu uchanganuzi wa sauti ya usimuliaji na mahusiano ya wakati wa usimulizi katika nyimbo teule za Bahati Bukuku.

SURA YA NNE

SAUTI YA USIMULIAJI NA MAHUSIANO YA WAKATI WA USIMULIZI KATIKA NYIMBO TEULE ZA BAHATI BUKUKU

4.0 Utangulizi

Sura hii inalenga kubainisha jinsi sauti ya usimuliaji, kama kipengele muhimu cha kuhakiki usimulizi imejitokeza katika nyimbo teule zenye sifa za kisimulizi zilizowasilishwa na msanii Bahati Bukuku. Utafiti umeanza kwa kutoa ufafanuzi wa dhana ya sauti ya usimuliaji kwa mujibu wa nadharia ya naratolojia. Maoni ya wananaratolojia mbalimbali kuhusu dhana ya sauti ya usimuliaji yametolewa ili kurahisisha uelewaji wa dhana hii. Utafiti huu umechanganua mtazamo wa Stanzel (1984) aliyehakiki sauti ya usimuliaji kwa kurejelea nafsi tatu za usimuliaji; nafsi ya kwanza, nafsi ya pili na nafsi ya tatu. Maoni ya wataalamu wengine wa kinaratolojia, kama vile Genette (1980), Lanser (1984), Fludernik (1993) na Manfred (2005) yamefafanuliwa kwa utendeti ili kuendeleza uelewaji wa dhana hii ya sauti ya usimuliaji. Mifano mwafaka imetolewa kutoka katika nyimbo teule za Bahati Bukuku ili kuendeleza maoni ya wananaratolojia hawa.

Sura hii vilevile imechanganua mahusiano ya wakati wa usimulizi kwa kuhakiki vipengele vyake muhimu kama usimulizi baadaye, usimulizi kabla, usimulizi sawia na usimulizi zongomezi. Maoni ya wataalamu wa kinaratolojia kuhusu vipengele hivi vya mahusiano ya wakati wa usimulizi yamefafanuliwa ili kuelewa zaidi dhana ya usimuliaji.

4.1 Sauti ya Usimuliaji

Kwa mujibu wa Genette (1980), msimulizi wa hadithi ana nafasi kubwa sana katika kufanikisha uwasilishaji wa hadithi hiyo. Anaeleza kuwa, kiini cha simulizi kinatokana na anayeona na kusimulia simulizi hiyo. Sauti ya usimulizi hujenga uhusiano na anayesimuliwa. Mtazamo wa masimulizi, mfuatano wa matukio pamoja na dhamira kuu huwasilishwa na msimulizi. Genette (1980) anaeleza kuwa kila msimulizi huzingatia njia maalum ambayo itaibua uhusiano kati yake

na anayesimuliwa. Kwa kuwa sauti ya msimulizi ndiyo inayojenga uhusiano na msimuliwa, basi yale yasemwayo na msimulizi yanaweza kuhakikiwa. Genette (keshatajwa) anaeleza kuwa sauti ya usimuliaji inaweza kuendelezwa kwa mitazamo miwili mikuu; usimulizi wa ndani na usimulizi wa nje. Genette (keshatajwa) anafafanua usimulizi wa ndani kuwa mtazamo wa usimulizi unaoelekezwa katika nafsi ya kwanza ilhali usimulizi wa nje ni ule unaoelekezwa katika nafsi ya tatu, ambapo msimulizi anasimulia matukio akiwa nje ya usimulizi wenyewe.

Mwananaratolojia mwengine, Stanzel (1984), anaunga mkono uhakiki wa Genette (keshatajwa) kuhusu ufafanuzi wa sauti ya usimuliaji. Hata hivyo, anatofautiana naye Genette katika mitazamo ya kuendeleza sauti za usimuliaji. Stanzel (keshatajwa) anaeleza kuwa mitazamo hii inaweza kuendelezwa kinafsi kutegemea mfumo wa kisarufi. Anapendekeza ufafanuzi wa sauti ya usimuliaji katika nafsi ya kwanza, nafsi ya pili na nafsi ya tatu. Mitazamo wa Gennete (keshatajwa) na Stanzel (keshatajwa) inafanana katika maelezo ila inatofautiana katika majina. Vilevile, Stanzel (keshatajwa) aliendeleza mtazamo wake zaidi ya mtazamo wa Gennete (keshatajwa) kwa kufafanua usimulizi wa nafsi ya pili ambao haukutathminiwa naye Gennete (keshatajwa). Sehemu hii ya utafiti imejiegemeza katika maoni ya Stanzel (keshatajwa) kwa kuwa mtazamo wake uliegemea nafsi zote ambazo hutumiwa katika kusimulia visa katika simulizi.

4.1.1 Usimulizi wa nafsi ya kwanza

Kwa mujibu wa Stanzel (1984), usimulizi wa nafsi ya kwanza ni usimulizi unaowasilishwa katika nafsi ya kwanza. Anaeleza kuwa usimulizi wa aina hii huainishwa kwa kutumia kiambishi cha nafsi ya kwanza “ni” katika umoja na “tu” katika wingi. Aidha, mbali na matumizi ya kiambishi cha nafsi ya kwanza, Stanzel (keshatajwa) anafafanua kuwa usimulizi huu pia hubainika kwa kutumia kiwakilishi nafsi huru “mimi” katika umoja na “sisi” katika wingi. Msimulizi husimulia kuhusu matendo yake mwenyewe na kuwapuuza wahusika wengine.

Kwa mujibu wa Lanser (1981), katika usimulizi wa nafsi ya kwanza, msimulizi hawezi kupatikana mahali kuwili kwa wakati mmoja. Anasema kuwa ni vigumu kwa msimulizi kujua yale ambayo yatatendeka katika wakati ujao, wala hawezi kusimulia kuhusu kifo chake. Wamitila (2002) anaeleza kuwa msimulizi, ambaye ndiye mhusika mkuu katika usimulizi wa nafsi ya kwanza, husimulia kutokana na mkabala mmoja pekee, na kwamba mitazamo yote ya usimuliaji inamhusu yeye. Mohamed (1995) hata hivyo anaeleza kuwa msimulizi anapaswa kuwa mwangalifu sana, asitumie "ni" na "mimi" kwa wingi, kwani anaweza kuwachosha wasomaji wake.

Kwa mujibu wa Gennete (1980), usimulizi wa aina hii unajulikana kama usimulizi wa ndani. Anaeleza kuwa huu ni mtazamo wa usimulizi ambapo sauti ya msimulizi husimulia matini katika nafsi ya kwanza. Kiambishi "ni" au "tu", katika umoja na wingi mtawalia huweza kutumika na msimulizi kwa kiwango kikubwa. Vilevile, maneno kama "mimi" au "sisi", katika umoja na wingi mtawalia hushirikishwa kwa kiwango kikubwa.

Kwa kuzingatia maoni haya ya usimuliaji wa ndani, msimulizi anajitokeza kuwa mmojawapo kati ya wahusika katika usimulizi unaowasilishwa. Matukio mengi pamoja na migogoro inayojitokeza katika usimulizi humzingira mhusika huyu. Genette (keshatajwa) anafafanua umuhimu mkubwa wa usimuliaji wa ndani, nao ni kuchangia katika kufupisha masafa ya kihisia kati ya mhusika mtendaji na msomaji wa matini.

Usimulizi wa aina hii unadhihirika katika wimbo wa *Lazima usamehe*. Msimulizi anasimulia kisa chake moja kwa moja. Kuna matumizi ya kiambishi nafsi "ni" katika usimulizi wake. Tazama mfano huu;

Mfano 1: *Lazima usamehe*

Nilikuwa na rafiki **yangu** mzuri
Aliyeugua ugonjwa wa ajabu
Kwa huruma zangu **ni**kamhurumia

Nikatumia muda **wangu** mwingi
Nikazunguka huku na kule kutafuta madaktari
Nikatembea huku na huko kutafuta uzima wake
Lakini Mungu sio mwanadamu
Ali**ni**hurumia
Akaachilia uzima moyoni mwake akawa mzima
Nikatafuta ata wachungaji nao wakamwombea
Lakini Mungu si mwanadamu
Alinisikia
Niliposema Mungu mponye, alisikia
Kwa kuwa Mungu si mwanadamu, alimponya
Cha kushangaza alipopona, malipo **yangu**
Aligeuka adui **yangu**
Amekuwa msiba **kwangu**…

Katika dondoo hili, msimulizi anasimulia kuwa alikuwa na rafiki yake aliyeugua ugonjwa wa ajabu. Msimulizi alizunguka huku na kule kumtafutia rafiki yake msaada ili apone, ila hakufanikiwa. Msimulizi akamgeukia Mungu ili aweze kumponya rafikiye, hadi akapona. La kumshangaza msimulizi ni kuwa, baada ya rafikiye kupona, alimgeuka msimulizi na kuwa adui yake. Ndipo msimulizi anaapa katika usimulizi wake kuwa hawezi kumsamehea kwa lolote.

Inavyobainika, kuna matumizi ya viambishi vya nafsi ya kwanza, kama alivyodokeza Stanzel (1984). Maneno kama; “nilikuwa”, “nikamhurumia”, “nikatuma”, “nikazunguka” na “nikatembea” yametumika katika dondoo hili kubainisha wazi kuwa usimulizi unaorejelewa ni ule wa nafsi ya kwanza, kwa kuwepo kiambishi “ni” cha nafsi ya kwanza. Vilevile, kuna matumizi ya vivumishi vimilikishi vya nafsi ya kwanza. Kwa mfano; malipo *yangu*, adui *yangu*, msiba *kwangu*. Kwa kuongezea, katika dondoo hili, msimulizi anasimulia kutokana na mkabala mmoja pekee, kama alivyodokeza Wamitila (2002).

Usimuliaji wa aina hii vilevile unadhihirika katika wimbo wa *Dunia haina huruma*. Mhusika mkuu ndiye msimulizi na matukio yote yanamzingira yeye. Tazama mfano ufuatao;

Mfano 2: ***Dunia haina huruma***

Ni asubuhi na mapema
Simu ya mkononi inaita
Naitazama kwa makini
Ni namba ya mume **wangu**
Sauti ya mwanamke inasikika
Inayorarua moyo **wangu**
Moyo **wangu** unafura hasira
Kwa taarifa **ni**nazopata
"Hallo, nenda mwimbini kachukue mzoga wako."
Namuuliza ni nani mwenzangu
Ana**ni**jibu kwa kejeli
"**Mimi** ni mke mwenzio kama hutaki potezea."
… **Na**watafuta ndugu na jamaa
Waliokuwa kwenye simu **yangu**
Ili niwaambie taarifa hizi
Zinazorarua moyo **wangu**…

Inavyobainika katika dondoo hili, ambalo ni sehemu tu ya wimbo wote wa *Dunia haina huruma*, matukio mengi kuanzia mwanzo hadi mwisho yamemhusisha msimulizi. Msimulizi anapigiwa simu asubuhi kujuzwa kuhusu mauko ya mumewe, anafika hospitalini na kupata kumbe mume wake hajafa, bali yuko kwenye chumba cha wagonjwa mahututi. Msimulizi anachukua jukumu la kumwokoa mume wake. Anajaribu kutafuta msaada kutoka kwa ndugu na jamaa, ila wanampa tu visababu bila kumsaidia kwa njia yoyote. Kwa wakati mmoja, msimulizi anajitolea kumpa daktari gari lake, ila daktari anakataa gari hilo kwa kusingizia unywaji mwingi wa mafuta wa gari hilo. Baada ya kukosekana kwa suluhisho, msimulizi anaamua kufanya mapenzi na daktari ili mumewe atibiwe. Baadaye msimulizi anabaini kuwa yu mja mzito, na baada ya kujifungua, anaamua kumwambia mume wake ukweli kuwa mtoto aliyezaliwa alikuwa wa daktari. Ni hapo ndipo matatizo yake yanapoanza, hadi kuitwa kwenye kikao kijijini kujibu mashtaka ya kumwendea mumewe kinyume.

Inabainika kuwa kuna wingi wa matumizi ya kiambishi cha nafsi ya kwanza “ni” pamoja na kiwakilishi nafsi huru “mimi”. Vilevile, kuna matumizi ya maneno yanayoonyesha kuwa ni msimulizi wa nafsi ya kwanza anayezingirwa na vitushi katika usimulizi. Kwa mfano; “naitazama”, “ninazozipata”, “namuuliza” na “nawatafuta”. Kwa kuongezea, msimulizi anatumia maneno yenye umiliki wa nafsi ya kwanza, kwa mfano, “wangu”. Uchunguzi huu umeonyesha kuwa wimbo wa *Dunia haina huruma* umehusisha msimulizi anayeshiriki katika matukio ambayo yeye mwenyewe anasimulia.

4.1.2 Usimulizi wa nafsi ya pili

Stanzel (1984) anaeleza kuwa katika usimulizi wa nafsi ya pili, msomaji huhusishwa katika masimulizi. Usimulizi wa aina hii hutumia kiambishi cha nafsi ya pili “u” ili kujenga uhusiano wa karibu kati ya msimulizi, mhusika mwengine na wasomaji.

Kwa mujibu wa Fludernik (1993), msimulizi akitaka kufanikiwa katika kubadilisha mtazamo wa usimulizi, hana budi ila kutumia nafsi hii. Msimulizi humrejelea na kumhusisha msomaji wake, au mhusika mwengine, katika matini, moja kwa moja. Humfanya msomaji aweze kuamini yanayosimuliwa. Kwa kurejelea ufafanuzi wa Fludernik (keshatajwa), inabainika kuwa matumizi ya nafsi ya pili katika usimulizi hujengwa na nafsi ya kwanza na vilevile nafsi ya tatu.

Usimulizi wa nafsi ya pili unajitokeza katika wimbo wa *Waraka.* Ingawa usimulizi unaopatikana katika wimbo huu ni ule wa nafsi ya tatu, msimulizi anabadilisha usimulizi wake na kuwa wa nafsi ya pili, wakati mhusika Esther alipoelekea kwa mfalme kumweleza kuhusu mpango wa Hamani wa kutaka kuwaangamiza Wayahudi wote. Tazama mfano huu;

Mfano 3: *Waraka*

…Akamwambia eh Mfalme **u**kiona vyema
Waweza kuniruhusu niingie malangoni **pako**

Esther kwa maombolezo
Huku akisindikizwa na maombi ya Wayahudi

…Mfalme akasimama
Akamtazama Malkia
Akachukua fimbo yake akamnyoshea…

…Akamwambia eh Mfalme **u**kiona vyema aha
Sasa nimeandaa meza karibu **u**nywe
Akamwambia eh Mfalme **u**kiona vyema aha!
Sasa nimeandaa meza **u**je na Amani

…Esther, kwa machozi, akamwambia eh baba yangu
Naomba subira
Mimi na Wayahudi wote
Tumetangaziwa kuuwawa
Na huyu adui wangu mtesi, naye ni Hamani
Tumetangaziwa kuuwawa
Na huyu adui wangu mtesi naye ni Hamani…

Usimulizi wa nafsi ya pili ni tegemezi, kama anavyohoji Manfred (2005). Hujiegemeza katika nafsi nyinginezo. Hii ndiyo kwa sababu umejitegemeza katika nafsi ya tatu kama ilivyojitokeza katika **mfano 3** wa *Waraka.*

Katika dondoo hili, Esther anamweleza Mfalme moja kwa moja kuhusu mipango ya Hamani ya kuwaangamiza Wayahudi wote katika ufalme huo. Esther akiwa katika nafsi ya kwanza, anamtaarifu Mfalme aliye katika nafsi ya pili. Mfalme vilevile anamjibu Esther moja kwa moja. Sehemu ya usimulizi inayomhusu Mfalme na Esther haihadithiwi moja kwa moja na msimulizi, kwani kwa kusimulia, angetumia nafsi ya tatu. Hivyo anabadilisha usimulizi wake kuwa wa nafsi ya pili ili msomaji au msikilizaji apate ufahamu zaidi au uhakika wa yanayotokea.

Ithibati ya matumizi ya usimulizi wa nafsi ya pili inajitokeza katika maneno kadhaa yanayotumiwa katika dondoo. Kwa mfano, maneno “ukiona vyema” yanaonyesha wazi kuwa katika usimulizi huu, mhusika Esther anamzungumzia mfalme maneno hayo moja kwa moja wakizungumza

wawili. Vilevile, maneno, “Waweza kuniruhusu niingie malangoni pako” yanaonyesha mhusika Esther akimsihi mfalme moja kwa moja.

Usimulizi wa nafsi ya pili pia unajitokeza katika wimbo wa *Dunia haina huruma*. Usimulizi huu unabainika katika maongezi yaliyofanyika nje ya usimulizi wa hadithi hiyo. Hii ni kwa sababu, kama ilivyoelezwa awali, katika maoni ya Manfred (2005), usimulizi wa nafsi ya pili hutegemea usimulizi katika nafsi ya kwanza na ya tatu. Usimulizi huu unabainika kati ya msimulizi na wahusika aliowaomba msaada ili mumewe aweze kupewa matibabu. Tazama mfano ufuatao;

Mfano 4: *Dunia haina huruma*

…Mashemeji wamegoma kutoa msaada
Maneno wanayoniambia,
“Samahani shemeji, ningeweza ku**ku**saidia,
lakini ninaenda kutazama mpira Ulaya.”
Nawatafuta mawifi kwa mara nyingine
“Kwa kweli wifi si **u**najua, tungeweza
ku**ku**saidia lakini wenzangu wote wacheza
shengele watakuja siku ya Jumamosi,
kwa hiyo nimewaambia na siwezi kughairi
kwa kuwa wameshona sare.”

Ingawa usimulizi umejengeka katika msingi wa nafsi ya kwanza, baadhi ya sehemu zinadhihirisha usimulizi wa nafsi ya pili. Shemeji wa msimulizi anamweleza, “ningeweza kukusaidia” kumaanisha kuwa sehemu hii si usimulizi wa moja kwa moja wa msimulizi. Iwapo sehemu hii ingekuwa katika usimulizi, basi msimulizi angeieleza kwa usemi wa taarifa kuwa, “Shemeji niliyemwomba msaada alinieleza kuwa angeweza kunisaidia lakini alikuwa anaenda kutazama mpira ulaya.” Mfano mwingine wa matumizi ya usimulizi wa nafsi ya pili unadhihirika katika maneno ambayo mawifi wa msimulizi walimueleza baada ya kuwaomba msaada. Mawifi wanamueleza kuwa, “Kwa kweli wifi si unajua tungeweza kukusaidia, lakini wenzangu wote wacheza shengele watakuja siku ya Jumamosi…” Kwa kurejelea dondoo hili, kuna mazungumzo ya moja kwa moja kutoka kwa mawifi kumwendea msimulizi. Neno “Unajua” pamoja na

“kukusaidia” linamwendea mhusika wa nafsi ya pili, ambaye ndiye msimulizi wa hadithi hii, moja kwa moja. Kwa kutumia nafsi nyingine, basi maneno yanayotumia nafsi ya pili huenda yasingekuwepo. Kwa hivyo, ni wazi kuwa kuna matumizi ya usimulizi wa nafsi ya pili.

Aidha, baada ya kupata ujauzito kutoka kwa daktari aliyemuuguza mumewe, msimulizi anaamua kumweleza mumewe ukweli wa mambo. Msimulizi anamwelekezea maneno mumewe kama inavyojitokeza katika mfano ufuatao;

Mfano 5: ***Dunia haina huruma***

“Mume wangu ile siku **u**lipocharazwa mapanga,
yule daktari aliyekuwa anakuuguza ndiye mwenye
mtoto huyu.”

Kwa kuzingatia dondoo hili, baadhi ya maneno yanaonyesha kurejelewa kwa mhusika wa nafsi ya pili. Kwa mfano, neno “ulipocharazwa” lina kiambishi cha nafsi ya pili “u”. Kiambishi hiki “u” kinaonyesha wazi ni nani aliyeathiriwa na kitendo cha kucharazwa, ambaye ni mhusika wa nafsi ya pili. Vilevile, neno “anakuuguza” lina kiambishi cha yambwa “ku”, cha nafsi ya pili. Hii ina maana kuwa mzungumziwa ndiye alikuwa akiuguzwa na daktari. Uhusiano wa karibu hujengwa kati ya msimulizi, mhusika mwengine na wasikilizaji, kama alivyodokeza Stanzel (1984).

Mbali na matukio haya, baada ya kuitwa kwenye kikao kule kijijini, ili kujibu mashtaka kuhusu kumpata mtoto nje ya ndoa, mawifi wa msimulizi wanamwelekezea maneno machungu moja kwa moja. Tazama mfano huu;

Mfano 6: ***Dunia haina huruma***

…“Kama **u**nataka kukaa na mtoto wetu, mtoto wako
ni lazima auawe maana sisi hatumtambui mtoto
haramu katika familia yetu.”

…Nilipoendelea kuomba msamaha
Wifi mkubwa alinyanyuka
"**U**natuletea usanii hapa. Fanyia kaka yetu hukohuko.
Sisi ni watoto wa mjini bwana hatutishwi na machozi.
Sasa huo upumbavu **wako** usituletee mbele ya kikao."

Kwa kurejelea dondoo hili, maneno kama, "unataka", "unatuletea" na "usituletee" yana viambishi vya nafsi ya pili "u" pamoja na yambwa inayowakilisha nafsi ya pili. Mhusika anayemwambia msimulizi neno "unataka" anamiliki nafsi ya kwanza, akimwelekezea nafsi ya pili moja kwa moja. Vilevile, kuna matumizi ya maneno yanayoonyesha umiliki katika nafsi ya pili. Kwa mfano, msimulizi anapoelezwa kuwa, "…mtoto wako ni lazima auwawe…" anaelekezewa maneno hayo moja kwa moja kama mhusika atakayeathiriwa na kitendo cha kumwangamiza mtoto.

4.1.3 Usimulizi wa nafsi ya tatu

Kwa mujibu wa Stanzel (1984), usimulizi wa nafsi ya tatu hutambulishwa kwa kutumia kiambishi "a". Katika usimulizi huu, msimulizi huwa amejitenga na mambo ambayo anayasimulia na hawezi kuwa mojawapo wa wahusika katika usimulizi huo. Wamitila (2002) anaeleza kuwa msimulizi huyu huwa na ufahamu mkubwa kuhusu matendo ya wahusika wote katika masimulizi.

Katika usimulizi huu, mwandishi hujikita na kujibana katika mhusika mmoja pekee yake. Mohamed (1995) anaeleza kuwa usimulizi huu humpatia mhusika mmoja nafasi ya kusimulia hadithi badala ya msimulizi pekee kuisimulia hadithi yote.

Kulingana na maoni ya Genette (1980), usimuliaji wa aina hii, anaourejelea kama usimuliaji wa nje, ni mtazamo wa usimulizi ambapo msimulizi huwa nje ya ulimwengu wa hadithi. Msimulizi husimulia hadithi moja kwa moja bila kuwa mshiriki katika hadithi yenyewe. Anaposoma hadithi, msomaji hawezi kumtambua msimulizi moja kwa moja, kwani hakuna uhusiano wowote kati ya msimulizi na hadithi yenyewe. Hata hivyo, kama wanavyodokeza Njogu na Chimerah (1999),

ingawa msimulizi hausiki kama mshiriki katika usimulizi wa nje, huonyesha ujuzi wa kila jambo lililotendeka katika usimulizi huo.

Usimuliaji wa nje umejitokeza katika wimbo wa *Tupatupa.* Kuanzia mwanzo wa usimulizi huu unaomhusu mhusika Tupatupa, inabaikika kuwa msimulizi ana ufahamu mkubwa kumhusu mhusika Tupatupa. Alifahamu tabia za mhusika huyu, ndiposa anaeleza kwa urahisi kuhusu tabia ya mhusika Tupatupa pindi tu anapowaona wanawake. Tazama mfano ufuatao;

Mfano 7: *Tupatupa*

Alikuwa tajiri tena mwenye sura nzuri
Kila **a**liyemwona alijua mambo sawa
Mzee Tupatupa **a**lipoona wadada
Kila **a**liyemwona **a**lijua **a**mepona
Mambo **yake** yalikuwa ni hivi
Ebu ngoja leo sikia nikwambie
"Mtoto mzuri, malkia, malkia, mrembo kama wewe
unatembea chini? Mimi nikikuoa nitakununulia ndege
uifanye kama daladala. Nitakua nakupeleka huko
Karioko, wakati mwingine Masaki, nitaifanya dunia
iwe kijiji kidogo kwako."

Usimulizi huu wa nafsi ya tatu unatolewa na msimuliaji aliye nje ya ulimwengu wa hadithi yenyewe. Anajitokeza kuwa na ufahamu wa hadithi hii kuanzia mwanzo hadi mwisho. Vilevile, baadhi ya maneno yanayotumiwa katika dondoo hili yanadhihirisha kuwepo kwa mhusika wa nafsi ya tatu ambaye anasimuliwa, na kuwa vitushi vyote vinamzingira yeye. Kwa mfano, neno "alikuwa", linamrejelea mhusika mkuu, ambaye ni Tupatupa. Kwa kutumia kiambishi cha nafsi ya tatu "a", msikilizaji anafahamu fika kuwa anayehadithiwa ni wa nafsi ya tatu. Aidha, maneno "aliyemwona" pamoja na "alijua" yanadhihirika katika dondoo kuwarejelea wale waliokuwa wakishuhudia maisha ya mhusika Tupatupa moja kwa moja, ambao vilevile wako katika nafsi ya tatu.

Mbali na kufahamu hulka za mhusika Tupatupa, msimulizi anasimulia matukio ya hadithi hiyo kuanzia mwanzo hadi mwisho kwa ujuzi mkubwa. Msimulizi anatangulia na jinsi Tupatupa alivyolewa hadi alipobaini ukweli kuhusu Shetani na Jehanamu. Tazama mfano huu;

Mfano 8: *Tupatupa*

> Tupatupa siku moja **a**lilewa, **a**liona taa mbili zinakuja
> Siku hiyo ilikuwa siku mbaya kwake Tupatupa
> **A**liona bila shaka hawa ni madereva wawili wa bodaboda
> wanashindana, jamani kumbe hakuwa dereva wa bodaboda
> Ila lilikuwa ni gari la kubeba mchanga, yaani lori
> Yule dereva wa lori **a**lijaribu kuhepa
> Lakini kwa kuwa mzee Tupatupa **a**likuwa kalewa
> **A**kaendelea kusimama katikati ya barabara
> **A**kitaka kuonyesha wale vijana kwamba yeye ni mwanamme,
> na kizito wa eneo hilo
> Mzee Tupatupa **a**ligongwa, **a**kapoteza fahamu palepale
> Malaika **a**katokea, **a**kamuuliza mzee Tupatupa
> Kuna njia mbili mbele yako. Unataka kwenda wapi?
> Mzee Tupatupa **a**likuwa mwanadini
> Neno **a**lilosema, “Nataka kwenda mbinguni.”
> Yule mtu **a**kacheka sana, **a**kamwambia leo
> Leo umefika siku nzuri, mbinguni utaenda, na Jehanamu utaenda
> Mzee Tupatupa **a**kasema
> “Yes! Hilo ndilo neno.”
> Basi, malaika **a**kamwambia, “Kwanza tunaanza kukupeleka Jehanamu.”…

Uchanganuzi huu unadhihirisha kuwa wimbo wa *Tupatupa* umehusisha msimulizi ambaye si mshiriki katika usimulizi anaosimulia. Hata hivyo, msimulizi anaonekana kuwa na ujuzi mkubwa kuhusu matendo ya mhusika Tupatupa pamoja wa wahusika wengine wanaopatikana katika usimulizi wenyewe. Mhusika huyu Tupatupa anasimuliwa na msimulizi kuanzia mwanzo hadi mwisho. Msimulizi ana ufahamu mkubwa wa mhusika huyu, kwa kufahamu hulka zake, uzoefu wake na matendo yake. Kuna matumizi ya kiambishi cha mofu “a” kumrejelea mhusika Tupatupa.

Mbali na kuwepo kwa matumizi ya kiambishi mofu cha nafsi ya tatu, kuna maneno vilevile ambayo yanarejelea uwepo wa wahusika wa nafsi ya tatu. Kwa mfano, maneno “alilewa” pamoja na “aliona” yanamrejelea mhusika wa nafsi ya tatu ambaye ni Tupatupa. Maneno haya yanaonyesha kuwa Tupatupa ndiye yambwa tendewa katika usimulizi huu, kwani ndiye anayepokea athari ya kitendo.

Waaidha, kuna wahusika wengine ambao wanarejelewa kwa matumizi ya vipashio vya nafsi ya tatu. Kwa mfano, mhusika ambaye ndiye dereva wa lori lililomgonga Tupatupa anarejelewa na maneno kama “hakuwa” pamoja na “alijaribu”. Ingawa maneno yanayomrejelea Tupatupa na yale yanayomrejelea dereva wa lori yameanza kwa kiambishi cha nafsi ya tatu “a”, yanarejelea wahusika wawili tofauti.

Mhusika malaika vilevile anadhihirika kuwakilishwa kwa nafsi ya tatu. Maneno yanayomrejelea Malaika yametangulizwa kwa kiambishi cha nafsi ya tatu “a”, kwa mfano, “akatokea” na “akamuuliza”. Mwisho, kwa kurejelea dondoo hili, kuna matumizi ya kiashiria cha nafsi ya tatu “yule”, kinachomrejelea mhusika Malaika.

Fludernik (1993) anahoji kuwa usimulizi wa aina hii unaweza kuwa na mwingiliano na simulizi za nafsi nyingine tofauti. Hali hii inajitokeza katika wimbo wa *Maamuzi,* unaosheheni usimulizi wa nafsi zote tatu. Tazama mfano huu;

Mfano 9: *Maamuzi*

…Tundo **a**lilia **a**kasema, “Mwili **wangu** wote
Sasa umebadilika.”
Rangi ya ngozi **yake** Tundo
Iligeuka ikawa gamba la nyoka mwili **wake** mzima
Siku moja marafiki **zake**
Waka**m**tembelea Tundo
Wakalia sana wakamwambia ndugu **yetu** Tundo
Tuna muhubiri **a**nahubiri twende

Ukaombewe Tundo

Kuna matumizi ya vipashio vya nafsi ya tatu kwa kurejelea dondoo hili. Matumizi ya viambishi vya nafsi ya tatu vinadhihirisha wahusika ambao wanasimuliwa katika usimulizi huu. Kwanza, usimulizi huu unasimulia kuhusu mhusika Tundo. Maneno kama “alilia” na “akasema” yametangulizwa kwa kiambishi cha nafsi ya tatu “a” kumdhihirisha yeye Tundo kama mhusika wa nafsi ya tatu. Mbali na Tundo, marafiki wake pia wanawasilishwa kwa kutumia vipashio vya nafsi ya tatu. Maneno yanayorejelea marafiki wa Tundo, kama “wakamtembelea”, “wakalia” na “wakamwambia” yanaonyesha hali ya wingi ya kiambishi cha nafsi ya tatu “a”.

Mbali na viambishi, pia kuna vimilikishi vya nafsi ya tatu ambavyo vimedhihirika katika dondoo hili. Kwa mfano, sehemu “mwili wake mzima…” pamoja na “marafiki zake…” zinadhihirisha matumizi ya mzizi –ake ambao kimsingi huwakilisha na kuvumisha nafsi ya tatu. Muhubiri vilevile ni mhusika mwengine wa nafsi ya tatu anayewakilishwa na neno lenye msingi wake katika nafsi ya tatu. Kwa mfano, neno “anahubiri” linamrejelea muhubiri huyu. Kwa kurejelea ithibati hizi, inabainika kuwa usimulizi huu ni wa nafsi ya tatu kwa kuwepo matumizi ya vipashio vya nafsi hiyo.

Kwa kurejelea dondoo hili, mkondo wa usimulizi unabadilika kutoka katika nafsi ya tatu ya usimulizi, na kutumia nafsi ya pili na vilevile nafsi ya kwanza. Kubadilika huku kunadhamiria kukidhi mahitaji ya muktadha unaotumika kwa wakati huo. Kubadilika kwa mkondo wa usimulizi kutoka nafsi moja hadi nyingine huondoa uzoefu wa kusimulia kwa mtindo mmoja na hivyo kuwezesha hadhira kufasili vyema matukio katika simulizi, kama anavyohoji Stanzel (1984).

4.2 Mahusiano ya Wakati wa Usimuliaji

Matukio katika simulizi hutendeka kiwakati. Arege (2012) akimnukuu Genette (1980) anayeeleza kuwa simulizi hutambulishwa katika wakati fulani kuhusiana na kitendo cha usimuliaji. Arege

(keshatajwa) anasema kwamba sifa hii ya simulizi husababisha kuwepo kwa aina tatu za usimuliaji wa matukio; usimuliaji wa wakati uliopita, uliopo na ujao.

Umbali kati ya hadithi na usimuliaji hutambulishwa na wakati. Matendo katika simulizi husimuliwa kiwakati; kabla ya kutendeka, wakati yanapotendeka, baada ya kutendeka na iwapo kuna uchangamano wa matukio kusimuliwa yakitendeka. Sehemu hii ya utafiti imejadili mahusiano ya wakati wa usimulizi kwa kurejelea usimulizi baadaye, usimulizi kabla, usimulizi sawia na usimulizi zongomezi.

4.2.1 Usimulizi baadaye

Genette (1980) anaeleza usimulizi baadaye kuwa matukio yanayosimuliwa baada ya kumalizika na kupita. Aghalabu, kiambishi cha wakati uliopita “li” hutumiwa katika kuendeleza usimulizi baadaye. Aina hii ya usimulizi inadhihirika katika wimbo wa *Maamuzi.* Msimulizi anasimulia kumhusu mhusika Tundo, ambaye matukio katika maisha yake yanasimuliwa baada ya kutendeka kwake. Tazama mfano huu;

Mfano 10: *Maamuzi*

A**li**kuwepo mama mmoja ngoja niseme
Jina lake a**li**itwa Tundo
A**li**sumbuliwa na ugumba miaka mingi
Ndoa yake i**li**kuwa matatani
Hata mawifi zake wote hawakumpenda tena

…Tundo a**li**amua kwenda kwa waganga
A**li**zunguka huku na kule kutafuta msaada
A**li**ona bora aende kwa waganga tundo
A**li**kutana na mganga mmoja nchini Congo
Akampa dawa za kutosha tundo
Tundo a**li**zaa mtoto wa kiume
Jina lake a**li**mwita Sinona
Maajabu a**li**yokuwa nayo mtoto yule
A**li**kuwa amezaliwa na meno
Maajabu a**li**yokuwa nayo Sinona
A**li**zaliwa na meno kama mtu mzima

Kwa kurejelea usimulizi huu, tukio la kukosa mtoto lilikwisha kumtendekea Tundo kabla kusimuliwa. Maamuzi yake ya kwenda kwa mganga mashuhuri kule Kongo vilevile yanasimuliwa. Msimulizi anasimulia kile kilichompata mhusika Tundo baada ya kufanikiwa kupata mwana kwa nguvu za kishirikina. Aidha, msimulizi anahusisha wahusika wengine katika kupata suluhu, kwa kuwaleta marafiki wake Tundo katika usimulizi, waliomsihi Tundo aende akaombewe ili madhara yaliyoletwa na mtoto Sinona yaishe. Matukio haya yote yanahadithiwa kwa wakati uliopita.

Mbali na usimulizi katika wimbo wa *Maamuzi*, usimulizi baadaye pia unajitokeza katika wimbo wa *Lazima Usamehe*. Matukio katika wimbo huu ni yale ya wakati uliopita, kwani masimulizi yenyewe yamesheheni wingi wa matumizi ya kiambishi cha wakati uliopita “li”. Tazama mfano huu;

Mfano 11: *Lazima Usamehe*

Ni**li**kuwa na rafiki yangu mzuri
A**li**yeugua ugonjwa wa ajabu
Kwa huruma zangu ni**ka**mhurumia
Ni**ka**tumia muda wangu mwingi
Ni**ka**zunguka huku na kule kutafuta madaktari
Ni**ka**tembea huku na kule kutafuta uzima wake
Lakini Mungu si mwanadamu, A**li**nihurumia
A**ka**achilia uzima mwoyoni mwake a**ka**wa mzima
Ni**ka**tafuta ata wachungaji nao wa**ka**mwombea…
Cha kushangaza a**li**popona, malipo yangu
A**li**geuka adui yangu
Amekuwa msiba kwangu…
Siwezi kumsamehe huyu

Kwa kurejelea dondoo hili, kuna maneno mengi ambayo yamejitokeza katika wakati uliopita. Baadhi ya vitenzi ambavyo vimetumiwa katika usimulizi huu vina kiambishi cha wakati uliopita “li” kudhihirisha kuwa yanayosimuliwa ni yaliyotendeka kabla ya wakati huo. Baadhi ya maneno haya ni kama; “nilikuwa”, “nikamhurumia”, “nikazunguka” na kadhalika.

Kama inavyojitokeza, msimulizi alikwisha kutendewa mambo anayosimulia. Anadai kuwa hawezi kumsamehe rafiki yake ambaye kabla kupona, alimsaidia sana katika juhudi za kupata uzima. Usimulizi huu unadhihirika kuwa usimulizi baadaye.

4.2.2 Usimulizi kabla

Kulingana na Manfred (2005), katika usimulizi kabla, matukio husimuliwa kabla ya kutendeka kwake. Usimulizi huu huchukua sifa za ubashiri au ndoto. Katika usimulizi huu, viambishi ambavyo hutamalaki kwa wingi ni vile vya wakati ujao “ta” pamoja na “ki” ya uwezekano wa matukio kutendeka kwa wakati ujao. Wimbo wa *Ahabu* umedhihirisha matumizi ya usimulizi kabla. Tazama mfano huu;

Mfano 12: *Ahabu*

…Ilifika wakati Elia akasema
Waitwe manabii wote mia na hamsini
Kama Baali ni Mungu basi leo
Tu**ta**mwabudu
Na kama Mungu yupo basi leo tu**ta**mjua

Wakajikusanya mabaalia wote
Mia nne na hamsini wakaanda sadaka yao
Ya kuteketezwa
Elia akawaambia Iteni Mungu
Lakini Mungu wa Baali hakushuka tena
Elia akawaambia Muamusheni
Mungu wa Baali hakuamuka
Baali hakuamuka na wala hakuwasaidia
Elia akasimama tena
Akaandaa sadaka yake
Akawaambia leteni maji
Sadaka yangu imwagiliwe
Akajipiga kifua chake
Na ujulikane Mungu wa Elia
Moto kutoka mbinguni ulishuka
Ulibeba sadaka ya Elia kila kitu
Wale miungu wa Baali wote
Walitetemeka…

Kwa kurejelea dondoo hili, msimulizi anatumia vitenzi vilivyo na kiambishi cha wakati ujao “ta” ili kubashiri yatakayotendeka hapo baadaye. Yanajitokeza maneno ambayo yanaonyesha kuwa kitendo kingali kutokea. Kwa mfano, neno “waitwe” kinadhihirisha wazi kuwa manabii waliohitajika hawakuwa wamefika walikohitajika. Vilevile, matumizi ya neno “tutamwabudu” inadhihirisha kuwa kitendo hiki kitafanyika baadaye. Maneno mengine ambayo yamesadifu matumizi ya usimulizi kabla ni kama “Iteni”, “muamusheni” pamoja na “leteni”.

Katika usimulizi huu, Elia anawaamuru manabii wa Baali waje waombee dhabihu yao ili miungu yao ishushe moto, naye Elia pia aombee dhabihu yake ili Mungu wake ashushe moto. Yule atakayeshusha moto kati ya miungu ya Baali na Mungu wa Elia, ndiye atakayeabudiwa. Hivyo basi, tukio la kujua Mungu wa kweli linasimuliwa na ilhali bado halijatendeka. Huu ni mfano wa usimulizi kabla.

Wimbo wa *Dunia haina huruma* vilevile unadhihirisha matumizi ya usimulizi kabla. Ingawa sehemu kubwa ya usimulizi wake inadhihirisha matukio yaliyokwisha kufanyika, kuna sehemu ndogo ya usimulizi huu inayosheheni sifa ya usimulizi kabla, kwani kuna ubashiri wa matukio. Tazama mfano huu;

Mfano 13: *Dunia haina huruma*

…Ninamuomba dakitari
Dakitari naomba nisaidie
Mume wangu a**ki**pona
Gharama zote tu**ta**lipa
Na kama la hajapona
U**ta**chukua gari langu

Kwa kurejelea usemi huu wa msimulizi, matukio yanayosimuliwa ni yale ambayo bado hayajatendeka bali yanayobashiriwa kuwa huenda yakatendeka baadaye. Hii ndiyo sababu kuna

matumizi ya kiambishi cha wakati ujao “ta” katika neno “tutalipa” na “utachukua” pamoja na kiambishi maalum cha masharti “ki” katika neno “akipona”, cha matukio ambayo huenda yakatokea baadaye. Mumewe msimulizi angali mgonjwa mahututi, hajapona. Msimulizi anamweleza dakitari kuwa iwapo atapona, basi malipo yatafanywa, na iwapo hatapona, basi msimulizi atamwachia dakitari gari lake. Huu ni mfano mwafaka wa usimulizi kabla.

4.2.3 Usimulizi sawia

Kulingana na Genette (1980), usimulizi sawia husimulia matukio wakati uo huo yanapotokea. Aghalabu katika usimulizi wa aina hii, kiambishi cha wakati uliopo “na” pamoja na kiambishi cha hali ya matukio kuendelea “ki” hutumika katika kiwango kikubwa. Usimulizi huu unajitokeza katika wimbo wa *Dunia haina huruma*. Tazama mfano huu;

Mfano 14: *Dunia haina huruma*

…**Ni** asubuhi na mapema
Simu ya mkononi i**na**ita
Naitazama kwa makini
Ni namba ya mume wangu
Sauti ya mwanamke i**na**sikika
I**na**yorarua moyo wangu
Moyo wangu u**na**fura hasira
Kwa taarifa ni**na**zopata…

…**Na**watafuta ndugu na jamaa
Waliokuwa kwenye simu yangu
Ili niwaambie taarifa hizi
Zi**na**zorarua moyo wangu…

…Ni**na**fika hospitali
Ni**na**wakuta watu wa mochwari
Maneno wa**na**yoniambia
Ya**na**umiza moyo wangu…

Msimulizi anasimulia kuhusu matukio yanayoendelea kutukia katika maisha yake. Msimulizi hana uwezo wa kubashiri yatakayomtukia baadaye katika usimulizi wake kwani anasimulia katika

wakati uo huo matukio hayo yanapotendeka. Kiambishi cha wakati uliopo “na” kinajitokeza kutumiwa pakubwa katika kufanikisha usimulizi huo. Jinsi matukio yanavyofuatana katika wakati uliopo, inadhihirisha matumizi ya usimulizi sawia. Kwa mfano, maneno kama “inaita”, “inasikika”, “ninawakuta” na kadhalika yanadhihirisha usawia wa masimulizi kwani yana kiambishi cha wakati uliopo “na”. Vilevile, kitenzi kishirikishi kipungufu “ni” katika mshororo wa kwanza wa ubeti wa kwanza wa dondoo unadhihirisha kuwa kitendo kiko katika harakati ya kutendeka. Maneno mengine yaliyotumiwa, kama “nawafuata” na “naitazama”, vilevile yanadhihirisha usawia wa masimulizi.

Usimulizi sawia vilevile unajitokeza katika wimbo wa *Unatisha*. Masimulizi haya yanasimuliwa katika wakati uliopo moja kwa moja jinsi yanavyotukia. Tazama mfano huu;

Mfano 15: *Unatisha*

U**na**tisha
U**na**tisha Bwana
Wewe ni Mungu, U**na**tisha

…Musa a**na**watawala wana wa Israeli
Wa**na**fika karibu na bahari ya Shamu
Wakigeuka nyuma wa**na**ona jeshi
La Farao li**na**kuja…

Musa a**na**fika mbele ya
A**na**iona bahari
Wote wa**na**mgeukia…

Kwa kurejelea usimulizi huu, baadhi ya vitenzi vinadhihirisha usawia wa vitendo au masimulizi. Neno “unatisha” linadokeza kitendo ambacho kinatendeka. Vilevile, maneno “anawatawala”, “wanafika”, “anaiona” pamoja na “wakigeuka” yanadhihirisha matukio wakati huo yanapotukia na kuripotiwa.

4.2.4 Usimulizi zongomezi

Genette (1980) anadokeza kuwa katika usimulizi wa aina hii, muda wa utendaji wa matukio huandamana na kubadilishana nafasi katika hadithi. Hujitokeza kuwa usimulizi ulio changamano kwani hali na nyakati hubadilikabadilika. Sifa za usimulizi kabla, usimulizi baadaye na usimulizi sawia hujitokeza katika matini moja, hivyo kuashiria mchangamano wa nyakati na hali hizi. Kwa mfano, katika matini moja, msomaji anaweza kukumbana na viambishi wakati “li”, “na” pamoja na “ta”. Hali hii imejitokeza katika wimbo wa *Maamuzi*. Tazama mfano huu;

Mfano 16: *Maamuzi*

…Tundo a**ka**ondoka na mtoto wake
Huku tatizo la utasa li**me**kwisha
Na kufurahia kumwona mtoto
A**li**pokuwa mhubiri a**ki**hubiri
A**li**mwona Tundo mbele yake
A**ka**mwambia mama njoo mbele
Tundo a**ka**sogea a**ki**jua muujiza u**me**fika

Dondoo hili lina mchangamano wa nyakati na hali tofauti katika wakati mmoja wa matukio. Kiambishi “ka” katika neno “akaondoka” kinaonyesha kitendo katika hali ya kuendelea, kiambishi “me” katika neno “limekwisha” ni kiambishi cha hali timilifu, kiambishi “li” katika neno “alipokuwa” ni cha wakati uliopita. Aidha, neno “njoo” linadhihirika kutumia usimulizi kabla. Kuwepo kwa uchangamano wa aina hii kunadhihirisha usimulizi zongomezi.

Usimulizi changamano vilevile unadhihirika katika wimbo wa *Ahabu*. Baada ya Elia kuomba, moto mkubwa ulishuka na kuteketeza sadaka yake. Kwa kuwa moto uo huo haukushuka walipoomba manabii wa Baali, inadhihirisha kuwa Mungu wake Elia ndiye alikuwa Mungu wa kweli. Baadaye, Elia anawaangamiza manabii wote wa Baali kwa kuwa manabii haramu. Habari hizi zinapomfikia Jezebeli, mkewe Ahabu, anaapa kumuua Elia kabla ya wakati huo wa siku

itakayofuata. Matukio haya, jinsi yanavyosimuliwa, yanadhihirisha uzongomezi wa usimulizi. Tazama mfano huu;

Mfano 17: *Ahabu*

…Wale manabii wa Baali wote walitetemeka
Elia aliwaua wote hawakuweza kumsogelea
Jezebeli akatuma mjumbe
Nenda kamwambie Elia
Kesho majira kama haya
Roho ya Elia itakuwa mikononi mwangu
Maneno ya Jezebeli yalimnyima usingizi Elia…

Dondoo hili linadhihirisha uchangamano wa matukio kwa kutumia nyakati na hali tofauti. Kuna matumizi ya viambishi vya nyakati na hali tofauti katika matini moja. Kwa mfano, neno "walitetemeka" linadhihirisha usimulizi baadaye, kwa kutumia kiambishi cha wakati uliopita "li". Aidha, kuna matumizi ya neno "akatuma" ambalo linadhihirisha kuwa kitendo kinatendeka kwa wakati kinaposimuliwa, hivyo basi kuwa usimulizi sawia. Vilevile, kuna matumizi ya neno "itakuwa" kudhihirisha matukio ambayo yatatendeka katika wakati ujao, hivyo kuainishwa kama usimulizi kabla. Uchangamano wa nyakati na hali unadhihirisha matumizi ya usimulizi zongomezi.

4.3 Hitimisho

Sura hii imehakiki kipengele cha sauti ya usimuliaji katika simulizi zinazopatikana katika nyimbo teule za Bahati Bukuku. Sehemu hii ya utafiti ilianza kwa kufafanua maana ya sauti ya usimuliaji kwa kuwarejelea wataalamu mbalimbali wa kinaratolojia. Utafiti huu vilevile ulihakiki mitazamo ya wananaratolojia wawili, Genette (1980) pamoja na Stanzel (1984). Mtazamo wa Genette (keshatajwa) ulihakikiwa kwa kutathmini vijenzi vyake vya usimuliaji wa ndani na wa nje. Mtazamo wa Stanzel (keshatajwa) ulihakikiwa kwa kutathmini vijenzi vyake; usimulizi wa nafsi ya kwanza, nafsi ya pili na nafsi ya tatu. Mbali na mitazamo ya wananaratolojia hawa, mahusiano

ya wakati wa usimulizi yalihakikiwa huku mifano yake ikitolewa kwa kurejelea nyimbo teule za Bahati Bukuku. Vipengele vya mahusiano ya wakati wa usimulizi vilevile vilihakikiwa, vikiwemo; usimulizi baadaye, usimulizi kabla, usimulizi sawia na usimulizi zongomezi.

Sura inayofuata inahusu hitimisho la sura zote za utafiti huu, kuanzia sura ya kwanza hadi tano. Muhtasari wa utafiti, matokeo, mchango wa utafiti, changamoto zinazokabili utafiti pamoja na mapendekezo ya utafiti ndizo sehemu kuu zitakazohakikiwa.

SURA YA TANO

MUHTASARI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

5.0 Utangulizi

Sura hii inahusu muhtasari, matokeo pamoja na mapendekezo ya utafiti. Sura hii imegawanywa katika vitengo vitano; kitengo cha kwanza kimezingatia muhtasari wa utafiti, kitengo cha pili kimezingatia matokeo ya utafiti, kitengo cha tatu kimeshughulikia mchango wa utafiti, cha nne kimezingatia changamoto zilizokumba utafiti na cha tano kimezingatia mapendekezo ya utafiti. Utafiti huu umefanywa kwa msingi wa nadharia ya naratolojia.

5.1 Muhtasari wa utafiti

Utafiti uliofanywa ulichanganua jinsi mbinu ya usimulizi ilivyojitokeza kama mtindo katika nyimbo teule za msanii wa nyimbo za kidini, Bahati Bukuku. Utafiti ulilenga kueleza jinsi usimulizi ulivyojitokeza katika nyimbo teule kwa kuzingatia mfuatano wa matukio na wakati. Utafiti vilevile ulilenga kudhihirisha usimulizi kama njia mojawapo ya kuwasilisha maudhui. Mwisho, utafiti ulilenga kufafanua jinsi sauti ya usimuliaji na mahusiano ya wakati wa usimulizi ilivyojitokeza katika nyimbo teule za Bahati Bukuku. Nyimbo zilizochaguliwa kutumika katika utafiti huu ni zile tu zilizopatikana kuwa na sifa za kihadithi. Kwa mfano: mianzo inayodhihirisha simulizi, mfuatano wa matukio kama ilivyo katika simulizi, upeo wa chini na upeo wa juu ambazo hujitokeza katika simulizi, mfuatano mahsusi wa matukio pamoja na miisho maalum iliyodhihirisha kuwa simulizi katika nyimbo hizo zilikuwa zimetamatika.

Tasnifu hii imewasilishwa katika sura tano. Sura ya kwanza ilishughulikia usuli wa mada kwa kudhihirisha nafasi wazi iliyokusudiwa kuzibwa na utafiti huu. Utafiti ulidhihirisha suala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada ya utafiti, upeo na mipaka ya

utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti, msingi wa nadharia, mbinu za utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data pamoja na uwasilishaji wa matokeo. Katika kuafikia malengo ya utafiti huu, nyimbo kumi zilizo na sifa za kihadithi ziliteuliwa. Hizi ni nyimbo zilizotangulizwa kwa njia maalum kisimulizi, zilizoambatanisha matukio kisimulizi, zilizokuwa na upeo wa chini pamoja na kilele, zilizowasilisha maudhui maalum kwa mtindo wa usimulizi pamoja na zilizotamatika kwa njia maalum kisimulizi. Nyimbo za *Abneli, Ahabu, Barthimayo, Mbeba maono, Unatisha* pamoja na *Waraka* ziliondolewa kutoka katika *Maandiko Matakatifu* ilhali nyimbo za *Maamuzi, Dunia haina huruma, Lazima usamehe* pamoja na *Tupatupa* zilibuniwa moja kwa moja kama simulizi katika nyimbo.

Sura ya pili ilichanganua jinsi usimulizi ulivyodhihirika katika nyimbo teule kwa kuzingatia mfuatano wa matukio na dhana ya wakati. Sura hii ilianza kwa kufafanua dhana ya usimulizi kwa kujikita katika maoni ya wataalamu mbalimbali waliohakiki usimulizi pamoja na vipengele vyake mbalimbali. Waaidha, sura hii ilizingatia vipengele viwili muhimu ambavyo hufanikisha uwasilishaji wa simulizi; ploti na wakati. Uchanganuzi wa kipengele cha ploti ulianza kwa kuzingatia maoni ya wataalamu mbalimbali walioshughulikia ploti pamoja na sifa zake. Baadaye, uchanganuzi wa ploti ulirejelea matumizi ya vipengele vyake muhimu kama; kuwepo kwa utangulizi maalum, tamati maalum, nafasi ya mhusika mkuu katika usimulizi pamoja na kilele cha usimulizi. Maoni ya wataalamu yalitolewa kwa utendeti kuhusu vipengele hivi vya ploti.

Mbali na kigezo cha ploti, sura ya pili ya utafiti huu vilevile ilichanganua kigezo cha wakati kama kipengele muhimu cha kuhakiki simulizi. Katika kuhakiki wakati, utafiti ulichanganua vipengele vitatu muhimu; umara, muda pamoja na mpangilio. Maoni ya wataalamu kuhusu vipengele vya wakati yalitolewa kwa utendeti pamoja na mifano mwafaka kutoka kwa nyimbo teule kutolewa. Utafiti ulibaini kuwa vipengele hivi vya wakati vina mihimili yake. Mihimili iliyofafanuliwa

katika kipengele cha umara ilikuwa usimulizi rudufu, usimulizi banifu na usimulizi mosi. Kipengele cha muda kilihakiki sehemu zake nne; muhtasari, udodoshi, onyesho na mtuo. Kipengele cha mpangilio kilihakiki aina zake; analepsia na prolepsia.

Sura ya tatu ililenga kufafanua usimulizi kama njia mojawapo ya kuwasilisha maudhui. Sura hii ilihakiki maudhui mbalimbali yaliyojitokeza katika nyimbo teule za Bahati Bukuku. Sura hii ya tatu ilianza kwa kutoa ufafanuzi wa dhana ya maudhui kwa kuwarejelea wataalamu mbalimbali wa kifasihi. Sura hii vilevile ilihakiki maudhui mbalimbali ambayo yalipatikana katika nyimbo teule za utafiti. Maudhui yaliyofafanuliwa yalikuwa; Imani ya dini, unafiki, msamaha, nafasi ya marafiki katika maisha ya mja, ushirikina, anasa pamoja na nafasi ya mwanamke katika jamii. Mifano maridhawa ilitolewa kutoka kwenye nyimbo teule Ili kutetea maudhui haya.

Sura ya nne ililenga kubainisha jinsi sauti ya usimuliaji na mahusiano ya wakati wa usimulizi yalidhihirika katika nyimbo teule za utafiti. Sura hii ilianza kwa kutoa ufafanuzi kuhusu sauti ya usimuliaji. Maoni mbalimbali yaliyotolewa na wataalamu wa kinaratolojia yalielezwa kwa utendeti ili kurahisisha uelewaji wa dhana ya sauti ya usimuliaji. Ingawa utafiti ulifafanua maoni ya wananaratolojia mbalimbali, ulijikita katika mtazamo wa Stanzel (1984) aliyehakiki sauti ya usimuliaji kwa kurejelea nafsi tatu za usimuliaji; nafsi ya kwanza, nafsi ya pili na nafsi ya tatu. Katika kufafanua nafsi hizi za usimuliaji, maoni ya wananaratolojia wengine yalikuwa na umuhimu mkubwa katika kujenga maoni ya Stanzel (keshatajwa). Mifano mwafaka ilitolewa kutoka katika nyimbo teule za utafiti ili kuonyesha wazi jinsi nafsi za usimuliaji zilivyodhihirika.

Sura hii vilevile ilichanganua dhana ya mahusiano ya wakati wa usimulizi kwa kuhakiki vipengele vyake muhimu; usimulizi baadaye, usimulizi kabla, usimulizi sawia na usimulizi zongomezi (changamano). Maoni ya wataalamu wa kinaratolojia vilevile yalitolewa kwa utendeti ili kusaidia

vyema katika kuelewa dhana hii ya mahusiano ya wakati wa usimulizi. Mifano mwafaka ilitolewa kutoka katika nyimbo teule zilizotumia vipengele vya mahusiano ya wakati wa usimulizi.

Sura ya tano imeshughulikia hitimisho la utafiti wote kwa kueleza muhtasari wa sura zote za utafiti, matokeo ya utafiti pamoja na changamoto zilizokumba utafiti huu. Sura ya tano vilevile imetoa mapendekezo kuhusu tafiti zinaziweza kufanywa na watafiti wengine katika wakati ujao. Maelezo kuhusu sura zote yametolewa kwa mujibu wa malengo ya utafiti.

5.2 Matokeo ya utafiti

Malengo ya utafiti huu yalikuwa kueleza jinsi mbinu ya usimulizi imejitokeza katika nyimbo teule za Bahati Bukuku.Malengo yalizingatia mfuatano wa matukio, wakati, uwasilishaji wa maudhui, sauti ya usimuliaji na mahusiano ya wakati wa usimulizi. Utafiti ulibainisha kuwa nyimbo teule zenye sifa za kihadithi zilizowasilishwa na Bahati Bukuku zimehusisha sifa, vipengele na mitazamo ya usimulizi katika sehemu mbalimbali.

Utafiti uligundua kuwa nyimbo teule zinasheheni sifa muhimu zinazotambulika kufanikisha mfuatano wa matukio (ploti) kifasihi. Ilibainika kuwa sehemu ya utangulizi maalum ni muhimu sana katika kufanikisha uwasilishaji wa simulizi. Baadhi ya manufaa ya utangulizi maalum yalielezwa kuwa: kuwavutia wasikilizaji, kuteka makini ya hadhira, kumtambulisha mwimbaji kwa hadhira, kuashiria mwanzo wa wimbo pamoja na kutoa hadhira kutoka ulimwengu halisi na kuwaweka katika ulimwengu wa mwimbaji. Utafiti uligundua kuwa msanii Bahati Bukuku alitumia mtindo wake binafsi katika kutanguliza hadithi, kwani itikadi ya kutanguliza simulizi kwa fomyula maalum haikutiliwa maanani. Msanii Bukuku alitanguliza simulizi katika nyimbo zake kwa kutumia mafumbo ambayo yalisaidia katika kuelewa dhamira yake ya utunzi wa nyimbo hizo. Vilevile, mianzo yake ilibainisha baadhi ya maudhui ambayo alinuia kuwasilisha katika simulizi

hizo. Wa aidha, tangulizi zilizotumiwa zilitilia msisitizo katika baadhi ya matukio ambayo yalijitokeza simulizini.

Utafiti ulibainisha kuwa usimulizi haufai kuanza ghafla wala kukamilika ghafla, bali huhitimishwa kwa upeo wa chini na wa aina ya kipekee. Manufaa mbalimbali ya kuhitimisha simulizi kwa njia maalum yalielezwa kuwa; kuashiria kumalizika kwa utambaji, kuwa kama kitangulizi cha shughuli nyinginezo, kuashiria kupewa nafasi kwa mtambaji anayefuata pamoja na njia maalum ya kuituliza hadhira na kutoa fikra zao katika utambaji unaoisha. Utafiti vilevile ulibainisha nafasi muhimu inayotwaliwa na mhusika mkuu katika usimulizi. Huyu ni mhusika ambaye uhusika vikamilifu katika vitushi vya usimulizi, kuanzia mwanzo hadi mwisho. Kilele cha usimulizi pia kilijitokeza kuwa sehemu muhimu sana katika ploti ya usimulizi. Kilele hiki kilielezwa kuwa upeo wa juu ambapo kitendo kinachosubiriwa kwa hamu hutendeka. Utafiti ulibaini kuwa kilele ndicho hutosheleza matarajio ya hadhira.

Utafiti huu ulichanganua nafasi ya wakati katika usimulizi kwa kuhakiki vipengele vya wakati, kama vile umara, muda pamoja na mpangilio. Kwa kuhakiki vipengele hivi, utafiti ulinuia kuonyesha jinsi matukio katika simulizi zinazopatikana katika nyimbo teule za Bahati Bukuku huweza kupangwa, jinsi matukio hujitokeza katika muda maalum na kuwa matukio katika simulizi lengwa hujitokeza mara ngapi. Kupitia kipengele cha idadi ya utokeaji wa matukio katika wimbo, ilidhihirika kuwa baadhi ya matukio katika simulizi za nyimbo teule hujitokeza mara moja na yakasimuliwa zaidi ya mara moja, huku mengine yakitokea zaidi ya mara moja na yakasimuliwa mara moja. Kwa mfano, kuhuzunika kwa msimulizi katika usimulizi wa *Dunia haina huruma* kulifanyika mara moja, ila kukasimuliwa mara kadhaa. Utafiti ulibaini kuwa mtunzi wa simulizi hupanga matukio yakajirudia kwa sababu zifuatazo: kutoa msisitizo wa mambo yanayorudiwa ili kumsaidia msilikizaji kubaini maudhui yanayowasilishwa, kuwasilisha dhamira ya mtunzi pamoja

na kufanikisha tamathali ya *takriri* ambayo ni mojawapo kati ya tamathali ambazo hufanikisha uwasilishaji wa kazi za kifasihi.

Waaidha, ilibainika kuwa iwapo matukio yaliyojitokeza katika simulizi lengwa zaidi ya mara moja yatasimuliwa, basi hujitokeza tofauti katika miundo ya kisarufi bila kupoteza maana. Kipindi kilichochukua tukio fulani katika usimulizi kutokea kinabainika kuwa muhimu sana katika usimulizi. Utafiti ulibaini kuwa iwapo matukio yote katika usimulizi yangeweza kusimuliwa, basi ingechukua muda mrefu sana kwa usimulizi kukamilika. Hivyo, inabidi matukio kufupishwa au kudondoshwa. Utafiti vilevile ulibaini kuwa usimulizi hupangwa kwa njia maalum, kuanzia mwanzo wa tukio hadi mwisho. Hata hivyo, wakati mwengine matukio yanaweza yakabadilishwa na mpangilio maalum kukiukwa.

Katika sura ya tatu, utafiti ulibaini kuwa kuwa usimulizi una nafasi kubwa katika uwasilishaji wa maudhui. Ilibainika kuwa hakuna usimulizi ambao unaweza kufanikishwa pasipo kuwepo na mawazo makuu yanayowasilishwa kupitia masimulizi yenyewe. Aidha, ilibainika kuwa malengo pamoja na wahusika wanaotumiwa katika kazi ya fasihi hutegemea pakubwa katika maudhui yaliyowasilishwa. Vipengele vya: uhusika, ploti na mandhari yalibainishwa kuwa muhimu katika uwasilishaji wa maudhui. Utafiti ulibainisha vipengele ambavyo vilisaidia kuunda maudhui tofauti katika nyimbo teule. Maudhui yalielezwa kuwa ujumbe wa jumla ambao hujitokeza katika kazi ya fasihi. Utafiti ulieleza kuwa maudhui na dhamira hushirikiana katika kutekeleza wajibu wa kuwasilisha ujumbe, kwani katika kuwasilisha dhamira ya kazi ya fasihi, maudhui hushirikishwa moja kwa moja. Utafiti ulieleza kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya maudhui na mtindo kwani mtindo ambao hutumiwa katika kubuni na kuwasilisha fasihi ndiyo humwezesha msanii kuwasilisha maudhui yake. Utafiti ulifafanua kuwa ubunifu wa mtunzi pamoja na uwezo wake wa kuteua mbinu bora za uandishi humwezesha kuwasilisha maudhui faafu.

Katika sura ya nne, utafiti ulihakiki vipengele muhimu vya usimulizi; sauti ya usimuliaji na mahusiano ya wakati wa usimulizi, kwa kurejelea nyimbo teule. Utafiti ulibaini umuhimu wa sauti ya usimuliaji katika simulizi zilizopatikana katika nyimbo teule za Bahati Bukuku. Utafiti huu ulijikita katika maoni ya Stanzel (1984) aliyependekeza ufafanuzi wa sauti ya usimuliaji katika nafsi ya kwanza, nafsi ya pili na nafsi ya tatu. Stanzel (keshatajwa) alifafanua kuwa sauti ingeweza kujitokeza moja kwa moja kutoka kwa msimulizi, ambaye vilevile ni mhusika mmojawapo wa kazi hiyo ya fasihi au ikajitokeza kutoka kwa msimulizi ambaye anajipata nje ya usimulizi ila ana ufahamu mkubwa sana wa matukio yote yanayotokea simulizini. Utafiti ulibaini kuwa katika usimulizi wa nafsi ya kwanza, aghalabu kiambishi cha nafsi "ni" na "tu" hujitokeza katika umoja na wingi mtawalia, kama ilivyojitokeza katika wimbo wa *Dunia haina huruma* ambapo maneno kama "Ninawatazama" na "Ninawapigia".

Katika usimulizi huu, msimulizi hujitokeza kuwa mmoja kati ya wahusika wengine walio katika usimulizi. Utafiti huu pia ulibaini kuwa usimulizi wa nafsi ya pili huwa tegemezi, kwani haujisimamii kivyake ila kwa kuambatanishwa na nafsi ya kwanza pamoja na nafsi ya tatu. Ilibainika vilevile kuwa msimulizi katika nafsi ya tatu husimulia akiwa nje ya usimulizi. Mbali na msimulizi aliye nje ya ulimwengu wa masimulizi, ilibainika kuwa mhusika mojawapo anaweza kupewa nafasi ya kusimulia hadithi, huku akiwarejelea wahusika wengine kwa kutumia kiambishi cha nafsi ya tatu "a" katika umoja na "wa" katika wingi.

Utafiti vilevile ulibaini kuwa simulizi hutambulishwa kwa wakati fulani kuhusiana na kitendo cha usimuliaji. Matendo katika simulizi huwasilishwa kiwakati kabla ya kitendo kufanyika, wakati kitendo kingali kinafanyika, baada ya kitendo kufanyika na iwapo kuna uchangamano wa kiwakati kitendo kinapofanyika.

5.3 Mchango wa utafiti

Utafiti huu utakuwa wenye manufaa kwa wasomaji wa kitaaluma, waandishi wa kifasihi, watunzi wa nyimbo pamoja na watafiti katika uwanja wa usimulizi na fasihi kwa jumla. Utafiti huu utamsaidia msomaji wa kawaida kuelewa muundo wa nyimbo na jinsi usimulizi unavyoweza kutumiwa kama mojawapo kati ya vipengele vya kimtindo katika nyimbo na fasihi kwa ujumla.

Utafiti vilevile utaweka msingi bora kati ya watunzi wa tanzu za fasihi. Usimulizi unaweza kutumiwa kama mtindo wa kutunga riwaya, tamthilia, hadithi fupi, fasihi ya watoto, nyimbo na kadhalika. Kwa hivyo, waandishi wanapotunga tanzu hizi za fasihi, wana nafasi nzuri ya kuhusisha baadhi ya vipengele vya kiusimulizi ambavyo vimeelezwa na kufafanuliwa katika utafiti huu.

Watunzi wa nyimbo vilevile watanufaika kutokana na utafiti huu. Kufanikiwa kwa wimbo hutegemea mtindo wa utunzi na uwasilishaji wa wimbo huo. Watunzi wa nyimbo wanaweza kunufaikia vipengele vya kimtindo wanavyovitumia, kwa kuiga mfano wa nyimbo za Bahati Bukuku ambazo zilitumia usimulizi katika uwasilishaji wake na kuvuma kote Afrika Mashariki. Utafiti huu aidha utawafaa watafiti watakaotafiti uwanja wa usimulizi. Baadhi ya vipengele vya usimulizi vilivyohakikiwa katika utafiti huu vitakuwa vya msaada katika uchanganuzi utakaofanywa na watafiti hao.

5.4 Changamoto zilizokabili utafiti

Utafiti huu ulikumbwa na changamoto mbalimbali. Kwanza, ikibainika kuwa utafiti huu ulikuwa wa maktabani, kulikuwa na uchache wa vitabu vya marejeleo vya Kiswahili. Kwa kuwa nadharia ya naratolojia ni ya kigeni, vitabu vingi vya marejeleo viliandikwa kwa lugha mbalimbali na kutafsiriwa katika kiingereza. Mbali na ugumu wa kupata marejeleo haya, ilimbidi mtafiti kutafsiri maneno mbalimbali ya kigeni hadi kwa Kiswahili. Aghalabu, utafsiri husababisha kupotea kwa

maana iliyokusudiwa au labda kupotoka kimaandishi. Kwa hivyo, shughuli ya kutafsiri maneno hayo ya kigeni kutoka katika vitabu na majarida yenye maandishi ya nadharia ya Naratolojia ilikuwa yenye changamoto si haba. Mbali na utafsiri, ugeni wa kutafiti usimulizi kama mtindo katika nyimbo ulileta changamoto katika kutafuta marejeleo ya tafiti zilizofanywa awali. Tafiti nyingi za kiusimulizi za awali zilizingatia riwaya, tamthilia, hadithi fupi na ushairi. Hivyo, ilimbidi mtafiti kurejelea tafiti zenye msingi katika tanzu zingine za fasihi kama zilizotajwa awali ilhali alikuwa akitafiti nyimbo.

5.5 Mapendekezo ya utafiti

Utafiti huu ulichunguza usimulizi kama mtindo katika nyimbo teule za Bahati Bukuku. Utafiti ulilenga kufafanua jinsi mbinu ya usimulizi ilivyojitokeza katika nyimbo teule kwa kuzingatia ploti na wakati, kudhihirisha usimulizi kama njia mojawapo ya kuwasilisha maudhui na kufafanua jinsi sauti ya usimuliaji na mahusiano ya wakati wa usimulizi zilivyojitokeza katika nyimbo teule za Bahati Bukuku. Kwa hivyo, kuna haja ya kufanya utafiti zaidi kwa kuchunguza vipengele vingine vya usimulizi, kwa mfano: uhusika, hali, dhamira, hali ya msimulizi, usemi na nafasi ya mtambaji, tofauti na vile vilivyofanyiwa utathmini katika utafiti huu.

Utafiti huu ulichunguza usimulizi kama mtindo katika nyimbo. Hivyo, kuna haja ya kuchunguza mbinu ya usimulizi kwa kuzingatia nyanja nyinginezo za fasihi, kwa mfano: mafumbo, vipera vya maigizo na vipera vya mazungumzo. Tafiti nyingi za mbinu ya usimulizi zimetathmini tanzu za fasihi andishi kama tamthilia, riwaya, hadithi fupi. Hivyo, kuna haja ya kufanya uchanganuzi kwa kurejelea tanzu zilizotajwa za fasihi simulizi, kwani utanzu wa ushairi na nyimbo pekee ndizo zimefanyiwa utafiti mpana. Vilevile, uwanja wa fasihi ya watoto unahitaji kuchanganuliwa kitafiti kwa msingi wa usimulizi.

5.6 Hitimisho

Sura hii ya utafiti imezingatia muhtasari wa utafiti, matokeo ya utafiti, mchango wa utafiti na changamoto zilizokumba shughuli ya utafiti. Utafiti vilevile umetoa mapendekezo kuhusu tanzu ambazo hazijafanyiwa utafiti na uwezekano wa mbinu ya usimulizi kutumiwa kufanya utafiti katika tanzu hizo.

Marejeleo

Arege, T. (2012). Narration in Swahili Narrative Poetry: An analysis of *Utenzi wa RASI 'L GHULI.* Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Aswani, B, Mayaka, G & Matinde, R. (2013). *Misingi ya Nadharia na Mbinu za Utafiti*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers, Tanzania.

Attenbernd, L. na Lewis, L. (1963). *Introduction to literature: Stories*. New York: Macmillan Company.

Bakari, M. (2008). Usemezano kama Mkakati wa Kufahamu Riwaya za *Babu alipofufuka* (2001), *Bina-Adamu* (2002) na Mkusanyiko wa Hadithi Fupi wa *Sadiki Ukipenda* (2002). Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa.)

Barry, P. (1995). *Beginning Theory*. New York: Manchester University press.

Biblia, (1952). *Maandiko Matakatifu*. Maryland: United Bible Societies.

Brogan.T.V.F.[eds] (1993) *The New Princeton Encyclopedia* of poetry and poetics. Princeton: Princeton University Press.

Chatman, S. (1990). *Coming to terms*: *The Rhetoric of Narrative in Fiction and Film.* Ithaca Cornel University Press.

Coombes, H (1953). *Literature and criticism*, London: Penguin books.

Dolozel, L. (1973). *Narrative modes in Czech literature.* Toronto: University of Toronto.

Dundes, A. (1999). *The meaning of Folklore.* Colorado: University press of Colorado.

Finnegan, R (1970). *Oral Literature in Africa*. London: Oxford University Press

Fludernik, M. (1993). *Second person fiction: Narrative 'you' as adressee and/or protagonist.* London: Routledge.

Genette, G. (1980). *Narrative Discourse*. New York: Cornell University Press.

Genette, G. (1988). *Narrative Discourse. Revisited.* New York: Cornell University Press

Gikandi, S. (1987). *Reading the African Novel*. Nairobi. Heinmann.

Gray, (2007). *The Research Imagination: An Introduction to Qualitative and Quantitative Methods.*London: Cambridge University Press.

Griffith, K. (2010). *Writing Essays about Literature*. Cengage. Wadsworth Publishers.

Hawthorn, J. (1985). *Studying the Novel: An Introduction*. New Delhi: Universal Book Stall.

https://youtu.be/WNLbTIPXQaQ. 20/04/2019.

Jones, E. (1994). *Critical Theory of African Literature Today*. London: James Curry Ltd.

Kieti, M. (1990). *The Wisdom of Kamba Oral Literature*. Nairobi: Phoenix Publishers.

King'ei, K. na Kisovi, C. (2005). *Msingi wa Fasihi Simulizi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau

Kothari, C.R. (1985) *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: Wiley Easton Limited.

Kothari, C.R. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques*, (second edition). New Delhi: New Age International Publishers.

Lanser, S. (1981). *The Narrative Act. Point of view in Prose Fiction.* Princeton. UP

Lodge, D. (1988). *Modern criticism theory*, London: Longman group limited.

Magaju, J.K. (2004). Uhalisia Ajabu katika Riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001) na *Bina-adamu* (2002). Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Manfred, J. (2005). *Narratology: A Guide to the Theory of Narrative*. Cologne: English Department, University of Cologne.

Mertens, D.N. (1998). *Research Methods in Diversity with Quantitative Approaches*. AGE Publications. London.

Mohammed, S.A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili*. East African Educational Publishers, Nairobi.

Mutwiri, G. (2005). Mitazamo ya Utendakazi wa Nyiso katika Jamii ya Watigania. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haijachapishwa.)

Mwaniki, M.W. (2011). Matumizi ya lugha katika nyimbo tohozi za Salim Junior. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa.)

Njogu, K. na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi*, Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nkonge, M (1988). Literary Study of Songs of Joseph Kimaru, Theme and Style. B.Ed Project. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa.)

Ntarangwi, M. (1990). Maudhui katika nyimbo za Remi Ongara. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa.)

Ong'ondi, B.E (2005). Uhakiki wa usimulizi katika Riwaya ya *Walenisi.* Tasnifu ya Uzamili. Chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Opondo, R. (2014). Oral Storytelling and National Kinship: Reflections on the oral narrative performance in the Kenya schools and colleges drama festivals. Tydskrif vir letterkunde, 51 (1), 102-117. University of Nairobi.

Prince, G. (1973). *A grammar of Stories*: *An Introduction.* The Hague-Paris. Walter de Gruyter.

Propp, V. (1968). *The Morphology of the Folk Tale*. The American Folk Society and Indiana University Press. Texas.

Rajweyi, A.C. (2009). Mtindo na Maudhui Katika Nyimbo Za Msanii Faustine Munishi. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa.)

Rimmon-Kenan, S (1983). *Narrative Fiction*: *Contemporary Poetics*. London: Metunen.

Rimmon-Kenan,S.(2002) *Narrative Fiction:Contemporary poetics*.London:Routledge

Raglan, L. (1956). *The Hero: A Study in Tradition Myth and Drama*. New York: Vintage Books.

Simiyu, W.F. (2015). Mwingilianotanzu Katika Fasihi Simulizi ya Kiafrika kama *Embalu* na *Mwaka Kongwa*. Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Senkoro F.E.M.K (1982). *Fasihi na Jamii*. Dar-es-Salaam: Press and Publicity Center.

Stanzel, F. (1984). *A theory of Narrative.* London*:* Cambridge University Press

TUKI, (1981). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, Nairobi: Oxford University Press.

Toolan, M.J. (1988). *Narrative, a Critical Linguistic Introduction*. London: Routledge and Kegan Paul Ltd.

Toolan, M.J. (1990). *The stylistics of fiction.* London; New York. Routledge.

Vonyoli, A.J. (2004). "Hadithi kama Chombo cha Maudhui katika Fasihi: Uchanganuzi wa riwaya za Mkangi, *Mafuta* (1984) na *Walenisi* (1995)." Tasnifu ya Uzamili. Chuo kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa.)

Wambua, M. (2001). Mtindo wa nyimbo za Kakai Kilonzo. Tasnifu ya Uzamili. Chuo kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa.)

Wambui, J. (2018). Usimulizi katika Riwaya ya *Dharau ya Ini*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Wafula, R.M. (1989). The use of Allegory in Shabaan Robert's prose works. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa.)

Wafula, R na Wanjala, L (2017). Narrative Techniques in Chinua Achebe's Things Fall Apart. Journal of Social Sciences, 50:1-3, 62-69, DOI: 10. 1080/09718923.2017.1311740

Wales, K. (1991). *A Dictionary of Stylistics*. New York: London Group UK. Limited.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa fasihi: Misingi na vipengele vyake.* Nairobi Focus Publishers (K) LTD

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na nadharia.* Nairobi: Focus books publications Ltd.

Wamitila,K.W(2008). *Kazi ya Fasihi.* Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd.

Yalwala, P. (1991). Maudhui katika nyimbo za John Mwale. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)